

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 5 Juni, 2021

(Bunge Lillanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA
MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA FEDHA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 - Wizara ya Maliasili na Utalii

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano, wapo Wabunge mbalimbali ambao watapata fursa ya kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Yahaya Omary Masare, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

Hayupo, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Fatma Hassan Taofiq ajiandae.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya, hatimaye na mimi nimeweza kusimama mahali hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii kama kuna watu wanaichonganisha Serikali na wananchi wake basi ni watu wa *TFS*. Mheshimiwa Waziri kama kuna watu ambao wanaichonganisha Serikali na wananchi ni watu wa *TFS*. Sisi Mvomero tuna Hifadhi ya Wame Mbiki. Hifadhi hii ilianzishwa miaka ya nyuma, ni hifadhi ambayo imepakana na vijiji vingi; ni hifadhi ambayo imepakana na Kata zaidi ya nne lakini shida iliyo po katika hii hifadhi ni suala la mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishamtafuta Mheshimiwa Waziri nikamweleza habari ya mipaka. Kuna wananchi wanalima, wengine kwa kujua mipaka na wengine kwa kutokujua, lakini mbaya zaidi hawa wenzetu wa *TFS* wanapowakamata hawa wananchi ambao wapo ndani ya yale maeneo, wanawapiga, wanawatesa na wanawapiga

mpaka risasi. Tunaye mwananchi mmoja amepigwa risasi hivi karibuni anaitwa Juma Shabani Bakari; amepigwa risasi zaidi ya mbili kisa amekutwa ndani ya hifadhi. Sasa hata kama ameingia ndani ya hifadhi, sheria zipo, kwa nini hapelekwi kwenye vyombo vya sheria, wanaamua kuchukua sheria mkononi na kumpiga risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaye mwananchi mwengine anaitwa Said Mwanamvua; huyu alipigwa fimbo, alinyanyaswa na walitaka kumchoma moto. Walikusanya miti wakamuingiza katikati wakataka kuwasha moto ile miti ili aweze kuungua. Sasa hao wananchi wapo Tanzania, kwenye nchi ambayo ipo huru, lakini leo wanataka kuuwawa katika nchi ambayo ni huru. Naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri katika jambo hili kwenye suala la mipaka.

Mheshimiwa Nailbu Spika, mbaya zaidi nilishawasiliana na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya nikamweleza tatizo ambalo lipo pale. Wananchi ambao wanalima yale maeneo wakati wa kulima wanaruhusiwa, wanalima vizuri, lakini wakati wa kuvuna, sasa hivi wanataka kuvunwa wanakatazwa. Wakikamatwa ndani wananyanyaswa kama nilivyo sema, lakini wakati wa kulima wanaruhusiwa walime. Nimezungumza na Mkuu wa Wilaya akaniambia mimi hayanihusu hayo mambo, waache wananchi huko wafuate taratibu ambazo zimepangwa na *TFS*. *TFS* kwenye wilaya ipo chini ya Mkuu wa Wilaya, nilishamweleza Mheshimiwa Waziri habari ya *TFS* na hawa watu wa Wame Mbiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana leo Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* atupe majibu, atueleze lini watakuja kurekebisha mipaka katika vijiji ambavyo vinapakana na Wame Mbiki. Yale maeneo ambayo tayari wananchi wanayatumia kama itaonekana wako ndani ya hifadhi, basi wanaweza wakayapima wakayatoa. Wame Mbiki hii zamani ilikuwa ina jumuiya ambayo inajiedhesha yenyewe, ile jumuiya imekufa, sasa hivi wanasmamia watu wa *TAWA* na watu wa *TFS*. Hawa wananchi zamani ndio walitoa hayo maeneo yao, sasa hivi kwa sababu wananchi wameongezeka wanayahitaji haya

maeneo. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri busara imwongoze aweze kutupatia haya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la tembo. Wilaya ya Mvomero sisi tumepakana na Hifadhi ya Mikumi, tembo sasa hivi kwenye Tarafa ya Mlali wapo kama mbuzi, yaani wametoka kule kwenye hifadhi nafikiri kule wameisha wote, wapo kwa wananchi, lakini tukiwaliza wanakwambia huu ni ushoroba/njia ya tembo; sasa njia ya tembo, tembo ndo anakaa hapohapo mpaka wanazaliana, kama njia si apite aende kwenye safari zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tembo wamekaa eneo moja, wanazaliana na sasa hivi wanaingia kwenye nyumba za wananchi. Wakisikia harufu ya mahindi ndani wanafumua paa wanaingiza ule mkonga wao wanakula mahindi ndani. Wananchi hawalali hata ndani kwenye nyumba zao, ni mateso makubwa wanayapata, lakini tukiambiwa ushorobo, kila sehemu tembo anapoonekana ushorobo sasa ushorobo utakuwa nchi nzima. Hapa siku moja tuliambiwa, Chuo Kikuu hapa (*UDOM*) kwamba tembo wameonekana, tukaambiwa nako ushorobo, sasa mwisho watakuja kuingia hata kwenye Bunge hapa utaambiwa nako ushorobo, barabara hii ya tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri lazima wawe na mikakati madhubuti ya kuwarudisha tembo wanapotakiwa kuishi. Kule wekeni hata mipaka itaonyesha wazi kabisa kwamba haya ni maeneo tembo wanapita wananchi msilime lakini ikiwezekana kule kwenye hifadhi wekeni fensi ya kutosha tembo asivuke. Kwa sababu sisi ni maeneo ambayo yanatuathiri sana mfano Kata za Doma, Msongozi, Mangai, Melela na Lubungo wananchi hawalimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi ambaowananadai fidia pamoja na fidia yenyewe ni ndogo, wapo 2,050 hawajalipwa fidia. Pia wapo wananchi ambaowameshakufa na tembo wamefika mpaka sasa hivi 26 hawajalipwa fidia na fidia yenyewe ni ndogo, hivi kweli mtu anauawa na tembo analipwa shilingi milioni moja, shamba

linavamiwa na tembo analipwa shilingi laki moja. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nimalizie kwenye suala la mkaa. *TFS* watusaidie kwenye suala la mikaa, hivi gunia moja shilingi 12,000 unatakiwa kulipa, wananchi wetu wa vijijini hawana nishati mbadala zaidi ya mkaa na kuni, lakini leo wakikamatwa anatakiwa kulipa 12,000 *TFS* na 2,000 halmashauri, hivi kule vijijini watatumia nini?

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kengele imegonga.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofit)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Fatma Toufiq ajiandae.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuishukuru Wizara hii kwa kunitfea kuwa Balozi wa Utalii wa Ndani, lakini pia nipongeze utendaji mzuri wa Waziri Mwalimu wangu Ndumbaro na Naibu wake kwa utendaji mzuri sana katika Wizara hii. Vile vile niwapongeze zaidi kwa hili ambalo wameliona juzi tarehe 2 kwa kuruhusu *export* ya mti wa mkurungu ambao ulikuwa *barned* pasipo sababu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya maamuzi haya mazuri, lakini baada ya maamuzi haya kuna changamoto ambazo mimi naziona na naomba niishauri Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, lakini bahati nzuri zaidi kwa *TFS* ambao wapo hapa chini ya Wizara hii, kuna jambo ambalo sidhani kama wanalionna; tunapoamua sasa

kufanya *export* ya mbao ngumu tunahitaji ma-saw *doctors*. Vyuo vyetu vya *FITI* bado havijatengeneza ma-saw *doctors* ambaao wanafaa kufanya kazi maeneo yetu. Viwanda vilivyopo maeneo ya Mufindi na maeneo mengine ya mbao laini bado wanatumia ma-saw *doctor* ambaao hawana elimu ya kutosha, ndio maana uchakataji wa magogo umekuwa na tatizo kubwa kwa maana mbao hazinyooki sababu ya kufanya hata *export* hizi zinakuwa na shida katika masoko ya dunia ni kwa sababu mbao zetu hazinyooki kwa sababu hatuna ma-saw *doctors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali ni moja, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ikubali wanapowadau wa misitu hasa wawekezaji wanapowekeza katika mazao ya misitu kwenye viwanda vya misitu, Serikali ikubali kuajiri ma-saw *doctor* wa kigeni ili kusaidia ku-*train* watu wetu baada ya muda nao wataweza kuchukua nafasi zile ambazo zinatafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo hapa limekuwa na changamoto kubwa sana, wananchi wengi hasa sisi wawakilishi wao wametutuma tuwazungumzie kuhusu sakata hili la mkaa. Gunia moja mtu anatakiwa kulipia sh.12,000, bado nchi hii hatujawa na mbadala wa nishati, sasa ni namna gani tunajipanga. Kwa kuwa Serikali ni moja labda ingefanya utaratibu basi gesi hii ambayo tunayo itapakae nchi nzima mabomba ya gesi yatoke kule Dar es Salaam yaje mpaka Mwanza, yaende mpaka Tanga na Mbeya kwako kule ili wananchi waweze kutumia hii gesi ya asili lakini matumizi mbadala leo ya mkaa hatuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali iangalie namna bora hasa *TFS* watafute *species* za miti ambazo ni nyepesi kama alivyosema jana ndugu yangu hapa Mheshimiwa Profesa Kishimba, miti ambayo inaweza kupandwa kwa haraka na ikaota kwa ajili ya kupata mkaa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa asilimia mia moja.

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq na Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa ajiandae.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa na mimi siku ya leo niwe mionganoni mwa wachangiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na changamoto ambazo zinajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mchangiaji wa kwanza alivyoanza kuchangia kuhusiana na tatizo la tembo, nami ni mionganoni mwa waathirika wakubwa sana katika Wilaya ya Kalambo imekuwa ni historia ambayo hatujui imetoka wapi kwa sababu tunaambiwa zaidi ya miaka 100 tembo walikuwa hawapo katika eneo letu la Kalambo, lakini kwa sasa hivi imekuwa kama ni mifugo ambayo inaongezeka kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri analijua hili na nimekuwa nikiwasiliana naye na wananchi wanatuambia kwamba enzi za mkoloni walikuwepo Maafisa Wanyamapori ambao walikuwa *stationed* pale. Sasa hivi ninachoomba wahakikishe kwamba wanakuwepo ili kutoa utaalalm, lakini pia kuwaswaga tembo hao ili wasiendelee kuharibu mazao ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo naomba kwa leo nichangie; wamechangia wachangiaji waliotangulia kuhusiana na *circuit* ku-promote upande wa Nyanda za Juu Kusini ikiwemo pamoja na Katavi lakini na *Kalambo Falls*. *Kalambo Falls* ndio maporomoko ya pili ya Afrika baada ya *Victoria Falls*; hili nalisema kwa mara nyingine nikiamini sasa hivi Serikali inaenda kuweka nguvu yake kubwa kufanya *promotion* katika maporomoko ya Kalambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Scenery* nzuri ipo upande wa Tanzania lakini wenzetu wa Zambia wamekuwa wakitangaza *as if scenery* nzuri ipo upande wa kwao. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na watalaam wake na Katibu Mkuu yupo, akiwa *TANAPA* tuliomba kwamba sisi Halmashauri ya Kalambo hatuna uwezo wa kutangaza, tuliwaomba wachukue maporomoko ya Kalambo kuyatangaza, lakini nini ambacho kimetokea, *TFS* ambao wana Hifadhi ya Msitu wa Kalambo wamechukua pamoja na maporomoko ambayo hawana uwezo wa kutangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba, *TANAPA* ndio wachukue maporomoko, ule msitu ubaki na *TFS* lakini isiwe *TFS* ndio wachukue na Maporomoko ya Kalambo kwa sababu hawana uwezo wa kutangaza. *It's high time* kwamba tutangaze Kusini Nyanda za Juu ikiwemo pamoja na Maporomoko ya Kalambo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namsihi sana Mheshimiwa Waziri, najua ana changamoto ya kibajeti, lakini kwa namna ambayo tunaweza kuchachusha, utalii ni pamoja na kuhakikisha kwamba maeneo yale ambayo hayajatangazwa, yanatangazwa na yanakuwa kivutio, sio kila wakati iende kaskazini, kaskazini imeshakuwa *saturated, it's high time* kwamba sasa hivi tutangaze kuelekea huko ambako kuna mambo mazuri sana kwa ujumla yikitangazwa Taifa letu litanufaika wakati tunaendelea na changamoto za huko kwingine ambako watu hawapendi tena kwa sababu tumekuwa tukizidiwa na wenzetu wa upande wa Kenya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri afike, kila Waziri ambaye amehudumu katika Wizara hii akifika Kalambo anakuja na picha, ndio inakuwa kwenye *budget speech* yake. Akawaulize Mheshimiwa Maige, Profesa Maghembe, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla mpaka kuna *point*wakati anateremka aka-*faint pale* tunaita Kigwangalla *Point* na yeye aende, hakika hatojutia kwenda kuona Maporomoko ya Kalambo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Naamini humualiki Mheshimiwa Waziri ili na yeye aje ku-*faint*. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki ajiandae.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema. Sambamba na hilo naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu wote kumpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii. Pia naomba niwapongeze Wizara pamoja na bajeti finyu, lakini kuna mambo ambayo tunayaona yanafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naomba niipongeze Serikali kwamba asilimia 17 ya Pato la Taifa linatokana na utalii. Sambamba na hilo, asilimia 25 ya pesa za kigeni zinatokana na utalii. Pia Sekta ya Utalii imeweza kuzalisha ajira 1,600,00, jamani hili sio dogo, lazima tuipongeze sana Wizara yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie zaidi kuhusiana na kutangaza vivutio vya utalii hasa kupitia vyombo vya habari. Ni ukweli usiopingika kwamba vyombo vya habari ni nguzo kubwa sana katika kusaidia kutangaza vivutio katika nchi yetu ili watalii wengi zaidi waweze kufika katika eneo letu. Pia vyombo vya habari ni tegemeo muhimu sana katika kukuza utalii katika nchi yetu.

Sambamba na hilo, natambua kwamba Wizara imekuwa ikijitahidi sana, lakini naomba nishauri na ushauri wangu unatokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 31 hadi 33 amebainisha kwamba Wizara imeandaa

vipindi 70 vya *television*, vipindi 51 vya redio na makala 36 kuhusu uhifadhi na vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudhi hizo, naomba niishauri Wizara kwamba, ufile wakati sasa waandae mpango mkakati kwa ajili ya Waandishi wa Habari kutangaza vivutio vya utalii Tanzania. Kama watasema labda *Media Strategy for Tourism in Tanzania* ili sasa ule mpango mkakati uweze kutumika kwa ajili ya kuandaa Waandishi wa Habari mbalimbali waweze kuandika habari za utalii kwamba wawe wame-*specialize* katika kuandika habari za utalii. Naamini kabisa kwa kuandika habari nyingi zaidi za utalii pamoja na mengi yanayofanyika, tunaona kabisa kwamba kuna *electronic media* imekuwa ikijitahidi, lakini basi hebu uwekwe mkazo kuwe kuna ile *media strategy* ili kusudi mwisho wa siku sasa katika ile *strategy* ambayo itakuwa inaelezea malengo, ione jinsi gani ya utekelezaji na pia iwepo bajeti maalum kwa ajili ya Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kabisa kwamba wasanii wamekuwa *engaged* kwa njia moja au nyingine, sasa hebu tuone kwamba *engagement* ya *media* nayo iwe katika mtindo wake ili kusudi sasa Waandishi wa Habari waweze kuandika vizuri hizi habari za kuhusu utalii. Nafahamu kwamba kwa mfano Mashirika kama TANAPA, Ngorongoro, TFS na TAWA yamekuwa yakishirikiana na Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina uhakika kama Wizara ina mpango maalum mkakati wa kuwashirikisha Waandishi wa Habari kwa muda wote, yaani isiwe tu kwamba kwa matukio fulani au labda ndani ya mwaka *no*, yaani kiwe ni kitu ambacho ni endelevu. Naamini kabisa Waandishi wa Habari wakashirikishwa kwa kipindi hiki wanawea wakaleta mafanikio makubwa sana katika kuleta tija katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Waandishi hawa wa Habari, kukiwa kuna ile *media strategy* lakini pia waende wakajifunze katika zile nchi ambazo zimefanikiwa zaidi katika kuvutia watalii. Kwa mfano katika

Afrika wenzetu kama Misri, South Afrika, Zimbabwe, Zambia na wengineo, wameweza sana ku-*advertise*. Pia kuna nchi zingine za një kwa mfano kama Ufaransa, Italia, United States, Spain wao pia wameweza sana ku-*attract* watalii wengi sana. Kwa hiyo nashauri kwamba ufile wakati sasa na sisi tuwe tuna Waandishi wa Habari maalum kuhusu masuala ya utalii katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda siyo rafiki sana, basi kwa uchache, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt Steven Kiruswa atafuatiwa na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Dkt Christina Christopher Mnzava ajiandae.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hii hoja ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Naomba nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi muhimu ya kuhifadhi rasilimali yetu ya Taifa wanayoifanya, lakini *specifically* nimshukuru pacha wangu Waziri Dkt. Ndumbaro na Naibu wake Mary Masanja kwa kitu kizuri nilichojifunza kutoka kwao. Tangu waingie katika Wizara hii wameanzisha mtindo mzuri wa kusikiliza kero za wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa sababu Mheshimiwa Waziri alisikiliza kero ya wananchi na mwekezaji wa *Green Miles* akaja mpaka uwandani kushuhudia mwenyewe na matokeo yake yamewafariji wale wananchi. Sasa kilichobaki tu ni yule mwekezaji naye kwa sababu alimpa kibali cha kurudi katika lile eneo, akajipatanishe na wananchi maana ye ye ndiye aliwakosea na ndiyo chanzo cha ule mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na changamoto kubwa ya eneo ambalo Wizara ya Maliasili katika awamu iliyopita ya Uongozi wa Awamu ya Tano, wallilitwaa kabisa na kutaka kuligeuza kuwa pori la akiba katika Wilaya ya Longido. Eneo lile ni mahsusil la wafugaji wa

Wilaya ya Longido, maeneo ya kuhemea wakati wa kiangazi la kupatia maji na majani, lakini Wizara ikaja na pendekezo bila kuwashirikisha wananchi la kutaka kugeuzwa kuwa pori la akiba. Ni eneo la *Game Controlled Area* ambalo limekuwepo tangu enzi ya ukoloni na wananchi waliendelea kufuga huku uwindaji ukiendelea bila bughudha, lakini baada ya Waziri kuingia na kupokea hicho kilio amewapa wananchi matumaini kwamba hilo jambo linahitaji kurejelewa na bahati nzuri au mbaya pia taarifa na kilio cha wananchi kimeshafika mpaka Ikulu, kimefika kwa Waziri Mkuu na kwake, lakini ile namna yake ya kusikiliza wananchi ni jambo la kupongeza sana. Nawapongeza sana Wizara ya Maliasili kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nitoe ushauri sasa katika maeneo machache kulingana na hotuba waliyoitoa wenzetu ya bajeti na mambo ambayo yanastahili kufanyiwa marekebisho. Eneo la kwanza hizi kanuni za kifuta jasho na kifuta machozi zinahitaji kurejelewa, kiwango ni kidogo mno na muda wa kusubiri mpaka hata hicho kidogo kinachotolewa kitoke ni muda mrefu mpaka hata inakuwa haina maana tena. Naomba hilo suala lirejelewe na namwomba Waziri atakapokuja kutoa mrejesho hapa hebu atuambie kwamba ni utaratibu gani amejiwekea wa kuongeza kile kipato na kuharakisha ulipwaji wa wale watu ambaao wameathiriwa na wanyamaporii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza tozo zinazotozwa Kampuni za utalii wa uwindaji. Hiyo tasnia imeshuka kabisa na ukiwasikiliza wawindaji wanasesma ni kwa sababu ya tozo, VATilipokuwa *introduced* mwaka 2016, idadi ya watalii imeshuka kutoka 1,500 kwa mwaka mpaka wakafikia kwenye 500 tu kwa mwaka. Mbaya zaidi ulipoingizwa ule mtindo wa kuuza vitalu kwa njia ya mnada vitalu vingi vimekaa bila wawekezaji na mapato ya Serikali na ya wao wenyewe na ya jamii ambayo walikuwa wanaisaidia kupitia ule mfumo wa uwajibikaji kwa jamii pia yameshuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika taarifa ya wanaitwa *TAHOA*, Chama cha Wawindaji; wanasesma

kwamba katika minada mitatu ambayo imeshatangazwa tangu huo mfumo uanze na vitalu 60 vilivyowekwa mnadani ni 11 tu vimepata wawekezaji vile vingine vikabaki *idle* kwa sababu hakuna watu walikuwa na *interest* navyo. Sasa naomba kuishauri Serikali kwamba wapange tu bei ambayo ni *reasonable* ili kila mtu anayetaka kitalu kwa sababu kina bei tayari iwekwe *price tag* kuondoa utata wowote wa rushwa na nini aweze kuingia na mapato yakapatikana badala ya kuvifanya vikose wawekezaji na vikose ulinzi na mazingira yetu yakazidi kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tatu kwenye mfumo wa marejesho ya mapato kwenye *WMA's*, wakati *corona* ilipoingilia Mataifa na pia nchi yetu ikaathirika, mapato yote yanayokusanywa kwenye vyanzo vyya hifadhi yakawa yanapelekwa Hazina. Utaratibu wa kurudisha zile fedha zije zisaidie uendeshaji wa *WMA*, kuwapa vijiji mgao wao, ulivurugika kabisa na *WMA* nydingi karibu zishindwe *operate* kwa sababu mfumo ulikuwa haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Waziri atueleze leo kwa sababu najua kilio cha wenye Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Jamii kwamba walikuwa wamekwama kabisa katika uendeshaji. Sasa Wizara imeweka mkakati gani wa kuwasaidia, mapato yaweze kurejeshwa na Hazina waweze kujidesha na wananchi waendelee kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa nne, ni kuimarishe mahusiano baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa. Kwa huu mtindo sasa hivi ulioko wa kwamba *TANAPA* wakiona eneo ambalo limeiva wanataka tu walinyakue, hautusaidii, inatakiwa washirikishe na watambue uhifadhi jumuishi, uhifadhi wa mseto maana ndiyo itakayotusaidia katika karne hii ya ongezeko la watu na haja ya maeneo mbalimbali kwa matumizi mbalimbali ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri hili suala la hizi *WMA*'s nimesikitika kweli kwamba kuna ambazo zimekufa, sijui Wami Mbiki imekufa, japokuwa sijui wamekufa kwa nini lakini inasikitisha, kwa sababu ulikuwa ni mpango mzuri wa Serikali kuona kwamba wale wananchi walio karibu na maeneo ya hifadhi, basi hawazikuti hizo hifadhi kwa sababu wanakutana na ya kwao ambayo wameyalinda wao wenyewe. Sasa mwangalie namna ya kuzinusuru, maana sasa hayo ni maeneo yao, kama kwa namna yoyote ile walisajiliwa hivyo na yale maeneo ni ya kwao, vile vijiji pale. Sasa ikifikia mahali tena ninyi mnataka na hayo yawe ya kwenu utakuwa mtihani.

Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt Christina Christopher Mnzava na Mheshimiwa Joseph Anania Thadayo ajiandae.

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi kuwa mchangiaji katika bajeti hii ya leo. Natumia nafasi hii kuwapongeza sana watendaji wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika kulihakikishia Taifa hili linapata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ningependa ujikite zaidi katika suala zima la uendeshaji sekta ya utalii. Duniani kote wataalam wa utalii wanapozungumza suala zima la utalii wanaainisha vitu vitano wanaita A5; kuna vitu vitano ambavyo ndivyo uti wa mgongo wa utalii. Kitu cha kwanza ni amani na utulivu tuliokuwa nao; Kitu cha pili ni vivutio duniani kote ambavyo vinapelekea watalii kwenda kutembelea; Kitu cha tatu miundombinu inayoweza kufikika katika sekta hiyo na kitu cha nne ni *good service*. Katika suala la *good service* Tanzania bado hatujakuwa *more advance*; na Kitu cha tano ni suala la *promotion and marketing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mimi zaidi nitajikita katika suala zima la *promotion and marketing*. Tanzania takriban tupo nchi ya pili kwa kujaaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii duniani. Nchi ya kwanza Brazil, lakini

cha kushangaza na cha kusikitisha sisi bado hatujajiwekeza zaidi katika kutangaza biashara hii. Ukiangalia duniani kote utalii siku zote unaletwa na matamasha, maonyesho pamoja na *festivals*, lakini sisi Tanzania mpaka hii leo tuna matamasha yasiyozidi manne wakati wenzetu Brazil wana matamasha yasiyoshuka 58. Ukija nchi kama Spain wana matamasha 48 na Uingereza wana matamasha 54.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusitarajie sana kutangaza utalii wetu kwa kutegemea zaidi labda Tanzania *Safari Channel* ya *TBC*, inawezekana hata hiyo *TBC* hata Dubai watu hawawezi wakaisikia. Unapoangalia *channel*/kama vile *CNN* pamoja na *Sky News* utaona utaona nchi za wenzetu kama vile Belarus, Bulgeria wameweka *clip* zao ndogo ndogo kuonyesha jinsi gani nchi zao zilivyokuwa na vivutio vingi nya utalii. Tuangalie mfano nchi ya Jirani hapa hii wanayoita Rwanda ni nchi ndogo sana, tumewazidi kwa vivutio vingi sana nya kitalii, lakini wao wanatumia bajeti kubwa katika kuwekeza katika sekta hii. Wameweza kuisaini *Memorandum of Understanding* na timu kama ya Arsenal, unapoangalia jezi za Arsenal mkononi hapa wameandika *visiting* Rwanda. Kwa hiyo wanatumia bajeti yao katika kuitangaza hii sekta nzima ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana ndugu zetu Simba, kama wenzetu wengi walivyokwisha kuelezea, wakati ambapo walipoenda kushiriki hizi ligi za klubu bingwa barani Afrika walijaribu sana kuitangaza Tanzania. Hata hivyo, lazima tukubali utalii wetu wa Afrika hususan Tanzania unategemea zaidi watalii kutoka Magharibi mwa Ulaya pamoja na nchi za Amerika na *Nordic countries*, sasa huko Simba bado hawajaweza kufika. Kwa hiyo, lazima tutafute njia nyngine za kuweza kuwekeza kama vile tunaweza kutangaza utalii wetu katika ligi kubwa kama vile ligi za Bundesliga Uingereza kule pamoja na nchi nyngine kama vile Ufaransa tukiwa tuna *clip* zetu za kuweza kututangaza tunaweza kufanikiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Tanzania tumebahatika kuwa na vyanzo vingi nya maji, lakini

Watanzania bado hatujaelimishwa namna gani tunaweza kuvitumia vyanzo vya maji kama ni sehemu moja ya utalii. Katika vyanzo vya maji tuna uwezo wa kupata utalii wa *water sport*, hauhitaji gharama nyingi wala hauhitaji bajeti kubwa ukilinganisha na utalii wa aina nyingine. Tanzania tuna visiwa ambavyo havitoshuka 220, havishuki hapo, lakini duniani kote utalii ambao una thamani zaidi ni utalii wa kivisiwa, lakini ukitizama huku kwetu sisi visiwa hatujaweza kuviorodhesha kama ni sehemu ya kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wanatumia visiwa kama sehemu ya kitega uchumi, lakini sisi badala ya kujaliwa neema hiyo tutumie kama ni sehemu ya kitega uchumi tunaenda katika migogoro. Nimpe mfano Mheshimiwa Waziri; kuna kisiwa kimoja kinaitwa *Latham Island* ambacho kwa jina maarufu tunaita tunaita Fungu Mbaraka, watembezaji wa watalii wanapotoka kule Zanzibar kwenda kuangalia kile kisiwa pale wakiwa na wageni mara nyingi wanazuiliwa sana, kumekuwa na malalamiko ya aina yake kwa watu wa *TMA* (*Tanzania Marine Authority*) kwa kushirikiana na *fisheries*, wanakuwa wanawazuia kwa sababu wana leseni za kibiashara kutoka Zanzibar. Wanafanya kitendo kile hali ya kwamba wale watembeza wageni wanao wageni na wageni wanafahamu kile kinachozungumzwa, hii inatuharibia, sisi sote tunajenga nchi moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kwa kuongezea kuna suala zima la miundombinu. Utalii ni sekta ambayo haiwezi ikajitegemea yenyele lazima inategemea sekta nyingine. Mtalii anapotoka kwao haji hapa na embe, haji hapa na wali katika *hotpot*, wala haji hapa na gari ya kutembelea, anataraja aje hivyo vitu avikute hapa. Cha kusikitisha sehemu nyingi ambazo zimepitwa na sekta hizi za utalii wanafanya biashara...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Naona Mheshimiwa Waziri ananiangalia nikawa najiuliza katika haya matamasha manne, sijui kama tamasha langu kule Mbeya limo au halimo, kwenye haya manne.

Mheshimiwa Dkt Christina Christopher Mnzava atafatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Thadayo na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai ajiandae.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili ya Utalii. Kwanza nipende kuwapongeza sana Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri na Naibu Waziri wamekuwa ni watu wasikivu sana, unapowafuata kwa kitu chochote kinachohusu Wizara yao kwa kweli wanachukua muda kusikiliza. Katika hotuba ya bajeti ya Maliasili na Utalii wametoa vipaumbele; moja ya kipaumbele ni kuratibu mapitio ya sheria, sera, kanuni na kuandaa miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna migogoro mingi baina ya hifadhi na wafugaji na kupelekea sehemu zingine wafugaji wanauawa au wananchi wanauawa. Tumesikia katika Wilaya za Kiteto, Longido, Ngorongoro na hata Chemba matukio kama haya yanatokea. Ningombaa Wizara kupitia Wizara ambayo inasimamia wafugaji na inasimamia hifadhi ambayo ni Wizara ya Ardhi. Kwa mtizamo wangu naona kwamba Wizara ya Ardhi ina jukumu kubwa sana la kuhakikisha kwamba maliasili inafuata sheria pamoja na wafugaji na wananchi wengine wanafuata sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ipo toka kuumbwa kwa dunia, haiongezeki na haitaongezeka lakini sisi

wanadamu tunazaliana kila siku iitwayo leo. Kwa maana hiyo mahitaji ya ardhi yanaendelea kukua kwa kasi kubwa sana kutokana na *population* yetu Watanzania, lakini unakuta kwamba hifadhi alama ambazo zilizowekwa au mipaka ambayo iliwekwa enzi zile za mwaka 1940 na ngapi kule bado zinatumika mpaka leo wakati kuna ongezeko kubwa sana la wanadamu. Kwa maana hiyo basi, Wizara ipitie katika vipaumbele vyake ipitie kuangalia sheria, kurekebisha mipaka, kuwapa nafasi wananchi wawewe kutumia hiyo ardhi, kwa sababu idadi ya wananchi inaongezeka kila leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna migongano ya matumizi ya ardhi kwa jamii ya wafugaji kati ya wahifadhi, wawekezaji lakini pamoja na wananchi kwa ujumla. Tunaomba Wizara hii ijaribu kushughulikia kuangalia kwamba inatatua vipi matatizo ambayo yanawapata wafugaji. *Solution* siyo kuwaa tumesikia kuna hili Shirika la TAWA Pamoja na TFS wanafanya kazi zao vizuri, lakini je ni lazima kutumia nguvu, ni lazima kutumia risasi, ni lazima kutumia bunduki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua sheria zipo, basi tunaomba wafuate sheria. Kama kuna wafugaji, kama kuna wananchi, kama kuna taasisi ambayo imeingia kwenye hifadhi tunaomba sheria zisichukue mkondo wake. Kuna chombo ambacho kinatoa maamuzi kuna mahakama, wasichukue sheria mkononi ya kuwaa. Kuna ambao wanapatikana, kuna ambao wanajulikana wameuawa, kuna ambao hawajulikani, unashangaa watu wamepotea.

Naomba sana Wizara ya Maliasili na Utalii ikishirikiana na Wizara ya Ardhi, ikishirikiana na TAMISEMI, ikishirikiana na Wizara ya Mifugo wahakikishe kwamba wanafuata sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Anania Thadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai na Mheshimiwa Vuma Augustino Holle ajiandae.

MHE. JOSEPH A. THADAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii la kwanza niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya Wizara kwa dhamana kubwa hii ambayo wamekabidhiwa ya Wizara hii nyeti kwa ajili ya mapato ya nchi yetu ajira na kuitangaza nchi yetu nje. Wanafanya kazi nzuri na kwa kweli tuna kila sababu ya kuwapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ya Awamu ya Tano na ya Sita imetumia nguvu nyingi sana katika kutangaza utalii jambo ambalo hapo kale pengine halikuwahi kufanyika sawasawa na kwa sasa naamini kabisa kwamba duniani hakuna asiyejua kwamba Kilimanjaro iko Tanzania, *Olduvai Gorge* iko Tanzania na Fukwe za Zanzibar zenye *Dolphins* wengi ziko Tanzania, pamoja na Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili pia tuipongeze Bodii ya Utalii chini ya Mheshimiwa Jaji Mstaafu Thomas Mihayo, walioneckana kabisa kuwa kutumia nguvu ya ziada kwenye hili, tunawapongeza sana. Juhudi hizi zisipunguzwe kwa sababu washindani wetu bado wako kazini. Hii ni sawasawa tu na vita ya kiuchumi, kwa hiyo tuendelee kujitangaza kwa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiache kuzungumzia suala la tembo kwa sababu Jimbo langu la Mwanga liko katika mazingira magumu zaidi kwa sababu liko katikakati ya mbuga mbili, upande mmoja kuna Mbuga ya Tsavo ya Kenya na upande wa pili kuna Mbuga ya Mkomazi. Naishukuru sana Wizara, Naibu Waziri alitutembelea. Alifanya kazi nzuri sana na kwa kweli niwashukuru wananchi wangu wa Mwanga pamoja na viongozi wote wa Chama na Serikali, walijitokeza kwa wingi na kimsingi wananchi wa Mwanga wamekubaliana na wito wa kuwa wadau wakubwa sana wa hifadhi na kazi inaendelea vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo matatu ambayo wananchi wa Mwanga wanayatarajia. La kwanza, ni kuongezewa idadi ya Askari wa Wanyamapori ili angalau waweze kuvuna vile walivyopanda na pia watoto waweze kwendaa shule, ahadi hiyo ilitolewa na tunaamini itatekelezwa. La pili, ni kufungua lile lango la la Kaskazini kwenye Mbuga ya Mkomazi kwenye maeneo ya Kata ya Toloha, ambayo kwa kweli wananchi wa Mwanga wanaisubiri kwa hamu na wameshajiandaa kwa ajili ya fursa za biashara zitakazotokana na lango lile la pale. La tatu, ni kwamba bado wananchi wa Mwanga wanaona kwamba watafiti wetu, Vyuo Vikuu vyetu pamoja na wataalam bado wanacho cha kutuambia juu ya tatizo hili la tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo ambayo Serikali imefanikiwa tu, kwa mfano; tatizo lile la majani yaliyokuwa yanaota kwenye mbuga ambayo siyo mazuri, yalimalizwa kitaalam na kitafiti na hali inaendelea vizuri sana. Sasa kwa vile tumeshajua kwamba kinachowatoa kule tembo ni nini kuwaleta huku, basi tuwajengee mazingira ili waendele waweze kuendelea kukaa kule. Kama yako aina ya malisho ambayo inawafanya watoke kule, naamini yanaweza yakapandikizwa huko huko kwenye mbuga ili waendelee kukaa kule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia liko suala la matumizi ya *electronic fence* ambacho taarifa nilizonazo ni kwamba pale *Tsavo National Park* wenzenetu wameweka *electronic fence* upande unaoelekea kwenye maeneo ambayo hawataki tembo waende, ndiyo maana wanakuja kwa wingi huku. Hata ukienda Amboseli National Park kuna maeneo mawili wametumia *electronic fence* moja linaitwa Namelok, ambalo limefanikiwa sana na *fence* nyingine inaitwa Kinama bado inachangamoto, lakini inaendelea kufanyiwa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoamini ni kwamba watafiti wetu; Vyuo vikuu vyetu na wataalam wetu, wakiingia kazini sawasawa, bado tunao uwezo mkubwa sana wa kuweza kupata suluhisho la kudumu kuliko kutegemea hizi

measures ambazo ni kama za dharura za kushughulikia jambo kama hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma utafiti wa *Cambridge University* kwenye *journal* yao moja *online*, wanasema hata suala la kutumia nyuki bado lina changamoto, tena walifanya utafiti mwaka 2018 kwenye Hifadhi ya Udzungwa, bado lina changamoto. Kwa hiyo nadhani, watafiti wetu wanapaswa kuingia kazini zaidi ili kusaidia juhudhi hizi za Serikali nazo zifanywe katika kuzuia hili tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina zaidi ya hapo, naunga mkono hoja, Wizara inafanya kazi nzuri, Serikali iwave fedha walizoomba ili waweze kutekeleza majukumu yao. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, atafuatiwa na Mheshimiwa Vuma Augustine Holle na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, ajiandae.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara hii na Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuongelea maendeleo ya Wizara hii bila kutaja Kanda ya Kaskazini hususani Mkoa wa Arusha. Wameongea vizuri sana Wabunge wa Majimbo wa Mkao wa Arusha, jana ameongea kaka yangu Mrisho Mashaka Gambo, ameongea vizuri kuhusiana na Wizara hii, umuhimu wa Wizara hii katika mkoa wetu.

Vilevile baba yangu Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido ameongea vizuri sana kuhusiana na umuhimu wa Wizara hii na mimi kama mwakilishi wa Mkao wa Arusha, naomba nisisitize umuhimu wa Wizara hii katika Mkao wetu wa Arusha (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba pia niwashauri Wizara hii ya Maliasili na Utalii

waendelee kuwashirikisha wadau wakuu wa maendeleo wa Mkoa wa Arusha katika maendeleo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba niongelee suala moja tu la sintofahamu iliyoko katika Wilaya ya Longido kuhusiana na maamuzi ya Serikali kutenga maeneo yao kuwa Mapori ya Akiba. Naomba niikumbushe Wizara kwamba asilimia 95 ya wakazi wa Longido wanajihuisha na ufugaji na wanategemea sana mapori haya kwa ajili ya malisho ya mifugo yao. Maamuzi haya ya Wizara yataathiri Zaidi ya vijiji 19, vya Tarafa ya Ketumbeine na vijiji 11 vya Tarafa ya Engarenaibor na kijiji kimoja cha Tarafa ya Longido. Tukumbuke kwamba pia katika maeneo haya kuna wakazi zaidi ya 90,000 ambao wanategemea pori hili katika masuala yao mbalimbali ya kuishi na katika kuinua kipato cha uchumi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa pia kwa juhudzi zao binafsi wameendeleza miundombinu ya masuala ya kijamii kama afya, elimu na kadhalika. Kwa hiyo sidhani kwamba ni suala la busara kuwaondoa katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu wa Awamu ya Tano yake alifanya jitihada kubwa sana kurudisha zaidi ya vijiji 900 kwa wananchi ili waweze kupata maeneo ya kuishi na kufanya shughuli zao mbalimbali za kiuchumi. Vile vile katika hotuba ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, alioisoma tarehe 22 Aprili, hapa Bungeni alionyesha dhamira kubwa ya Serikali katika kuongeza maeneo ya wafugaji hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi za Wizara hii ya Maliasili na Utalii, naona dhahiri zinakinzana na dhamira njema ya Serikali kwa wananchi wetu. Naiomba sana Serikali yangu sikivu kupitia Wizara hii, itumie busara katika jambo hili ili basi lisiweze kuleta madhara kwa wananchi wetu. Naomba pia wizara hii kabla ya kufanya maamuzi kama haya iweze kuwashirikisha wadau mbalimbali hususani wa maeneo yale ili waweze kutoa maoni yao juu ya mambo haya. Vile vile naomba sana Wizara kabla ya kufanya maamuzi haya iweze

kutembelea maeneo haya ili ijue basi, kama kweli maeneo haya ni mapori ama ni makazi ya wanadamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami kwamba, nadhani Mbunge kweli alijiandaa kuja kuchangia Wizara hii, alivyovaa tu inaashiria mambo mazuri ya utalii wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kushukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia na kushauri machache kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza nipende kumshukuru na kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kwa ushirikiano ambao anaendelea kutupa sisi wananchi wa Kasulu, hususani Kasulu vijjini baada ya mvurugano mkubwa na *TFS*. Busara za Mheshimiwa Waziri zimetusaidia sana, tunamshukuru sana, sana, asiyeshukuru ni kafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu miaka mitatu iliyopita kama sikosei miwili, kulitokea mlipuko huu wa ugonjwa wa *corona* yaani *Covid 19*. Ugonjwa ambao umefunga dunia kabisa na uliathiri sana, sana, mwenendo wa utalii duniani hata kwetu sekta ya utalii ilisinyaa sana. Sasa wakati huu ambapo tunajifunza kuishi na ugonjwa huu, nipende kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa juhudhi na hatua anazochukuwa kuhakikisha kwamba anafungua Taifa letu ili kuhakikisha kwamba Taifa letu wageni wanakuwa na *confidence* ya kuja hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu tunajua sekta ya utalii *key players* ni *foreigner* hao ndio wakubwa. Sasa kama hawana *confidence* na nchi yetu, sasa kama hana *confidence* na njia ambazo tunazitumia

kuhakikisha kwamba tunafungua nchi yetu au kufanya nchi kuwa salama, hapa utalii wetu utaendelea kusinyaa, ni lazima tukubali. Dunia imekubali kwamba namna ya kuweza kufungua dunia tena na shughuli mbalimbali za utalii ziendele ni namna ya kuwapatia watu chanjo, watu wapate chanjo ili wawe na *confidence* ya kusafiri kwenda sehemu mbalimbali, mtalii ajija hapa akipokelewa na mtu ambaye amepewa chanjo, naamini atakuwa na *confidence* kubwa zaidi kuliko kupokelewa na mtu ambaye hajapewa chanjo. Sasa katika hili kule mtaani tunasema, mama anaupiga mwangi sana katika upande huu wa kushughulikia suala la *Covid-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina machache ya kumshauri Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro hasa kwenye utalii wa uwindaji. Kule kwangu Kasulu tuna kitalu cha uwindaji, sasa wakati wa *Covid 19*, utalii wa uwindaji umesinya sana, lakini wako wawekezaji wachache pamoja na kwamba utalii wa uwindaji ulisinya sana lakini wameendelea kuwa na sisi, vitalu vingi viko wazi kwa sababu ya *Covid-19*, lakini wako wachache ambao waliendelea kuwa na sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande huu, ningependa kushauri yafuatayo ili kuhakikisha kwamba utalii wa uwindaji unaendelea kuwa na nguvu na unaendelea kutuletea mchango kwenye sekta ya utalii. Moja, ningependa tuwatie moyo wale ambao wamesimama na sisi wakati wa *Covid 19*. Kwa sababu ni ukweli usiopingika wengi wao wametengeneza hasara, wamelipa kodi, wamelipa kila kitu lakini watalii hawakuwa wengi kama ambavyo walivyotegemea, sasa lazima tuwape moja tuwatie joto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kwenye mnada unaokuja hawa watu tuwape holiday wasishiriki mnada, waendelee kuwa na maeneo yale yale ambayo wamekuwa nayo, ili kuhakikisha kwamba wanaweza kurudisha zile gharama ambazo wameingia hasara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sana kwa wakati huu ambapo tunapambana na ugonjwa hili, tujitahidi sana kuwaruhusu watu walipe kwa *instalment*. Kama mtu umemwambia kitalu unachomuuzia ni dola 80,000, basi ufanye alipe kwa *instalment* ili kwamba aweze kupata nafasi pamoja na mazingira magumu ya kiuchumi ya kuweza kulipia Serikali ipate mapato.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kengele imeshagonga.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja tu, lipo la msingi.

NAIBU SPIKA: Kila mtu akiomba moja sitawenza, sekunde 30.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, moja muda wa watu wa kufanya mnada urefushwe. Haya mambo ya kumpa mtu mwaka mmoja halafu utegemee aendeleze kitalu kwa kuendelea kufanya uwekezaji haiwezekani, lazima tuongeze muda wa kufanya mnada. Ukipa mtu umpe miaka mitano, miaka angalau kumi aweze kufanya uwekezaji, aendeleze kitalu vizuri. Kwa kufanya hivyo..

NAIBU SPIKA: Muda wako sasa umekwisha.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, ajiandae.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana kwa Jimbo letu na kwa Mkoa wetu

wa Kilimanjaro. Nawashukuru na nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu wake kwa kuwa wenye mwamko chanya katika kushughulika na matatizo yetu kwenye mikoa yetu hasa sisi ambao tunapakana na hifadhi na tunasimamiwa na *TFS* ambayo imekuwa inanyanyasa sana watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuzungumza jambo moja hili la nusu *mile* na natumaini limezungumziwa vizuri sana, nusu *mile* ni kitu ambacho kwetu kinatuuma kwa sababu kama mnajua kwamba ardhi yetu kule Kilimanjaro ni ndogo, lakini pia ukiwa unapakana na msitu huu unaozunguka Mlima Kilimanjaro unakuta kwamba fursa iliyopo ni kuokota kuni, kukata majani, kuweka mizinga ya nyuki na kadhalika. Mwanzoni tuliruhusiwa kuingia hadi nusu *mile* hiyo, lakini baadae *TFSwakang'ang'ania* kuchukua hata eneo hilo, walkuwa wanaturuhusu hata angalau wanawake waingie kukata kuni na kuchukua majini, lakini sasa hawaruhusiwi. Naomba hilo jambo lifikiriwe na nimeshazungumza pamoja na Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu, naamini kwamba litakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nazungumzia kuhusu *stimulus package* kwa sekta hii muhimu ya utalii. Naamini kwamba wengi wanaelewa jinsi ambavyo watu wameathirika; mahotelii yameathirika, hayajatengeneza fedha, yametengeneza hasara kwa muda mrefu na hawa *tour operators* pia wametengeneza hasara. Hivyo nafikiria itafaa kujua ni namna gani ya kuweza kuwanusuru kwa kuwapa muda kama wana mikopo, kama wana tozo wanadaiwa kwenye vitalu au kwenye maeneo yao wanayoshughulika nayo, Serikali iweze kuona ni namna gani ya kuwanusuru kwa kuwapa muda mrefu wa kulipa au kuwasamehe kwa maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme pia kwamba kuna tatizo baada ya hilo na kama ikiwezekana naamini linawezekana kama tukilifikiria vyema, tukijua hii ni sekta muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni *issue* ya *tour operators*; niliwahi kuzungumza kuhusu *tour operators* hapa. *Tour operators* wameunda jumuiya yao kule kwetu Kilimanjaro kupandisha watalii mlimani. Wameunda hii jumuiya ili kui-serve na kui-regulate; waweze kujivekea *discipline* na namna gani wanapandisha watu na nidhamu katika kushughulikia watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa walikuwa wanafikiri kwamba ni vizuri ili waweze kujadiliana vizuri malipo yao na *tour operators* waweze kupata au waweze kupewa fursa ya kujadiliana na wawekezaji wa *tour operators* na pia kujichagua wenyewe nani anapandisha huyu kwa vile anajua Kiswahili, Kifaransa na kadhalika. Kwa hiyo tunaomba kwamba *tour operators* wapewe mwongozo huo wa kutumia jumuiya hiyo ili waweze kupandisha watu/watalii mlimani wakiwa wamekaa vizuri na mtalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, watalii hawarudi kwa sababu hawaii-*treated properly*, lakini wakitumia jumuiya hiyo ambayo ni wataalam watawaweza wakawa-*treat* na wale ambao wanafanya mambo ambayo siyo ya kinidhamu, wakashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni suala zima la utalii wa vivutio vya kiasilia. Watu wanasema kwamba kivutio cha kiasilia hapa Tanzania ni Mmasai tu, kumbe kuna vivutio vingi, kuna mahandaki, kule kwetu Mamba, Komakundi kuna mahandaki ambayo ukiingia utashangaa, utafikiri upo mahali tofauti kabisa, kule Tanga - Amboni; sio Amboni, watu wamechimba kujificha wakati wa vita, kuna mengi ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi pia kuna vivutio kwa mfano, namna watu walivyokuwa wanafua vyuma asilia, uhunzi kule kwetu watu wanafua, wanatumia namna ambayo ni teknolojia ambayo ni ya kizamani lakini watalii wakiona wanashangaa ni kitu gani kinafanyika. Kwa hiyo, nashauri, tusing'ang'anie tu hifadhi ya misitu, hifadhi za wanyama na kadhalika, tuanze sasa kuunda kitengo maalum ambacho kitashughulika na vivutio asilia, vitangazwe na

vierodheshwe, ni wapi utaona nini na wapi utafanya nini.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, ajiandae.

MHES. RASHID SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara, Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wanafanya kazi nzuri sana ambayo imeanzia kwenye kule ku-*planjezi* ya wekundu wa Msimbazi kwa kuweka lile jina la Visit to Tanzania, naamini kabisa kwamba tutaona athari chanya za neno lile muda si mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kushauri mambo kadhaa katika Wizara hii. Jambo la kwanza nataka niwaarifu Wizara kwamba, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi inapakana na wilaya nne; Wilaya ya Mwanga, Same kwa Mkoa wa Kilimanjaro, lakini kwa Mkoa wa Tanga, kuna Wilaya ya Lushoto pamoja na Wilaya ya Mkinga. Sasa mara zote Mawaziri wanapofanya ziara wanakwenda Mkoa wa Kilimanjaro pekee. Sasa nataka niwaambie na Tanga ipo kwa maana ya Lushoto na Mkinga, inapatikana Hifadhi ya Taifa Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule tuna changamoto ya tembo wamevamia katika miji kadhaa hasa katika Tarafa ya Umba, Kata ya Mnazi na Kata ya Lunguza, Vijiji vya Mkundi Mbaru na Mkundi Mtate kule tembo wanasumbua sana. Juzi wamemwona Naibu Waziri yuko Kilimanjaro wakasema huyu Mheshimiwa Naibu Waziri mpaka asikie tumevuna tembo ndio afike hapa. Kwa hiyo namwomba sana afike eneo lile akatatuwe matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nataka nichangie kuhusu soko la utalii. Wizara hii kuna maeneo

ambayo inakosea, tunasubiri watalii waje wenyewe Tanzania kwa kutumia *tour operators* wa Kitanzania. Nataka niwaambie kwenda kwa stahili hiyo ya kuvua samaki walioko kwenye kapu haitatusaidia, ni lazima tujitahidi twende kule ambako wanapotoka. Kuna *festival* kubwa mbili zaidi duniani; ya kwanza iko kule *South Africa* ambayo wanaita Indaba, iko kama ile Karibu *Festival* ya Arusha, lakini hii ya *South Africa* inakusanya Mataifa ya Afrika, Ulaya pamoja na Mataifa ya Amerika ya Kusini. Hali kadhalika kule Ujeruman *Berlin*, nako kuna shoo kubwa sana ya mambo ya utalii. Kule ndiko Wizara inapaswa kwenda kukutana na *tour operators* wa kimataifa wale ndio wanaosukuma watalii kuja katika nchi zetu, lakini tutakapokuwa tunasubiri huku itakuwa sio kazi rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tumwombe sana Mheshimiwa Waziri sana, yeeye ni Mngoni na ame-*migrate* kutoka *South Africa*, sasa asikae Wizarani, atoke aende huko duniani akatuletee watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nataka kuchangia kwenye eneo la vitalu vya uwindaji. Uwindaji ni sekta ambayo imefifia. Mwaka 2013 tulipata wawindaji takribani elfu 1,550, lakini mwaka 2018 kabla hata ya *covid* walishuka mpaka 473. Kuna mambo fulani tuliyafanya pale ambayo tulikosea, ikiwa ni pamoja na kuongeza ile tozo ya leseni ya vitalu kutoka dola 30,000 kwenda dola 85,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana sisi nchi yetu jiografia imetawanyika sana, mwindaji anapotoka Ulaya, anakuja aidha *Kilimanjaro International Airport*, Dar es Salaam ama Zanzibar, anahitaji tena kuchukua *charter flight* kwenda Selous, kwenda Katavi, kwenda Burigi wakati huo kabla haijawa hifadhi kwa ajili ya kufanya huu uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna gharama nyingine ambazo wanazipata. Hivyo, sasa tutengeneze *inclusion* ya kupunguza gharama hizi ili tuweze ku-*facilitate* hizi shughuli za uwindani katika maeneo ambayo yako *scattered*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sekta nzima ya Utalii nataka niwaambie, tuna *advantage* kwa mwaka huu kwa sababu hata Zanzibar watalii walipatikana mwaka uliopita na mwaka huu ni wengi zaidi kuliko historia ya utalii Zanzibar. Hii ni kwa sababu *covid* kote duniani wanajua Tanzania ndio sehemu ambayo ni *covid free*, kwa hiyo wenzetu Wazanzibari kwenye eneo la utalii watakuwa mashahidi, miaka hii miwili wamepokea watalii wengi sana.

Kwa hiyo na sisi tuboreshe tu mazingira tuangalie tozo zetu zimekaaje tuweze kupata hiyo *advantage* ya kuwa *covid free* kwa ajili ya kuvutia watalii wengi sana kuja kutilii katika nchi yetu. *Otherwise* nawapongeza wanafanya kazi nzuri, waendelee hivyo hivyo. Namshukuru pia hata akienda pale uwanja wa Taifa ye ye kama ye ye magoli huwa yanakuwa mengi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro na Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nami kuchangia Wizara hii muhimu katika uchumi wa Taifa letu. Kama nchi tumejiwekea malengo kwamba tufikie watalii milioni tano lakini ukiangalia *trend* kuanzia hata mwaka 2016 kwa takwimu za Wizara yenye we walikuwa na watalii milioni 1.28; mwaka 2017 wakawa milioni 1.3; wakaja milioni 1.5; na sasa hivi 2020 waka-*drop* mpaka 620,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sisi ni wa pili kwa vivutio vingi duniani, lakini hatujaweza kuvitumia vizuri kuhakikisha kwamba utalii unatuingizia fedha nydingi za kigeni. Sasa nitakwenda kushauri machache tu kwa sababu ya uchache wa muda, kama Taifa na hili tumekuwa tukilisema, tuhakikishe katika balozi zetu tunaweka Maafisa Utalii ambao wanaujua utalii *per se*, ambao wanajua vivutio vyote tulivyonavyo Tanzania. Wakiwa kule kwenye zile nchi,

watatumika kutangaza utalii wetu katika maeneo mbalimbali kwenye nchi husika. Hii itaenda kuongeza utalii na watu kutembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine utalii wa ndani kama sisi Watanzania tunakuwa mpaka unamaliza chuo, unaenda, wengine wanaenda mpaka nchi za nje, lakini hawajui hata vivutio tulivyonavyo Tanzania. Kwa hiyo tuki-*promote* utalii wa ndani kuhakikisha kwamba *entry fee* inakuwa nindogo, Mtanzania wa kawaida akiingia pale, basi hata yale mahoteli yawe *accommodated* kwa hawa Watanzania. Unakuta mahoteli ya mle ndani bei zao ni juu sana dola 200, 300 mpaka 1,000 huko, Mtanzania wa kawaida hawezи ku-*afford* kwenda pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatakiwa hata wanafunzi wetu wa Shule za Msingi, Sekondari wanapata fursa ya kwenda kule, wanajifunza ili wanapokuwa wakubwa baadaye wakienda nchi za huko wanatangaza. Wakija watalii wa nchi zingine hapa kama ni watalii wa kibashara wakikutana na mimi Esther Matiko nakuta nimeshajifunza, najua mbuga zetu, najua vivutio vyote, kwa hiyo nikiongea naye, akitoka akienda huko nje atatangaza na utalii utaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuweza kuboresha miundombinu ya barabara hasa kwenye maeneo ambayo yako mipakani ili hata watalii ambapo wako nchi za jirani wanavyotaka kuja huku waweze kuwa vizuri, mathalani kule Tarime, tunapokea watalii ambao unakuta wameingia nchi ya Kenya, wanatoka Nairobi wanaingia Sirari, lakini wakishafika pale Tarime kwenda Serengeti, barabara ni mbovu na tumekuwa tukiongea kwa muda mrefu, irekebishwe ile barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marais wote wa Awamu ya Tatu, ya Nne na ya Tano walihidi kutengeza barabara ile. Barabara tukitengeneza kwa kiwango cha lami watalii wakitoka kule ni wengi sana kuingia Serengeti tunaweza kukuza uchumi wetu. Serengeti imetajwa kuwa ni mbuga ya

kwanza duniani na hata kwa Taifa letu ndio inaongoza kuleta mapato kwenye nchi yetu. Kwa hiyo ile barabara lazima iwekewe lami na maeneo mengine hata zile barabara za ndani ya mbunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uchache wa muda, niendelee kuzungumzia mgogoro wa hifadhi na wananchi wetu. Tumekuwa tukizungumza hili Watanzania wetu wanauawa na hawa maaskari *game* mathalani kule Tarime, kuna Watanzania wameuawa Manga wa Kijiji cha Kenyamusabi; kuna ndugu John wa Kijiji cha Nyandage; kuna ndugu Mangenyi wa Kijiji cha Kegonga; hawa walikuwa ni wakulima tu wako mpakani. Ikasikika tu risasi wamepigwa wananchi wale hawajaonekana mpaka leo, lakini kuna wengine ni wafugaji zikasikika tena risasi ng'ombe hawajaonekana na hao wananchi hawajaonekana mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio Tarime tu, Mbunge wa Mbarali alisimama juzi kati hapa akawa na *statement* na wananchi wengi hapa kama hatuwezi tukathamini wanyama huku tukawa tumewaua ndugu zetu, ichukuliwe hatua stahiki, kama askari *game* walinde hifadhi vizuri, wakiwakamata wawapeleke kwenye sheria, Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wake na Naibu Waziri najua haw ani watu ambao hawataki kuona haya mambo yanatokea, lakini watendaji kule chini wanafanya ndivyo sivyo. Hii haikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni vile wanavyotaifisha ng'ombe. Hata wakienda mahakamani, mahakama ikaruhusu kwamba hawa watu warudishiwe ng'ombe wao, bado hawarudishiwi. Mathalani kuna Ndugu Hamisi wa Chato alinitafuta sana, ng'ombe wake walikamatwa kwenye Pori la Kigosi huko Kibondo mwaka 2018, walikuwa ng'ombe 420, lakini hawa askari wakasema walikuwa ng'ombe 216, wale wakawapekeleka mahakamani wakasema walipe tozo ya shilingi 500,000 wale ndugu wakalipa, lakini hawakurudishiwa ng'ombe wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale watu wakaendelea kufuatilia.wakakata rufaa kwenda mkoa wakashindwa, kwenda Kanda ya Tabora wakashindwa, wakawa wanaamuriwa warudishiwe ng'ombe wao, wakashindwa kurudishiwa. Wakampigia aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, walivyopiga simu kule wakaitwa wakapewa ng'ombe 73 tu. Hii ni dhuluma, kama wanaweza wakawakamata Watanzania wengine wakasema ni uhujumu uchumi, ina maana na wao wanafanya uhujumi uchumi dhidi ya Watanzania. Kama yule mtu tangu mwaka 2018 alikamatiwa ng'ombe wake 420, waka-*declare* wenyewe ni ng'ombe 216, yet wanaipa ngombe 73 wengine wanaenda wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haikubaliki, mpaka hukumu tatu zote na wakiomba nitazi-*table* hapo, tunaomba hii ni *just a single case study*, wako wengi sana wamezungumza hapa. Kuna juzi kati nilimwona hata yule wa Longido kule alikuwa analia, yule baba na familia yake, ng'ombe wanataifishwa, tuna sheria tumejitungia ng'ombe wakiingia wapige faini inajulikana, kwa nini wanawataifisha, yet hawawarudishii ng'ombe wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa matumizi bora ya ardhi; kuweza kuondokana na hii sijui mara mara ng'ombe wametaifishwa, wananchi wanauawa, sijui tembo wanaingia kwa raia, sasa hivi hifadhi tulizokuwa nazo kama tunataka tuzichukue kwa matumizi bora ya ardhi tutenge, iljulikane kabisa hili eneo ni kwa ajili ya hifadhi, hili eneo halitakiwa kuwepo, ili hata vile vijiji ambavyo viro kwenye hifadhi basi Wizara iweze ku-*declare* waondoe wale wananchi, kuliko hiki wanachowafanyia wanawaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bora ijulikane, kama wameamua kuondoa hivyo vijiji zibaki hifadhi waondolewe, wawape *alternatives* ardhi waende wakakae. Hatuwezi kuvumilia kama nchi kuona Watanzania wanauawa. Nina majina zaidi ya Watanzania 30 ndani ya Mkoa wa Mara ambaao wameuawa kwenye ile Mbunga ya Serengeti, hatuwezi kukubali kitu kama hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Bunda, Serengeti na Jimbo la Tarime Vijiji haikubaliki. Kwa hiyo tunaomba sana Waziri na watendaji wote hawa askari *game* ukinikamata kama nimeenda kinyume, nichukue nipeleke kwenye vyombo nya sheria, *why are you killing our people?* Ni Tanzania pekee ambapo mtu anaweza akauawa *then inachukuliwa easy tu*, yaani maisha ya Mtanzania hayana thamani dhidi ya tembo, fisi, simba na mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii is *unbecoming* kabisa, hatuwezi tukathamini wanyama dhidi ya Watanzania. Naomba sana naongea *very bitterly*, tunataka tujue hatma ya hawa Watanzania wa Tarime. Kama waliwauwa watupe maiti tuzike, tunasubiria kama wapo hai, wako wapi wapelekwe kwenye vyombo nya sheria ili ndugu wale wawewe kujua, hawa walikuwa ni baba wa familia, walikuwa ni baba ambao wanatunza wazazi wao. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilinyamaza ninaposikia hizi habari za watu kuuawa, naamini Mheshimiwa Waziri atakuja atoe ufafanuzi, lakini tusijaribu kujenga picha kana kwamba wale walinzi wa kule wanatoka pale wakisema leo tunauwa kila tunayemkuta. Nafikiri na sisi kama Wabunge, kama viongozi tushiriki kwenye hili zoezi la uhifadhi, kwa maana ipi? Kwa maana hii, huyu askari anapofanya ulinzi, upo uwezekano wa majangiri pia kuwa na silaha kule kwenye yale maeneo. Wako pia maaskari wa wanyamapori wanaouawa, kwa hiyo tusijenge picha kana kwamba wale watu kazi yao ni kuuwa binadamu. Kwa sababu na wao kuna mazingira ambayo wanakuwa wanajihami maana hawajui yupi ni jangili na yupi sio jangili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ni vizuri kuipata hiyo picha, tusije tukajenga picha kana kwamba hawa maskari wa wanyamapori wao kazi yao ni kuuwa Watanzania. Hatutaki kabisa Watanzania wafe na hasa tukisikia humu Bungeni hiki chombo cha wawakilishi tunatamani maaskari wale watende haki, lakini katika yale mazingira ambayo ni ya kujihami, basi na sisi wote kama

viongozi tushiriki kwenye hili zoezi kwa maana ya kuwaelimisha wananchi wetu hayo mazingira yaliyopo huko.

Upande wa Maaskari wetu wa Wanyamapori waangalie namna ambayo wanaweza kulifanya hili hata kama ni mazingira ya kujihami, basi kwa namna bora zaidi wajitahidi kama wanaweza kuwakamata, wawakate hawa watu, lakini mazingira yale ambayo pengine ni usiku, giza, hujui kama mtu ana silaha na nini lakini hawa wa mchana nadhani wao wamefunzwa kuliko wananchi. Wananchi hawajafunzwa lakini wao ni maaskari wamefunzwa, wanao uwezo wa kulifanya hili kwa namna bora zaidi.

Kwa hiyo tunaomba mlitazame hilo kwa sababu halileti picha nzuri, tunatamani maeneo yetu yawe salama, yahifadhiwe, lakini yasihifadhiwe kwa namna ambayo basi kila kichwa kiliingia huko kinapotelea huko, kwa sababu wao wamefunzwa namna bora ya kufanya hili.

Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdulla Juma na Mheshimiwa Anjelina Adam Malembeka ajiandae.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Maliasili na Utalii. Jambo la Kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi ambayo wanaifanya, lakini pia kwa wasilisho zuri la bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili ya kuchangia; unapotaja utalii kwa kipindi cha sasa huwezi kuiacha Makete nyuma kwa sababu Makete ina hifadhi ya Kitulo, hifadhi ya kipekee hifadhi ambayo ukiambiwa utafute Bara zima la Afrika hata duniani ikiwezekana utaikuta Makete tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu umejkita kwenye mambo mawili; cha kwanza ni kuitangaza Hifadhi ya Kitulo. Kuna Wabunge wamezungumza hapa jana

kwamba tumejikita kwenye kuzungumzia vyanzo vilevile vyatutali kwa maana Serengeti, Ngorongoro tunavitaja hivyo, lakini Hifadhi ya Kitulo ambayo kwa muda mrefu na ina upekee tumekuwa tukitelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wauiangalie sana Hifadhi ya Kitulo. Kwanza afahamu jambo moja kwamba kwa upande wa Nyanda za Juu Kusini kwa maana za *highlands*, Hifadhi ya Kitulo ndio ina mlima kwa maana iko kwenye ukanda wa juu zaidi kuliko hifadhi yoyote, kwa maana kwamba ina mlima ambaao unaitwa Mtorwi Mountain ambaao una urefu wa mita 2,961 kutoka usawa wa bahari, hamna sehemu nyingine ukiambiwa utafute nyanda za juu kusini iko ndani ya Kitulo, ndani ya Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana watu wasikimbilie tu kupanda mlima Kilimanjaro, Makete pia tuna hii, waanze kuitangaza, lakini ukiwa kwenye mlima huu unaiona moja kwa moja Malawi, Kyela na Matema. Ni fursa sasa kwa Wizara ya Maliasili kuruhusu hata uwekezaji binafsi kama Serikali imeshindwa tuite uwekezaji binafsi, waweke hata *aerial cables*, kwa maana zile *aerial car cables* za kutoka kwenye millima ya *Livingstone*, ukipita kule Unyangala, ukipita kule Utengule ukipita Kitulo yenyewe, ukielekea kule Busokelo inatakiwa watu wasafiri *at least* kwa *aerial car cables* kwenda kufika Matema, Kyela na utalii wetu ukakua, kuliko kuendelea kujikita kubaki kule Serengeti na Ngorongoro na maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namsihi Mheshimiwa Waziri, sisi Makete hizi fursa zipo wazitumie wananchi. Sasa kwa nini tunapiga kelele? Ile hifadhi

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Ni nani anayesema taarifa. *Okay*, Mheshimiwa Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba niliwahi kwenda Taifa la Jamaica nikakuta mtindo wa utalii unaotumia hiyo kamba inaitwa *aerial cable* inaitwa *zipline*, unatoka mlima mmoja unakwenda mwingine kwa kuambaa angani na watalii waliokuwa wanakuja *ku-experience* jinsi ya kusafiri kwenye *zipline* walikuwa wanazidi milioni 12 kwa mwaka kwa nchi ile na uliwaingizia mapato makubwa sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Sanga unapokea taarifa hiyo.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono miwili, lakini naomba ulinde dakika yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitulo tunaiomba sana waiangalie kwa jicho la pekee, zile *aerial cables* zinaruhusu kabisa mazingira ya kule na ukipita kule utadhani huko Alaska, kumbe upo Makete jinsi ambako kumepangika. Hiyo ni fursa ya namna nytingine

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie jambo lingine kwa haraka kwa sababu dakika ni chache, ni suala la migogoro ndani ya hifadhi ya *TANAPA* kwa maana ile ya Kitulo na hii *Game Reserve* ya Mpanga Kipengele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitulo imezungukwa na maeneo mengi ambayo wananchi wanaishi. Kuna *Vijiji* vya Makwaranga, Misiwa, Nkondo, Lugoda, Kinyika na vingi ambavyo vinazunguka hifadhi hii. Hadi leo hadi *GN* inatoka tuliyoitunza ile hifadhi ni Wanamakete, lakini kilichojitokeza sasa hivi ni changamoto ya mipaka ile mikubwa kwa kiwango ambacho hakijawahi kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza muda huu kwenye *Kijiji* cha Lugoba kuna mwananchi wangu amefyekewa mazao na watu wa *TANAPA*, amefungwa ndani, wanasema ameingia kwenye eneo la hifadhi, lakini

Mheshimiwa Waziri ukisoma Sheria ya Uhifadhi inakwambia kabisa; ibara ya 16 kifungu cha 5 inasema hivi: *"For the purpose of the subsection (4), sitaisoma, the Minister shall ensure that no land falling under the village land is included in the game controlled areas."*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo lakini Wizara wamechukua kwenye makaburi ya wananchi wetu. Hii hapa Mheshimiwa Waziri ataisoma. Ukienda kule Makete sehemu kwa mfano ya Mpanga Kipengere eneo la makaburi ya wananchi ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakiishi, limechukuliwa limeingiwa ndani ya hifadhi. Juzi wananchi wawili wamefariki, wanaenda kuzika wamefukuzwa na watu wa *game reserve*. Pia angalia ukienda hapa maeneo ya Kinyika wananchi wangu shughuli zao kubwa ni za kulima viazi wanafukuzwa na watu wa *TANAPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, watu wa *TANAPA* si wastaarabu, kwamba *at least* wangkuwa na mahusiano mazuri na wananchi; wanafyeka mazao, wanazuiwa watu kwenda kuzika kwenye maeneo ambayo walikuwepo, lakini nikwambie kitu kingine hadi shule wamechukua, wanasema inasoma ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *you can be a champion to this country*, juzi tumefungua kitabu cha sensa, provision inaonyesha Watanzania tunaenda kuwa milioni 64. Mheshimiwa Waziri anaandaa mazingira yapi ya kukaa na watu milioni 100 Tanzania kwenye hifadhi ambazo wanaendelea kuwa nazo.

Je, tukiendelea na hizi sheria ambazo zinadhibiti wananchi kwa kiwango hiki, Watanzania wakiwa milioni 100 watawapeleka wapi. *You need to be a champion to this country* kuandaa sheria ambazo zitalinda nchi hii ikiwa na watu millioni 100 au 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeshindwa kujenga barabara zinazoweza kuishi miaka 20, tutashindwaje kuunda sheria inaweza ikawa na Watanzania milioni 200

mwakani; *you can be a champion* kwa kuunda sheria ambayo inatuhifadhi Watanzania zaidi ya milioni 200 kama ambayo milioni 64 wanakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru lakini namwomba Mheshimiwa Waziri...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FESTO R. SANGA: Dkt. Ndumbaro tunaamini katika hili ataandaa sheria ambayo itawa-*acommodate* watanzania milioni 200.

NAIBU SPIKA: Sasa hayo, unayoongea hata hayaingii kwenye *Hansard* kwa sababu wewe mwenyewe umeshazima *microphone* yako hapo.

Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Anjelina Adam Malembeka na Mheshimiwa Ngwasi Damasi Kamani ajiandae.

MHE. ASHA ABDULLA JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mungu kunipa uwezo leo wa kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kuweza kutoa mchango wangu mdogo kwa Wizara hii. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Ndumbaro na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii pamoja na wahifadhi kwa sababu bila wao hakuna Wizara hii. Wote wamefanya kazi nzuri sana kusaidia kunyanya ukipato katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwanzo nataka nianze kwa ile staili ya kuunganaungana, yaani nioanishe utalii huu unaofanyika bara na wa Zanzibar ili watalii wanapokuja kwa mfano huku, wanaoshukia huku moja kwa moja waambiwe vivutio vilivyokuwepo kule Zanzibar na kwa utaalam maalum ili waweze kwenda na kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, na wale wanaokwenda kule vilevile waambiwe vivutio gani nya ziada vilivyopo huku ili waje. Kwa sababu utalii wa visiwani ni tafauti na utalii wa bara; huku kuna wanyama, kule kuna samaki, fukwe nzuri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jambo hilo naomba lioanishwe vizuri zaidi kama tulivyoungana kwenye Muungano tukaweza kupata watoto, mpaka Kakonko tuna watoto sisi wengine, kwa hiyo na utalii uje kwa staili hizo hizo. Hilo ndilo langu la mwanzo ninalopenda kulisemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia ni hili la malikale na uhifadhi ambalo lina mchango mkubwa katika kuendeleza sekta hii ya utalii. Ukweli tumeona kuna sehemu hizi ambazo zimeainishwa kama zinahifadhiwa, kwa mfano Kilwa Kivinje, Songo Mnara, Bagamoyo, Kaole na Kolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku baadhi kwa mfano kama Kilwa Kivinje mimi mwenyewe nimeona yale majengo yanapotea kabisa. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, Wizara ifanye jitihada ya kufanya ukarabati kwa staili ileile ili haya yasiweze kupotea wala yasiweze kuvamiwa. Hasa haya ya Kilwa Kivinje ambayo nimeweza kuyaona, haya yanapotea, hata madirisha, milango, yote yanachomolewachomolewa. Kwa hiyo Wizara waliangalie jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia sasa hivi ni hili la kusafirisha baadhi ya wanyama. Nafikiri kuwe na *control* kwa sababu wanyama inaonekana wengi tunasafirisha tembo, chui na wengine, kwa hiyo tuwe na *control* ili wasije kwisha, halafu hizi tunu zikahamia huko katika nchi nydingine sisi tukawa hatuna kitu. Kwa hiyo, Wizara waongeze *control* katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano zamani hapo nilikuwa nasikia sana vipepeo, ndege na nini, sasa siku hizi sijasikia, hata vyura walipelekwa kule. Kwa mfano vyura

kutoka Kihansi walipelekwa kule, hatusikii tena chochote. Mwisho na sisi wenyewe tutapelekwa tukazae kule huku hakutakuwa tena watoto. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu lingine ninalotaka kulizungumzia ni hili la kuhakikisha kwamba utalii wa ndani unaongezeka kwa kuwashawishi wananchi wetu kufanya hizi ziara za kutembelea vivutio mbalimbali kwa kuwawekea *excursion*. Kwa mfano, niliwahi kwenda Kigoma nikataka kwenda kutembelea kule kwenye wale masokwemtu, nilishindwa. Bei ya kule ilikuwa ni kali sana. Kwa hivyo angalau kwa Watanzania ambao wana midomo mirefu wale ndiyo wa kuwapeleka, wa kuwapunguzia bei ili wakasemee kwengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine kwa Wizara hii ambayo lnafanya kazi vizuri, ni kwamba mshiriki kwenye makongamano ya kimataifa kwa sababu huko ndiko tutakakojuza zaidi. Ingawaje wanatuambia wamefungua *app*, wachangiaji wangapi sijui wameonekana ku-*click* au kufanya nini, hii haitusaidii bwana. Tutoke, tuvae *masks* zetu, tupige sindano za *COVID*, twende tukaitangaze Tanzania yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi hawa watu wanavyofanya kazi hii vizuri, na huyu jamaa Waziri anavyokuwa vizuri, sina la kusema zaidi ila apewe hiyo bajeti yake aliyoomba afanye kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Angelina Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo na Mheshimiwa Martha Festo Mariki ajiandae.

MHE. NG'WASI D. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kushukuru kwa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze tu kwa kuishauri Wizara hii juu ya migogoro kati ya wafugaji na wahifadhi. Wabunge wengi, hasa wa majimbo ya maeneo ambayo shughuli kuu ni ufugaji na wanapakana na hifadhi wamezungumza juu ya madhara mengi sana yanayotokana na migogoro hii kati ya wafugaji na wahifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili tu ya kushauri kwa Wizara hii. Kwanza naomba Wizara hii ifanye upya tathmini na upimaji wa hifadhi zao na waweke upya mipaka yao. Tuache kutumia mipaka ya zamani, kuna ramani tunaambiwa sijui mwaka themanini, mwaka wa ngapi, miaka kama ishirini, thelathini iliyopita. Tuache kutumia kutumia ramani hizi, tufanye upimaji mpya kwa sababu tayari kuna mabadiliko makubwa sana yamekwishafanyika kwenye ramani hizi na watu wamekwishaishi kwenye baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya vijiji Wabunge wake humu ndani unakuta kijiji chote ni eneo la shoroba au eneo la hifadhi. Kwa hiyo tukitumia ramani za zamani maana yake hata kuna baadhi ya Wabunge humu wananchi wao wote wame-*trespass*. Kwa hiyo tufanye upimaji upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upimaji huo basi kama ambavyo maeneo ya hifadhi yako *landlocked* na GN kwenye sheria zetu, basi na sisi maeneo ya vijiji, maeneo ya kulima na maeneo ya ufugaji yaye *landlocked* hivyo hivyo ili tuanze kuiwajibisha Wizara hii pale ambapo na wao wanyama wataingia kwetu na sisi tuwajibishwe pale ambapo wananchi wetu wataingia kwao. Kwa hiyo ulinzi wa kisheria uwe kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na mzungumzaji aliyepita juu ya hili suala la usafirishaji wa viumbi hai kwenda nje. Nianze tu kwa kusema kwamba kama ilivyooneshwu kwenye wasilisho la Mheshimiwa Waziri, Wizara hii inachangia asilimia 21 ya GDP ya nchi hii. Kati ya asilimia hizi 21, asilimia 17.6 zinatokana na utalii peke yake na asilimia 80 ya suala

hili la utalii kwa maana ya hii 17.6, inatokana na utalii wa wanyama. Maana yake ni kwamba watalii wengi wanakuja kwenye nchi yetu kwa sababu tuna wanyama mbalimbali ambao wangependa kuwaona, aidha, kwa sababu wa kwetu ni tofauti sana au hawapatikani kwenye sehemu nyingine ya dunia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sambamba na hayo, Wizara hii inachangia asilimia 25 ya fedha zote za kigeni zinazoingia katika nchi yetu, lakini vijana milioni 1.6 wameajiriwa katika sekta hii ya utalii ikiwa ni pamoja na madereva, *tour guides*, hotelini na sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu kwamba hili ni suala la kizalendo; tukiruhusu wanyama wetu ambao wanapatikana kwa upekee kabisa kwenye nchi yetu, wakapelekwa katika nchi zingine, maana yake tunasema watalii hawatakuja tena kuangalia wanyama hawa, lakini pia hawatakuja tena kwa shughuli zozote za kiutafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutakuwa tu tumeathiri hii asilimia 17.6 ya pato letu la ndani, bali tutakuwa tumeathiri hizi ajira milioni moja na laki sita za vijana wa Kitanzania ambao wanategemea utalii kama shughuli kuu ya uchumi katika maisha yao. Pia tutakuwa tumeathiri biashara ya Shirika letu la Ndege la ATC ambalo tumetumia fedha nyingi sana kullifufua mpaka sasa. Vile vile, tutakuwa tumeathiri sekta binafsi ya hoteli, usafirishaji, yote haya yataathirika kwa kiasi kikubwa kama tukiruhusu usafirishaji wa wanyama kwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, hebu tutafakari, kama ingekuwa madini, kwa mfano *gold*, inaweza ikapandwa na ikaota kama mti, tunategemea wale watu wangeendelea kuja kuwekeza kwetu? Wangechukua wakaenda wakapanda wakaendelea na mambo yao. Sasa hiyohivyo wanyama leo hii tukiruhusu waende wakazalishwe kwingine maana yake *species* ambayo tungetaka wale watalii waje kuiona kwa upekee katika nchi yetu itapatikana

sehemu zingine zote duniani. Hakutakuwa na haja ya mtu kufunga safari. (*Makofi*)

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Haya, naona jirani anataka kumpa taarifa, Mheshimiwa Asia Halamga.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Kanda ya Kaskazini tunategemea sana utalii na kipindi hiki kifupi cha *COVID-19* kimeathiri sana uchumi, hasa uchumi wa vijana wa Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi zimeahidiwa ajira zaidi ya milioni nane za vijana zitakazotokana na masuala ya utalii na masuala mengine ili kuweza kufikia ajira milioni nane. Naamini kabisa tukiruhusu wanyama wakatoka nje ya nchi, hatuwezi kufikia kwa sababu nchi zingine hazitakuwa na sababu ya kuja katika nchi yetu ya Tanzania. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Naona huo ulikuwa ni mchango wa Mheshimiwa Asia Halamga kwenye hii Wizara kuliko taarifa. Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, malizia mchango wako.

MHE. NG'WASI D. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akiwa anazungumzia sekta ya madini wakati bado nchi yetu hajapata nafasi ya kutosha kuwekeza huko alisema kama bado hatujawa tayari kuwekeza na madini haya yakawafaidisha Watanzania, basi tuache uwekezaji huu ili uje uwafaidishe Watanzania pale ambapo tutakuwa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama bado Watanzania hatujawa tayari kutumia wanyama wetu vizuri ikatuletea tija, kuliko kukubali tuwasafirishe kwenda nje, tuwaache ili tutakapokuwa tayari wawafaidshe Watanzania

wenyewe. Rai yangu tulinde ajira hizi za vijana ambazo zinakwenda kupotea, tulinde mapato haya ambayo tutayapoteza kama tukiruhusu suala hili likaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, napenda tu kuchangia kwenye suala zima la misitu. Tunaishukuru sana Serikali yetu, imekuwa ikiweka mkazo sana kwenye upandaji wa miti, misitu ya Serikali na misitu ya watu binafsi. Hata hivyo, changamoto kubwa kwenye sekta hii ya misitu imekuwa ni uchomaji moto wa misitu. Wote tunakubali kwamba kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa mazingira ambao umesababisha mabadiliko ya tabianchi yanayoutuathiri nchi na hata dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wamejitolea kwa rasilimali zao wenyewe kupanda misitu kwenye mikoa mbalimbali ya nchi hil ambayo inatusaidia. Kwanza inaisaldia Serikali kutunza mazingira; lakini pili, inasaidia sana katika suala zima la kuleta mvua na kusaidia kwenye kilimo ambacho zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania tunakitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye misitu ya Serikali nafahamu suala hili la moto ni changamoto, lakini wao wana watu ambao wanawasaidia...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Sasa naona umeishia neno wanasaidia, malizia sentensi yako.

MHE. NG'WASI D. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwenye misitu ya Serikali wao wana vijana wao ambao Serikali imewaweka kwa ajili ya kusaidia kulinda moto, kitu ambacho mtu binafsi hana rasilimali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Wizara hii itafakari upya namna gani wawekezaji wanaowekeza kwenye misitu nao wanalindwa kwenye suala hili la moto, ikiwa ni pamoja sasa na Serikali kuona kama inaweza kusaidia kuweka walinzi hawa kwenye misitu ya watu binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Festo Mariki na Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau ajiandae.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa na mimi nitumie fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri wanazofanya. Kwa kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni; wanafanya kazi vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa harakaharaka; kwanza katika Mkoa wangu wa Simiyu. Mkoa wangu unaitwa jina la Simiyu, maana yake ni mto. Kuna Mto unaitwa Simiyu, hauna maana yoyote. Ni mto ambao mvua zikinyesha unapata maji, mvua zikikatika kwa muda mchache mto unakauka. Hauingizi shughuli yoyote ya kiuchumi, hauna chochote kiatalii, hauna tija yoyote. Isipokuwa tu tulita Simiyu, ilikuwa ni vita vya makao makuu ya mkoa, yatakuwa Maswa na wapi, kuna wenzetu wakaamua kubadilisha jina badala ya kuuita Mkoa wa Maswa ukawa Mkoa wa Simiyu ili kuchengesha tu Makao Makuu ya Mkoa. Sasa vita hivyo vimeisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Game Reserve* inaitwa *Maswa Game Reserve*; kwa nini Mkoa huu usiitwe Mkoa wa Maswa tuka-*promote* hiyo *game reserve*, *tukai-market*, *tukau-market* mkoa wetu. Najua sikuwepo wakati wa michakato hii, sikuwa Mbunge na nadhani ningekuwa Mbunge pangechimbika. Hata kama makao makuu yangekwenda sehemu nyingine, lakini mkoa ule ungeitwa Mkoa wa Maswa

tuka-*promote* Game Reserve ya Maswa kuliko mto ambao unakausha maji na usiyokuwa na maana yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ruvuma wame-*promote* mto wao, una maana na historia. Kilimanjaro kuna Mlima Kilimanjaro; Manyara wana Mbuga ya Manyara; Katavi kuna Mbuga ya Katavi; hata huko Chato mnataka leo tuweke Mkoa wa Chato, uitwe Burigi. Ni hilo tu nimesema nianze nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine la ng'ombe kwenda kwenye hifadhi. *Control* ya ng'ombe kwenda kwenye hifadhi, wewe ni shahidi, inahitaji *brain* ya mtu mmoja tu. *Just the brain of one person*; anaswaga ng'ombe hata 5,000 wanakwenda sehemu fulani. Kwa hiyo *decision* ya ng'ombe kwenda kwenye hifadhi ni ya binadamu, tena mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali tunapo-*charge* kila ng'ombe, yaani adhabu inakwenda kwa ng'ombe mmojammoja, hiyo hapana. Hebu turudi tujipange upya tufikirie adhabu. Hivi kwani adhabu ya mtu ambaye anaendesha gari ndogo aka-overspeed na anayeendesha gari kubwa adhabu yake ni tofauti? Au kusema unaendesha basi, basi wewe kwa sababu umebeba watu wengi ukivunja sheria ina maana adhabu yake inakuwa ni tofauti na gari ndogo? Adhabu ni adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anapoingiza ng'ombe wengi kwa sababu *discretion* ni ya mtu mmoja, basi adhabu iangaliwe, kama alivyozungumza Mbunge wa Kiteto hapo, aadhibiwe aliywapeleka ng'ombe, lakini siyo ku-*charge* gharama ya ng'ombe mmoja mmoja. Huo kwa kweli ni uonevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nimesikia na wewe umekuwa balozi wa kutetea mjis. Huyu mjis ambaye yuko Ujerumani ambaye ni *dinosaur*, juhudhi hizo...

NAIBU SPIKA: Nani huyo kanitunukia ubalozi? Maana sina taarifa.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa mama Riziki Lulida amekunukia.

NAIBU SPIKA: Ahaa, amenitunikia? Nilikuwa sina habari.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, amekutunikia, *u-champion* wa kutetea yule mjusi arudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba niseme hivi; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sisi ni wajumbe au tuseme ni *member* wa Umoja wa Mataifa. Sisi ni *member state*, tuko katika mikataba ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *UNESCO* inasimamia masuala yote ya elimu pamoja na haya masuala ya maliasili. Mwaka 1970 tuliingia mkataba ambao unajulikana kwa jina la *Convention on the Means of Prohibiting and Preventing the Illicit Import, Export and Transfer of Ownership of Cultural Property*. Huu mkataba tuliungia Paris tarehe 14, Novemba mwaka 1970 na nia ni kulinda maliasili za nchi hizi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, *UNESCO* ndio anayesimamia masuala yote ya ulinzi wa hizi mali za urithi katika nchi husika. Sisi tumeanza juhudzi za kufuatilia mjusi huyu toka mwaka 2005. Cha kushangaza Wizara ya Maliasili badala ya kwenda *UNESCO* kupeleka malalamiko kule kwa sababu *UNESCO* ina tume yake hapa nchini na tume hiyo ndiyo yenye kazi ya kwenda kupeleka hizi hoja kule *UNESCO* kuishtaki Serikali ya Ujerumani ili iweze kuturudishia mjusi wetu, lakini badala yake Wizara ya Maliasili inaongea na watu wa *museum* (makumbusho) ambayo inahifadhi mjusi yule.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule anayehifadhi mjusi ni mtu ambaye tunaweza tukasema labda ni mwizi. Haiwezekani wewe unadai kitu chako cha wizi, badala ya

kwenda mahakamani kuomba kitu chako unakwenda kwa mwizi kwenda kujadili naye akurudishie hicho kitu. Naomba nikwambie, Kamati za Bunge zitakwenda huko, watakwenda watu wa maliasili watapokelewa vizuri na balozi, watapokelewa vizuri na watu wa *museums*, watakwenda watamwona mjusi lakini hakuna chochote kitakachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali, tunaomba Wizara waongee na Tume ya UNESCO waandike barua kwenda kwenye tume ambayo itakwenda kwenye vikao vinavyokubalika kisheria kutokana na mkataba wa mwaka 1970, tudai *officially* mjusi huyu arudishwe. Atarudishwa kwa gharama ya Serikali ya Ujerumani na atakuja kupangwa na kuwa *assembled* kwa gharama ya Ujerumani. Naomba hilo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Muda wako umeshakwisha Mheshimiwa Nyongo. Mheshimiwa Kanyasu, muda wake wa kuchangia umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Martha Festo Mariki, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama ajiandae.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Maliasili. Kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo wameendelea kufanya kazi vizuri katika Wizara hii. Hata hivyo, kipekee sana nampongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchache wa muda, moja kwa moja nitaanza kwa kuchangia kwa Mkoa wangu wa Katavi kuhusiana na suala la *TFS* kutokana na tozo

mbalimbali ambazo wamekuwa wakizitoza kwenye vitu vinavyotengenezwa kwa mbao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Katavi, *TFS* wamekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa wananchi. Huwezi kuamini, mfano mwananchi anaponunua kitanda chake pale Mpanda Mjini na anataka akipeleke katika Wilaya ya Mlele, Halmashauri ya Mpimbwe, kumekuwa na tozo mbalimbali ambazo zimekuwa kama *double payment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, juzi tu hapa kuna wananchi ambao wamenunua vitanda vyao na meza Mpanda Mjini na wanavipeleka katika Halmashauri ya Mpimbwe. Vitanda hivi, huyu mtumiaji anakuwa ameshalipia na amepata risiti lakini wanavyopita kwenye mageti wanatozwa tena pesa na watu wa *TFS* wakiambiwa tena walipie gharama za vitu hivyo. Hii imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aje ashughulikie suala hili kuangalia tozo hizi, ikiwezekana ziondolewa kwani wananchi hawa wamekuwa wakipata adha kubwa na watu hawa wa *TFS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwa kuna migogoro mbalimbali baina ya wananchi na *TFS* kwa mfano, katika Wilaya ya Mlele Kata ya Kamsisi; kumekuwa na mgogoro mkubwa baina ya watu hawa na mgogoro huu umekuwa ni wa muda mrefu, wananchi wamekuwa wakichomewa nyumba zao, wananchi wamekuwa wakichomewa mazao yao, lakini pia *TFS* hawa wamediriki kabisa kuwachomea hata maduka wananchi, wananchi hawa wamefanyiwa ukatili, mgogoro huu umekuwa ni wa muda mrefu na Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukimwambia mara nyingi na hata Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alikuwa anafahamu suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Serikali yetu sikivu iweze kushughulikia mgogoro huu ili wananchi hawa waweze kuishi kwa amani, kama tunavyojuwa ardhi

haiongezeki, lakini wananchi wanaongezeka, tuombe sana tuangalie mgogoro huu, ikiwezekana kabisa tuumalize mgogoro huu kwani wananchi hawa wamekuwa wakipata adha, mama zangu na baba zangu wa Kijiji cha Kamsisi, Kata ya Utende, maeneo ya Ilunde na Illela wamekuwa wakichapwa sana, wakiadhibiwa, wakiambiwa kwamba wanaingilia maeneo ambayo ni ya mapori. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri waje washughulikie suala hili, ikiwezekana waje katika Mkoa wetu wa Katavi, waweze kufanya ziara, waje wawasikilize wananchi, wasiwe wanasikiliza tu watendaji wakati mwingine imekuwa ikipotoshwa. Hivyo, waje wafanye ziara kule wajihakikishie wajueje, mwenye kosa ni mwananchi au wenye kosa ni watu hawa wa *TFS*. Niwaombe sana Wizara wafanye ziara kule ili waweze kujua nini chanzo cha tatizo hilli na ikiwezekana tulimalize ili wananchi wetu waweze kuishi kwa amani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kumekuwa kuna tatizo la kubambikiziwa kesi. Watu wa *TFS* wamekuwa na tabia ya kuwambambikizia kesi wananchi wale wanaozunguka *Katavi National Park*. Sasa tunachotaka wananchi wale wa Katavi waweze kufurahia kuwepo kwa *Katavi National Park* hifadhi ambayo Mwenyezi Mungu ameibariki na siyo waone ni kero kuwa karibu na hifadhi hiyo. Wamekuwa wakibambikiziwa kesi mbalimbali, wakiambiwa kwamba wengine wamekutwa na nyara za Serikali, wengine wamekutwa sijui na nyama za pori kama hizi za Nyati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aje katika maeneo hayo atafanye ziara aangalie kesi hizo hasa zile ambazo zimekuwa hazina vithibitisho, ikiwezekana ziondolewe. Wananchi wa vijiji hivi wamekuwa wakihangaika, wananchi wa Vijiji vya Majimoto, Mamba, Chamalendi na Mwamapuli wamekuwa wakiteseka sana. Hivyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri afanye ziara Mkoa wa Katavi, tunataka wananchi wa Mkoa wa Katavi wafurahie kuwepo kwa *Katavi National Park* na siyo hifadhi hiyo iwabugudhi wananchi. Wananchi tunawapenda na

hifadhi pia tunaipenda kwa sababu inatuingizia mapato. Tunachotaka tu ni kwamba migogoro hiyo ikiwezekana iishe na hasa hiyo migogoro na kesi ambazo hazina uthibitisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, ajiandae.

MHE. MARTHA N. GWAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwa mmoja wa wachangiaji katika Wizara hii muhimu kabisa ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa moyo wa dhati kabisa na kipekee nipongeze Wizara hii kuanzia Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri na wataalam wote waliopo katika Wizara hii, kwa jitihada madhubuti wanazozichukua kuhakikisha kwamba suala la utalii Tanzania linatangazwa vilivyo na pia tunapata watalii wa kutosha. Naomba nitoe pongezi hizo za dhati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba nijikite kwenye utalii; utalii ni sekta muhimu sana kwa nchi yetu ambayo inatuingizia pato, lakini pia vijana wetu wanapata ajira, lakini pia pesa za kigeni, kwa hiyo unaweza kuona umuhimu wa sekta hii ya utalii nchini kwetu ilivyokuwa kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite kuelezea watalii wanaotoka nje kuja Tanzania. Mikakati ya Serikali kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni kujitahidi kuhakikisha namba ya watalii wanaotoka nje kuja Tanzania inaongezeka kwa miaka mitano ijayo. Mikakati hii ni mizuri na naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati hii itafanikiwa tukifanya mambo matatu; cha kwanza lazima tukubali kuwa *creative* na *innovative*. Lingine, tukubali kuwa *competitive*, lazima tukubali kushindina na wenzetu na la tatu lazima tukubali *ku-learn from others*, waliofaulu walifanyaje na sisi tunafanyaje, kwa nini tunakwama hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia Tanzania ni ya pili kuwa na vivutio vingi duniani, lakini kwa nini Tanzania siyo ya kwanza au ya pili au tatu, au ya tano kwa namba ya watalii wanaoingia Tanzania, ina maana hapa kuna shida ambayo hatujaitatua vizuri na ndiyo maana tunashindwa kufikia ile idadi ya watalii kuwa wengi kwetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukajifunza kutoka kwa wenzetu wa Comoro, Egypt na *South Africa*, wamefanya nini, kwa nini wenyele wanapata namba kubwa ya watalii wanaokuja nchini mwao na sisi Tanzania hatupati namba hiyo, lazima kuna shida ambayo inabidi tujifunze na tukubali kubadilika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, napenda kuongelea sana *quality of service* inayotolewa baada ya wageni kuja Tanzania. Mheshimiwa Waziri na timu yake wanaweza wakatangaza matangazo yote ya *promotion* za utalii watu waje Tanzania. Wanaweza wakatumia wacheza mpira, ma-*celebrity* tofauti tofauti, lakini, je, wameshawahi kuijuliza swali mtalii akifika hapa anapata huduma inayostahili? *The quality of service is it equal to value of money?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama anakuja kuangalia tembo Tanzania na hapati huduma nzuri na tembo huyo huyo yupo Kenya ina maana ata-*opt* kwenda kwenye *service* nzuri ya Kenya na asije Tanzania. Kwa hiyo tukitoa *quality service* tutamvutia huyu mtu aseme Kenya kuna tembo mfano, Uganda kuna tembo na Tanzania kuna tembo na *opt* kwenda Tanzania *because I will get a quality service* na nitapata huduma nzuri inayotakiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nime-*highlight* mambo machache ambayo naona kama ni tatizo na *of course* tumesafiri sana unakutana na watu kwenye ndege popote huko duniani, wanakwambia Tanzania mnavivutio vizuri, lakini kuna shida kwenye huduma zenu. Kwa hiyo naomba Wizara wavi-note; cha kwanza, *service provider* wetu *waiter, waitress, guide, chefs* na *receptionist* hawa ni *face* ya watalii wote wanavyoingia nchini. Hawa watu ni lazima wapewe mafunzo mbalimbali, *training* mbalimbali ya kuhakikisha kwamba mtalii anapofika hapa ye ye ndiyo kioo cha kumpokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Waziri na Naibu na Waziri na timu yake kumtangazia kuna Ngorongoro Tanzania, akishafika anakutana na nani, anakutana na *service provider* atahitaji kulala, anahitaji kula, anahitaji kutembezwu hawa watu Wizara inawaangaliaje, ili wao watoe huduma nzuri, huyu mtalii aridhike, aseme badala ya kwenda Kenya nataka niende Tanzania kwa sababu nitapata huduma nzuri. Hilo ni tatizo (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ni lugha, watoa huduma wengi Tanzania wanaongea Kiswahili na Kiingereza, lakini wangeongeza lugha ya tatu kwa mfano, Wachina wengi wanapenda kwenda kutembea Thailand kwa nini? Ina maana kule wanaongea Kichina, kuna mtu anaye-*guide* anaongea kachina, anavutika kwenda kule, lakini barabara zetu ni mbovu za kwenda na ndani ya utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine *network, communication network*, siku hizi kuna kitu wanaita *live*, mtu akiwa kule kwenye mbuga za wanyama ataonyesha *live* nipo na simba kwa hiyo *network communication iboreshwe...* (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana.

MHE. MARTHA N. GWAU: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri niliwhahi kusoma kuna mtalii alikuja hapa akawa anashangaa namna ambavyo alikuwa anaombwa zile raba na mtu aliyekuwa anamwongoza, kwamba utakapokuwa unaondoka naomba uniachie hiso raba.

Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge kukushukuru kwa kupata fursa ya kuzungumza, lakini kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kazi kubwa na kwa ubunifu ambao wanao ili kuendeleza sekta ya uhifadhi na utalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Mheshimiwa Waziri baada ya kumweleza changamoto za wananchi wangu wa Jimbo la Madaba alikwenda mwenyewe, kwenda kuwasilikiza na kuanza mchakato wa kumaliza changamoto zao. Namshukuru sana Waziri na naomba aendelee na moyo huu huu. Nimemwona anakwenda Tunduru, nimeona anakwenda sehemu mbalimbali ndani ya nchi yetu kwenda kuwasikiliza Watanzania na kuona namna gani tunamaliza changamoto zao na naamini *approach* aliyonayo itatufikisha salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina changamoto kubwa sana, tumeipa mzigo mkubwa sana. Nchi hii inawategemea wakulima, inawategemea wafugaji, inawategemea watalii na inawategemea wahifadhi. Sekta hizi zote zinategemeana na Watanzania wanaongezeka kwa idadi. Changamoto ya Mheshimiwa Waziri ni namna gani

tunaweza ku-*accommodate* tuka-*strike balance* mionganini mwa wafugaji, wakulima na hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu Mheshimiwa Waziri azingatia ushauri uliotolewa na baadhi ya Wabunge hapa wa kurejea upya michoro ya nchi hii ili kuweka bayana maeneo ya mifugo, maeneo ya kilimo na maeneo ya hifadhi ili kuhakikisha kwamba kila kitu kinapewa kipaumbele na Watanzania wanaishi kwa utulivu na amani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri pia aendelee kuangalia mgogoro wa wananchi wa Madaba kwa eneo la Slow ambalo tayari ameanza kulifanyia kazi. Wananchi hawa pamoja na kazi nzuri aliyoifanya Waziri, bado hawaamini kwamba lile eneo ni mali ya maliasili, wanaamini kwamba wameporwa.

Naomba jukumu la maliasili siyo kushambulia wale wananchi, jukumu la maliasili ni kukaa nao chini na kuelekezana kwenye michoro, ni wapi inaonyesha kwamba ni mali ya maliasili na wapi ni mali ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maeneo kama alivyosema Mheshimiwa Ng'wasi, yanatumia michoro ya zamani sana na tayari haya maeneo yameshatangazwa kuwa vijiji, Kijiji cha Nderenyuma kimetangazwa kwenye ziara ya mwisho ya Mheshimiwa Rais Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli ameitanganza Nderenyuma kuwa Kijiji. Mbangamawe ni Kijiji cha muda mrefu, maeneo haya yote sasa maliasili wanasema kwamba ni kivuko cha wanyama kwa hiyo wananchi wasilime mazao ya chakula kama mahindi. Ni ushauri mzuri, lakini ukiwa *participatoryutatusaidia* kumaliza mgogoro huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia...

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Nani anayetoa taarifa. Waheshimiwa Wabunge ukiomba taarifa inabidi usimame ili nikuone sasa nikupe hiyo nafasi. Mheshimiwa Neema Mgaya.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa kaka yangu Mheshimiwa Joseph Mhagama kwamba tatizo hili la migogoro hii kati ya mipaka ya mapori ya akiba na hifadhi na vijiji vingi ndani ya Tanzania imekuwa tatizo kubwa sana na Wabunge wengi wanalalamikia tatizo hili. Ifikie mahali sasa Mheshimiwa Waziri waweze kutatua migogoro hii, wakae waende kwa pamoja na Waziri wa Ardhi ili mkienda kumaliza tatizo mniamaliza moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kule Wanging'ombe, alikuja Naibu Waziri wa Ardhi mwaka 2018, lakini mpaka leo ille tatizo halijamalizika, hebu wakae kwa pamoja na Wizara ya Ardhi muweze kumaliza matatizo haya...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema ahsante kwa mchango wako. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Joseph Mhagama.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, napokea kwanza taarifa ya dada yangu Neema Mgaya kwa sababu ya muda...

NAIBU SPIKA: Naambiwa na kengele ilikuwa imeshagonga hapa mbele.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri basi tuendelee kushirikiana na wananchi wa Madaba kumaliza changamoto zao kwa njia ya kushauriana. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ajiandae.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na timu yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwangu nitatoa tu ushauri wa kuongeza mapato katika Wizara hii. Nchi yetu hii imejaliwa misitu mingi sana na misitu hii imejaa miti dawa na mimea dawa. Ndiyo maana hata imefikia hatua ina maana tumekabiliana na ugonjwa huu wa *Covid-19*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana, Wizara imeangalia mali hizi bila kuzifanyia kazi, hata katika taarifa yake hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna sehemu iliyotaja miti dawa, hakuna sehemu iliyotaja dawa zetu za asili. Nimwombe sasa, naamini lametaja tu eneo ambalo kwa kweli ni la vinyago, kwamba vinyago viwekwe kwenye maduka ya utalii. Nishauri kabisa na dawa za asili ziwekwe kwenye *pharmacy* za kitalii. (*Makofii*)

MHE: FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Flatei Massay.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa ndugu yangu Shekilindi asisahau ku-*declare interest* kwamba yeye pia ni mtalaam na ana madawa hayo kuititia hiyo miti mishamba, hiyo ya *Covid* na sisi tumetumia humu. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Kwa ile kanuni yetu hawesi kusema hayo kwamba yeye ana maslahi kwenye hilo jambo, kwa sababu yeye anachangia kuhusu misitu yote, maana ukisema una

maslahi lazima ututajie kiasi gani, sasa ye ye si anaauza dawa yake jamani inaitwa Shekilindi, watu wakanunue huko.

Mheshimiwa Shekilindi malizia mchango wako.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, mimi sikutaka kufanya hivyo kama Massay anavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kuishauri Serikali sasa, kwamba watalaam wetu washirikiane na watalaam kama sisi kuhakikisha kwamba tunaanzisha viwanda vy a kutengeneza dawa zetu hizi. Pia kama unavyofahamu nchi za wenzetu Ulaya kule wanakuja kuchukua miti yetu huku na anaenda kutengeneza dawa, sisi ndugu zangu tupo wapi na nchi hii ina watalaam ambao ni wabobezi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali yangu Tukufu kwamba, hebu sasa watalaamu wakae na sisi tuhakikishe kwamba tunaenda kujenga viwanda, *then* tunaenda kutengeneza dawa zetu, ukizingatia sasa hivi deni, Wizara ya Afya inadaiwa na *MSD* mamilioni ya fedha, karibu asilimia 93 za dawa zinatoka nje, lakini tukishajenga viwanda vyetu hivi kwa sababu *raw materials* zetu tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi niishauri Serikali kwa kweli isichukulie jambo la mzaha kwamba asilimia 93 hizo hatuwezi tena kwenda kuzichukua nje tuna uwezo wa kujenga viwanda vyetu hapa na dawa za kutosha zikatengenezwa hapa nchini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo niiombe Serikali iwe *serious* juu ya jambo hili, kwa sababu watu wanasema sijui nini taharuki ndiyo maana sasa hivi hapa hatuvai barakoa kwa sababu dawa za *Corona* zipo kwa watu ambao ni watalaam wa dawa za asili. Kwa hiyo, Serikali iwashike mkono watu hawa, iwa boreshee ili pato la Serikali hususan Wizara hii kama inaingiza asilimia 17, basi naamini itapiga mara mbili asilimia 34. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali iwe *serious* juu ya jambo hili, iwashike mkono watu hawa ili wazungu nao washike adabu kwetu, wajue kabisa kwamba Watanzania nao kumekucha, siyo wachukue mizizi yetu, waende wakatengeneze dawa *then* waje watuuzie sisi. Mfano, nchi ya Nchi ya China, Bara la Asia inatengeneza dawa zao za asili, lakini sisi tunakimbia kivuli chetu, kwa nini? Hivi tumerogwa na nani, namwomba sana Mheshimiwa Waziri alichukue hili ili akae na wataalaam kama sisi na watalaan hao tunaamini wa nchi hii ni waelewa na wana uwezo mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu sasa ingekuwa Wizara haina...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele imegonga.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa shukrani sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, ajiandae.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kuwa mionganoni mwa wachangiaji. Nitajikita kwenye utalii wa ndani, sote tunafahamu kwamba sekta hii ya utalii ni sekta muhimu na mchango wake kwa Taifa takribani kwenye *GDP*inachukua asilimia 21. Mimi nieleze tu utaona hapa katika asilimia 21, asilimia karibu 17 ni fedha zinazotokana na watalii kutoka nje ya nchi. Sasa utaona kwa kiwango gani utalii wa ndani haufanyi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri tu, Wizara ya Maliasili na Utalii ijikite kwenye *manmade tourism*. *Manmade*

tourism itatusaidia, kwa mfano, ukienda kule Dubai *una-drive* kilometra 100 kutoka *city center*, kuna eneo unakwenda linaitwa *Camel Ride*, unafika pale unapanda ngamia tu, unaendesha ngamia, ukitoka unapanda kwenye V8unaruka ruka. Yaani jambo lenyewe ni la kawaida kabisa lakini watu wanakwenda na wanapata fedha kule Dubai. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii atusaidie. Aongeze thamani ya maeneo yetu ya utalii, kwa kuwekeza kwenye utalii ambao tunauzungumzia *manmade tourism*.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine watu wengi wamezungumzia migogoro baina ya wananchi na wahifadhi. Naomba niseme hili ni janga la Taifa, hili tulipofikia sasa ni janga la Taifa. Kuna Watanzania wanaishi kwenye nchi hii kama wageni, hasa wanaoishi maeneo ya mipaka ya hifadhi, hawajui kesho yao. Sasa jambo hili lifike mwisho, tutakuwa tunajadili kila siku humu tufike mahali tuseme inatosha. Hatuwezi kuwa tunakaa humu tunajadili kitu hicho hicho wakati wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali naona hili jambo sio tu la Wizara ya Maliasili na Utalii. Niishauri Serikali, ije na mpango wa pamoja shirikishi. Wananchi washirikishwe lakini twende pamoja, kwa mfano, *custodian* wa masuala ya ardhi ni Wizara ya Ardhi, Maliasili wao wanakabidhiwa tu kulinda. Leo hii mimi nashangaa kuona Maliasili nao wanakwenda kuweka mipaka, sasa kazi ya Wizara ya Ardhi itakuwa ni kazi gani? Nadhani Wizara ya Ardhi iachiwejukumu lake, libaki pale pale na kuna baadhi ya maeneo hakuna migogoro, Wizara ya Ardhi imeshafikia imefanya hadi mpango wa matumizi bora ya ardhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano pale kwangu Mlimba Kijiji cha Ijia kimeshasajiliwa kwa mujibu wa sheria na tayari kina mpango wa matumizi bora ya ardhi, lakini mpaka leo wananchi wale wanaishi kama ugenini. Hivi punde wiki iliyopita walikuja hapa wananchi tisa wamelala pale stendi, asubuhi napewa taarifa. Eneo hili halina mashaka, kijiji

kimesajiliwa kwa mujibu wa sheria na wananchi wale wangepaswa kuishi bila bugudha. Niombe na niwapongeze pia Waziri wa Ardhi kwa kweli kuna baadhi ya maeneo tayari mipango ya matumizi bora ya ardhi yamekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tushirikiane kazi ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni kuomba ramani kwa Wizara ya Ardhi, waende wakazingatie hizo ramani. Yaani hilo jukumu sio la Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara inajipa mzigo ambao isingefaa ijipe, eneo hilo nadhani tulitazame.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende katika eneo lingine ambalo pia hapa nimshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri. Ametusaidia wananchi wa Jimbo la Mlimba kutoa vibali vya kuvuna mpunga wetu, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto inayokuja kwa wananchi wale, naomba, tufanikiwe kwenye eneo hili Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha basi atoe tamko. Wananchi wangu wamekuwa waoga sasa, Meneja wa TAWA anasema njoo uombe vibali, wananchi wanasesma wanatuorodhesha ili watukamate tena. Kwa hiyo, hawawezi tena kuvuna. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba shemeji anapokwenda kuhitimisha bajeti yake atoe tamko kwamba, suala la kuhakikisha wananchi wa Mlimba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunambi Taarifa Rasmi za Bunge hazitajua nani ni shemeji yako humu ndani.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ni shemeji yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, Waziri aje atoe tamko hapa ili awatoe hofu wananchi wa pale Ijia kwamba, Wizara imeruhusu wavune kwa wakati, wakimaliza kuvuna maeneo yale ni vyema sasa yakaendelea na shughuli ambazo zimekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, nizungumzie kuhusu hawa vyura walioelezwa, vyura ambao wanazaa na kunyonyesha, wapo pale Kihansi Udagali. Sasa niombe tu ndugu zangu Mheshimiwa Waziri atusaidie, kuna watu hawa *academic tourism*, wakija pale na wenzetu wa *TANESCO* wamefanya kazi nzuri sana wameweka hadi *rest house* pale. Kwa hiyo, mtalii akija pale analala vizuri, waje waone *academic tourism*, waje Mlimba pale Kihansi kuna vyura wanaonyonyesha na wanazaa. Duniani kote hawapatikana wanapatikana pale tu Kihansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka niliseme, kuna hoja hapa ya msingi, nihitimishe kwenye hoja hii ya eneo hili la utalii wa ndani. Tukijuliza hapa maswali Wabunge wote humu ndani ni wangapi wameshafanya utalii wa ndani hapa? Jibu utakalopata ni wachache kati yetu. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Wabunge, tuwe sehemu ya utalii wa ndani, twende tukahamasishe kama mabalozi wa utalii wa ndani ili nchi yetu ipate fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na Mungu atubariki sote. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia hii nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika sekta hii ya Maliasili na Utalii. Jambo la kwanza, nawapongeza sana viongozi wa Wizara kuanzia kwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote na Wahifadhi wote wamefanya kazi nzuri sana, pamoja na changamoto ambazo zinawakabili kutokana na ugonjwa huu wa *COVID 19*. Hongera sana kwa kazi ambayo wameifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kabisa kwamba, sekta ya utalii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu,

sisi sote tunajua hilo, mchango wake kwenye pato la Taifa, kwenye ajira na kwenye fedha za kigeni ni kitu muhimu sana. Hata hivyo, wengi wanasema Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii, lakini nafikiri kwa sasa hivi ni nchi ya nane, sio ya pili tumeshaharibu, tumeshavuruga vuruga kwa hiyo, sasa hivi Tanzania sio ya pili tena bali ni nchi ya nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili nchi iweze kunufaika na vivutio vya utalii vilivyopo, lazima tuchukue mikakati ya makusudi ya kuhakikisha kwamba, tunaiendelea hii sekta ya utalii. Sasa ili kufanya hayo nitapendekeza mambo machache, lakini kwa sababu ya muda sitaweza kuyasema yote. Nataka kusema kwamba, nchi yetu ina bahati ni nchi yenye Mlima mrefu kuliko milima yote katika Afrika. Ni nchi ambayo mwanadamu wa kwanza wa kale alipatikana Tanzania. Ni nchi yenye Maziwa, ni nchi yenye bahari, yenye milima, yenye kila kitu, lakini tatizo tulilonalo hatujaweka mikakati ya kutosha ya namna ya kutumia huu utajiri ambaao Mungu ametupatia. Kwa hiyo, tufike mahali tuweke mikakati ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi nchi kumi zinazoongoza kwa utalii duniani Tanzania hatumo. Inaanza Ufaransa ambayo ina watalii milioni 89, kuna *Spain* milioni 82, USA milioni 79, China milioni 62, *Italy* milioni 61, *Turkey* milioni 45, *Mexico* milioni 41, *Germany* milioni 38, *Thailand* milioni 38, UK milioni 36, Tanzania hatumo wala Afrika hatumo, pamoja na utajiri wote huu tulionao. Hivyo, ni lazima tukae chini tuijilize kwa nini sisi tunakosa kuweka mikakati ya makusudi na kuweka uwekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo lazima tuhakikishe tunalifanya, ni kutengeneza miundombinu thabiti ya kuvutia utalii nchini. Hii Serikali wameanza kufanya vizuri, lakini hapo katikati tumeshajichanganya. Tumeamua kuchukua mapato ya utalii yale tumeyapeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Sasa tunaziacha Taasisi za Uhifadhi hazina fedha za kujenga miundombinu, halafu tunataka kujenga

utalii, nani atatangaza utalii? Tutauendelezaje katika utaratibu wa namna hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuna haja ya kukaa chini na kulitafakari, ili tuone haya Mashirika ya Hifadhi sasa yawe na mapato yake, yawekeze, yajenge miundombinu, watu waende mahali sehemu mbalimbali, wakale maisha, hapo ndio tutaijenga nchi yetu, bila kufanya hivyo hatuwezi kufika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mbozi kuna Kimondo cha aina yake, ni moja ya vimondo nane duniani, kiko pale Mbozi. Naishukuru Serikali imewekeza pale, lakini bado hatujakitangaza vya kutosha. Tunayo maji moto kule Mbozi, hatujatangaza vya kutosha. Sasa na maeneo mengine yote ya mali kale ambayo hatujayatangaza lazima tuwe na mkakati wa namna ya kutangaza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini tunatakiwa kufanya katika kutangaza? Tunayo *TBC, Channel Two* ambayo tuliweka mahususi kwa ajili ya kutangaza, lakini je. hiyo ndiyo itawafikia watalii wote tunaowahitaji? Lazima tutafute namna ya kutangaza utalii, tutumie mbinu gani, tuwekeze, bila kuwekeza hatuwezi kupata vitu. Hatuwezi kupata fedha, lazima tuwekeze kwenye matangazo ya kutosha ili kuweza kuvutia utalii. Hapa Dodoma kwa mfano, Bunge tumekaa miezi minne niambieni ni sehemu gani ambapo sisi tumeenda kula maisha, wapi? Sijapaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujawekeza vya kutosha, kwa hiyo, lazima tuwekeze mkakati kuwekeza ili kusudi watu wahakikishe kwamba wanaenda kula maisha. Naomba kwa sababu, Kamati imependekeza, tuanzishe Mamlaka ya Kuendeleza Utalii. Naunga mkono hii mamlaka ni muhimu sana, ikafanye hii kazi, ikalitangaze Taifa letu, ikatangaze vivutio vyetu, tuweze kuleta maendeleo, tuweze kupata fedha nydingi, tuweze kutengeneza ajira mbalimbali kwa Watanzania, hii itakuwa ni kazi nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imependekeza tuanzishe Mamlaka ya Misitu Tanzania badala ya kuwa Wakala. Naunga mkono, lakini nitaunga mkono tu wakimaliza tatizo lililopo Mkoa wa Songwe la matumizi ya mkaa. Walizua wananchi kwamba, wasitumie mkaa, wasivune mkaa, lakini tunajua kabisa matumizi ya mkaa yapo, lazima yawekewe utaratibu mzuri na wananchi wa Songwe wapate sehemu hiyo, hiyo itawasaidia sana. Kwa hiyo, nitaunga mkono kama haya mambo yatakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema bahati mbaya naona muda haukuwa upande wangu, lakini niwahamasishe Watanzania twende tukale maisha, ndipo tutajenga uchumi imara. Tafuta fedha, katumie, utapata maendeleo, Mungu awabariki, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge, mimi nasikiliza hapa michango yenu wote, kuna Wabunge wanasema gharama ziko juu, gharama zishuke. Wakati huo huo tunataka kuunda vyombo zaidi ya hivi vilivyopo, ambavyo navyo hakuna mtu mwagine wa kuvilipia lakini ni mlaji wa hizo huduma. Sasa, nadhani hata wataalam wetu yaani sijui kama tunawachanganya ama ndio somo linaleleweka, lakini mazingira yetu yako namna hiyo.

Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe na Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, ajiandae.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muda huu ili niweze kuchangia hoja hii muhimu ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, niungane na wenzangu kupongeza kazi nzuri inayofanyika na Wizara hii, Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake pamoja na Kamati kwa ujumla, bajeti iliyoletwa na mapendekezo yote ni mazuri kabisa, nawaponga sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu, jambo la kwanza, napenda nikumbushe nililizungumza hili wakati nilipochangia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Ile Mbuga ya Udzungwa asilimia 80 ipo Wilaya ya Kilolo na hilo Wizara inalifahamu. Jambo la kwanza, hakuna geti hata moja la kuingia Mbuga ya Udzungwa kwa Wilaya ya Kilolo ambako ndiko asilimia 80 ilipo. Zile ofisi za TANAPA zilizopo pale Udekwa, barabara yake hajajengwa na nilisema hapa kwamba, walianzia kule Udekwa kuja pale Mahenge kwenye barabara ya lami. Wakatengeneza kilomita 14 kwenda barabarani ikaishia porini bado kilomita saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba, Wizara hii na TANAPA kwa sababu, ofisi zao ziko pale Udekwa hatuwezi kushindwa kutengeneza zile kilomita saba ili tuingie kwenye zile ofisi zao na pia ili tuweze kulifika lile geti, kwa sababu, kwa sasa tunazunguka karibu kilomita 60 mahali ambapo tungetumia kilomita 20 kufika pale kwenye lile geti na ile barabara ya kilomita 60 yenye si nzuri. Kwa hiyo, napendekeza kwamba, kwa pamoja mimi niko tayari kushirikiana hata na wananchi, tutoboe ile barabara na yenye tutafute fedha kidogo tuweke greda tumwage kokoto, hatusemi lami lakini ifike kwenye lile geti, angalau tuwe na geti moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, Mbuga ya Udzungwa hiyo inayotumika ni asilimia 20 tu kwa sababu, kule kote kumebaki pori, asilimia 80 ya mbuga haitumiki, jambo ambalo ningependa tushirikiane ili tufungue na kama kuna haja ya kuongeza mageti mengine tuongeze, kwasababu, ile ni Mbuga kubwa na ina maeneo mengi, ambayo yangeweza kuwa na vivutio.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kwa unyenyekevu sana, naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wanisikilize kwa sababu hii ni changamoto ya kipekee. Katika Kata ya Kidabaga, Kata ya Masisiwe na kidogo Kata ya Ng'ang'ange kuna changamoto ya ngedere na wale ngedere wanatoka kwenye ule mpaka na ni wengi. Wale ngedere wanavuna mahindi kama ya kwao na kuna usemi

usemao ukicheka na ngedere au nyani utavuna mabua, wale watu kule sasa hivi wanashinda kule porini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilienda kwenye mikutano, watu wanafanya zamu, natakiwa niwe na mikutano miwili wa asubuhi ili wengine wahamie ngedere na wa mchana ili wengine waende warudi. Wale ngedere sio kivutio kwa sababu, kuna baadhi ya wawekezaji kule wanatoka hata Ulaya, lakini nao wanalamika. Ngedere wale wanakula wakimaliza wanakaa hata kwenye shule za msingi na wanafanya burudani zao nyingine siwezi kusema hapa. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kitolewe kibali wavunwe. Kama kuna mahali wanaliwa wakavunwe waliwe, kwa sababu, ni wengi na wanazaliana sana. Ni changamoto kubwa sana na ningependa itatuliwe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nyamoga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, ifike wakati sasa watu wa Maliasili waangalie, kama wenzetu hapa wachina hivi vitu vyote wanakula? Kwa nini bucha za ngedere, nyani na vitu vingine zisiwepo? Ili hao watu waje wanunue hizo nyama wapeleke huko? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Haya Mheshimiwa Getere ahsante sana, huo ni mchang'o sio taarifa. Mheshimiwa Nyamoga, kengele ilikuwa imeshagonga hapa, kwa hiyo dakika moja.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia suala la tembo pale Kata ya Nyanzwa pamoja na Kata ya Ruaha Mbonyuni. Kwa sasa kwa mwaka huu tu wamekufa watu 12, Kata ya Nyanzwa nane

na Ruaha Mbuyuni wawili, tayari wameshauawa. Huenda nao ni ushoroba, lakini kwa kweli ni changamoto kubwa na naomba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wakimaliza hapa, twende pale, wameweka askari pale wanalima vitunguu tu. Tena wakati tembo akiua mtu, wanataka wananchi wachange fedha. Sasa tembo ameshaua watu wakae vikao, wachange fedha wakakodi gari ndipo wakawachukue, ndipo waende wakawaue au wakawafukuze hao Tembo.

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, inachukua muda mrefu sana nawaombeni sana haya.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba Wizara wayafanyie kazi hayo. Hata hivyo, naunga mkono hoja, ikiwa hayo niliyosema yatazingatiwa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pallangyo na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, ajiandae.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii. Kabla sijaendelea, naomba nitoe pole nyingi sana kwa wananchi wa Jimbo la Hai, kwa kuondokewa na mama yetu mpendwa ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro, lakini ni mke wa Waziri Mstaafu baba yetu Msilo Swai.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pole hizo, niungane na wenzangu kupongeza sana uongozi wa Wizara hii. Bahati nzuri nilikwishesema mimi sio mwepesi sana wa kupongeza, ila napongeza kwa sababu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa namna ambavyo anasimamia Wizara hii na taasisi zake. Pia nimpongeze kwa sababu, yeye

anafikika na anasikia akiambiwa, ni Mawaziri wenyе sifa za pekee pamoja na huyu. Hata hivyo, nimpongeze Naibu Waziri kwa namna ambavyo na yeye pia ni mtu anayefikika, mama mwema kabisa huyu, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia watendaji wa taasisi wakiongozwa na Katibu Mkuu. Isipokuwa wale wa *TAWA* wao sitawapongeza kwa sababu, nina jambo nao. Vile vile nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri tulienda naye kwenye ziara kwenye Jimbo la Hai na tulitembelea eneo lile la Makoa kwenye Chama cha Ushirika. Nimshukuru sana kwa kusimamisha mkataba ule uliokuwa mbovu na leo sitaki kuzungumza jambo lile kwa sababu najua Waziri anaendelea na uchunguzi. Nimpongeze kwa hatua za awali kusimamisha mkataba ule ambaо ulikuwa hauna maslahi kwa wananchi wa Jimbo la Hai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pamoja na pongezi hizo sasa nishauri. Tumekuwa tukipokea mapato makubwa sana kwenye Serikali kuu kwenye vyanzo vinavyotokana na maeneo ya utalii. Hata hivyo, imekuwa bahati mbaya, wananchi wanaozunguka maeneo haya, hawanufaiki moja kwa moja pamoja na kwamba, tunapokea fedha kutoka Serikali Kuu. Hili linaongeza kutokuwa na upendo na maeneo yale. Ili wananchi hao wanaozunguka maeneo haya wawe na upendo na watanze vyanzo vyetu, lazima tuone namna ya kuwa-*motivate* na kuwafanya wawe na upendo na vivutio hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tuna Mlima Kilimanjaro pale, utashangaa sana wale wanaoenda kusaidia watalii wanaowapandisha mlima wanatoka nje ya maeneo yale. Lakini vile Vijiji vya Foo na vingine vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro, wale vijana hawapati kazi hizi. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri, mimi niko kwenye mchakato naandaa *database* ya vijana wanaozunguka vijiji vya Mlima Kilimanjaro, ambaо wana sifa za kupandisha watalii kwenye Mlima huu waweze kupata ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitakabidhi *database* hiyo ya vijana wa Hai, wako tayari, wana afya njema na wana sifa za kupanda Mlima Kilimanjaro. Wizara iwatumbu na ipeleke maelekezo maalum kwa makampuni yanayopanda Mlima Kilimanjaro, ili waweze kuwatumbu vijana hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kushauri, tuna mageti kadhaa yanapanda Mlima Kilimanjaro, lakini ukiyaangalia najua tumeaita kwenye kipindi cha mpito ambacho ugonjwa ya *Corona* umesababisha idadi ya watalii ishuke. Hata hivyo, najua mungu ni mwema atatusaidia na watalii wanaongezeka. Kwa sababu hiyo naomba sasa tuwe na geti lingine jipyaa ambalo litaanzia pale barabara ya kutoka Kwa Sadala, litapita pale Ng'uni, litapia Mula kwenye Kata ya Masama Mashariki na Masama Kati. Lengo ni nini, ni kupanua wigo wa utalii kuelekea Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifungua barabara hii kuna vivutio vingi vya tofauti na barabara ile ya Machame na barabara nyngine zilizoko kwenye wilaya nyngine. Kwa hiyo naomba sana hili pia walitazame. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kushauri, Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamesema. Utaratibu wa kutoa vibali kusafirisha nje ya nchi lazima tubadilishe mfumo huu, tumeshatoa vibali vingi ndege wetu, wanyama wetu wanapelekwa nje ya nchi. Swali la kujuliza hapa, hawa wanyama wanakwenda huko nje ya nchi tuna-control vipi kuzaliana kwao. Nataka niwaambie kuna siku hapa tutakosa watalii kwa sababu wanyama hao wakienda kule wanazaliana wanaongezeka na bahati nzuri wenzi hawa wanateknolojia ya kutushinda sisi. Watakwenda kutunza hawa wanyama watatengeza *zoo* kubwa kubwa, mwisho wa siku huku nchini tutakosa watalii wakuja kututembelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kawaida, wewe mwenyewe huko hapa ukiona kwamba leo tutakushangaa eti unatoka hapa Tanzania kwenda

kushangaa au kutembelea Zoo ya Simba nje ya nchi. Ndivyo itakavyokuwa simba watakuwa wengi, vyura watakuwa wengi, ndege watakuwa wengi na mamba watakuwa wengi kule kwao, huku hawatakuja. Kwa hiyo niombe sasa imetosha, vibali tulivyowapa vimetosha. Hili ni sambamba pia na wanyama wanaokuja kuletwa huku kwetu, iwe ni kuja kutunzwa au vinginevyo. Najua kwenye hili kuna shughuli inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vibali vya kuruhusu wanyama kutoka nje ya nchi kuja huku kwetu tutazame. Tusije tukaletewa wanyama wa kuja kuharibu wanyama wetu. Tunafahamu hapa Tanzania sisi ndio tunaongoza kwa idadi kubwa ya simba lakini tunaletewa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kengele ya kwanza?

NAIBU SPIKA: Ni kengele moja tu.

MBUNGE FULANI: Endelea.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niunge mkono hoja. Nashukuru sana sasa, lakini nimalizie kwa kuomba Wizara hii ishirikiane na wizara nyingine...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ng'azi Ulenga* ajiandae.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie kwa ufupi hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Nianze moja kwa moja kwa kutoa pongezi zangu kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara. Kusema kweli Waziri, Mheshimiwa Dkt.

Damas Ndumbaro; Naibu wake, Mheshimiwa Mary Masanja; Katibu Mkuu, Dkt. Allan Kijazi; Wakuu wa Taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Mnyonge mnyongeni lakini haki yake apewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na salam zangu za pongezi, nzungumzie tatizo la mipaka. Wabunge wenzangu wameshazungumzia jambo hili kwa kirefu na kwa undani zaidi, lakini nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba kule kwenye Jimbo langu Arumeru Mashariki kuna tatizo la mpaka kati ya Arusha *National Park* na Kitongoji cha Omela. Arusha *National Park* walichukua ekari takriban 960 mwaka 2017 na baadaye wakarudisha ekari 360. Baada ya kuchukua lile shamba waliwaacha wananchi wakiteseka hawana mahali pa kufanyia kilimo ambacho ndio ajira kubwa kwa wananchi wetu wa Tanzania. Kwa maana hiyo waliwaacha wananchi wakiwa maskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara kupitia Waziri, watumie busara kidogo waangalie ekari zilizobaki ekari 640 sio tatizo kubwa kwa Taifa hili na sio tatizo kwa hifadhi. Wapime faida ambayo hifadhi inapata na hasara ambazo wananchi wameingia katika kunyang'anywa yale mashamba. Ikiwezekana zile ekari zirudishwe kwa wananchi waweze kuendelea na maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kidogo kuhusu Sekta ya Nyuki. Taifa hili tangu tumeypata Uhuru, tumesomesha wataalam wengi sana kwenye sekta ya nyuki na kama tungetumia sekta hii vizuri, mazao ambayo yanatokana na nyuki yana uwezo wa kuingizia Taifa hili fedha nyingi tu hasa fedha za kigeni. Hata ile sumu ya nyuki ina soko sana nje ya nchi. Rai yangu kwa Wizara, iongeze nguvu kwenye sekta ya nyuki iweke kipaumbele ili hatimaye sekta hii nayo iweze kuchangia kwenye pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, wenzangu walizungumza kuhusu kuwekeza kwenye *cable cars*; ni kweli kabisa kwamba sisi Tanzania utalii tunaofanya kwenye milima

ni utalii wa kupandisha watalii milimani kwa miguu. Tukubaliane kwamba kupanda mlima ni zoezi na jinsi watu wanavyozidi kuzeeka mazoezi yanakuwa ni tabu kidogo kuyafanya, huwezi kupanda mlima baada ya kufikisha miaka 80. Kwa hiyo, niseme kwamba Wizara iangalie, ifungue mlango kwa wawekezaji waweze kujenga miundombinu ya *cable cars* kwenye milima yetu hususan Mlima Kilimanjaro, Mlima Meru na kule Kitulo ambako mwenzangu, ndugu yangu Mheshimiwa Festo Sanga alisema kwamba miundombinu hiyo ikijengwa itaweza kutuingizia fedha nydingi sana za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kutembelea nchi fulani, South Africa *Cable mountains* ni ngumu sana kupanda, lakini nilishuhudia jinsi ambavyo *cable cars* ambayo imejengwa pale inavyoingiza fedha nydingi kwa nchi ile. Nina uhakika kabisa kabisa kwamba...

MHE. CONSTANTINE J KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka kumpa taarifa Mheshimiwa anayechangia kwamba Nchi ya Thailand inapata watalii milioni 16, lakini asilimia zaidi ya 80 ya watu wanaokwenda Thailand wanakwenda kwenye *cable car*na hawana milima mirefu kama Mlima Kilimanjaro. Wana milima ya kawaida tu ambayo wameunganisha na *cable car* lakini ndiyo inayopeleka watalii wengi ambaa ndio wanakwenda kutembea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pallangyo unapokea taarifa hiyo.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono 70. Ni kweli kwamba *cable cars* zina-supplement sana *income* kutokana na *tourism*. Ukiangalia fedha zinazoingia pale *cable mountains* utasema ni kwa nini hatufanyi hivyo na sisi. Niseme kwamba

ninavyozungumza sasa hivi kuna ndugu yangu yupo Marekani alinidokeza kwamba ikiwezekana nirushe hiyo karata mezani kwako ili Wizara illichukue halafu tuangalie namna gani tunaweza tukakaribisha wawekezaji waweze kuja kushirikiana na Taifa hili kujenga ile miundombinu kwa sababu pia nayo ile ni gharama, lakini ni njia mojawapo ambayo ingeweza kusaidia kutengeneza fedha nydingi sana za kigeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, nakushukuru kwa muda ulionipa na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kuna wageni watatu hapa niwatangaze. Pengine huenda wanataka kutoka. Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Mary F. Masanja, ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni wadau Utalii kutoka Mkoaa wa Mwanza. Hawa ni Ndugu Senator Mselya, Ndugu Kasanzu Apolinaly na Ndugu Badia Mwashambwa. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'azi Ulenge na Mheshimiwa Asia Mwadini Mohammed ajiandae.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti yao. Nianze kwa kuwaomba sana Wizara waanze kuyafanya kazi mambo ambayo yalifanyiwa mjadala kati yao na Washika Dau kwa maana ya Wafanyakazi wa Utalii, lakini na mawasilisho ya Vyama vya Wafanyakazi wanaojihuisha kwenye biashara hii ya utalii kama ma-guide, ma-porter na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na maslahi ya wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye utalii, ma-porter, ma-guide na wapishi. Kundi hili ni kundi kubwa la vijana lilioljajiri kwenye kazi ngumu hii ya utalii, lakini hawana mikataba wengi wao, lakini pia hawana bima za afya, wanakwenda

kule kwenye baridi sana. Ningiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuandaa hata mfumo wa kuwa na pensheni kwa watu ambao hawako kwenye sekta rasmi, lakini wanaopata kipato kama hawa ambao wanajihuisha na biashara ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia hao watu wanahitaji elimu kubwa, kwa *nature* ya biashara ya utalii, mfanyakibashara yule akishawapokea wageni huwa mara nyingi wanakabidhiwa kwa hawa waongoza utalii. Sio wote wana utashi wa kutosha, naomba sana Wizara iangalie uwezekano wa kuwapa elimu ya mara kwa mara na semina za mara kwa mara hasa kuhusu mambo muhimu ya nchi yetu ikiwa na takwimu, kwa sababu hawa ni mabalozi muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kilio cha muda mrefu sana kuhusiana na ada zetu kwenye mbuga zetu na maeneo yetu ya utalii pamoja na viwanja vyetu vya ndege. Kama kichocheo muhimu cha utalii naomba Wizara ifanye utafiti wa kutosha kulinganisha bei hizi pamoja na maeneo mengine ili kuweza kufanya maamuzi sahihi. Kama ilivyo kwenye halmashauri zilizopo kule Geita zinapata *CSR* kutoka kwenye machimbo yale, katika Mkoa wa Kilimanjaro halmashauri zinazozunguka kwa mfano Mlima Kilimanjaro, tungependa sana na sisi tuwe tunapata kipato fulani kwa ajili ya kusaidia halmashauri zile ambazo zinazunguka mlima ule na ambazo zinafanya kazi kubwa ya kulinda mazingira maeneo yale. Nimeona wenzetu wa Geita wanapata kipato kizuri sana, lakini kwetu naona suala hilo halipo. Tunaomba sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba suala hili liliwasilishwa na wafanyakibashara suala la sera hasa kwenye suala la kodi, naomba Serikali ifanyie kazi hasa kwenye eneo la kukata rufaa hasa wafanyakibashara wanapokuwa wana matatizo kwenye kodi. Katika sheria ile kuna kifungu cha 16 ambacho kinapingana kabisa ambacho kinasema ukikata rufaa kwa Kamishna lazima iwe suala linalohusu *Civil Concern*. Sasa kipengele hiki kinapingana

kabisa na kipengere kifungu cha 7 na kifungu cha 53 ambacho kinatoa haki ya rufaa. Wafanyabiashara waliwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri, naomba nilitilie msisitizo ili basi marekebisho yaweze kufanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii imepigwa sana kipindi hiki cha *Corona*, lakini imetupa mafunzo mawili. Funzo la kwanza ni kuweza kuweka *record* zetu sawa ili baadaye tuweze kutoa *stimulus* ikiwezekana na *stimulus* siyo lazima iwe kwa kutoa fedha hata kwa kuwapunguzia gharama kwa kipindi ambacho kitakuja cha utalii. Hata kuhuisha leseni zao kwa sababu walikata leseni kipindi ambacho hawakufanya biashara. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba sana hilo liweze kuzingatiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuangalia masoko mapya, kipindi cha *Corona* tumeweza kupata soko jipya la Urusi, lakini kikwazo kikubwa kimekuwa ni lugha, wenzangu wameshataja. Ni vizuri tuanze kuchunguza masoko mapya na tuhakikishe tunafanya kazi ya kujua lugha hizo za Kichina, Kirusi na za maeneo mengine ili tuweze kupata masoko hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *helicopter* ya Uokozi, *Rescue helicopter*. Pale Kilimanjaro ilikuwa inafanyika na mfanyabiashara binafsi. Ilikuwa ina tija sana na ni chanzo cha mapato, lakini kutokana na hali hii ya *COVID*yule bwana ameshindwa kujidoresha. Ni vizuri Wizara iangalie chanzo hiki cha mapato, iweze kununua *helicopterya* uokozi ambayo itakuwa inalipiwa kwa wale ambao wanakwenda kupanda mlima ili mtu akipata tatizo basi huduma ile ambayo imeshazoeleka, imeshatangazwa iweze kuwepo na ni chanzo cha mapato kwa ndugu zetu wa Wizara ya Utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi kabisa naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'azi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia

Mwadini Mohammed na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde ajiandae.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote niwashukuru Mawaziri na niwapongeze sana kwa *collabo* nzuri ya kupiga kazi, hakika inatupendeza sana. Tunaona kabisa kwamba mafanikio makubwa yanakwenda kupatikana kwa kuunganika kwenu na kufanya kazi pamoja kwa bidi. Ni mfano mzuri tuwaige Mawaziri hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwenye Wizara hii ambayo inachangia kwa kiwango kikubwa kwenye GDPya Taifa letu. Mkoa wa Tanga nasi tumebarikiwa kuwa na Hifadhi ya Saadan kwa kilomita zaidi ya 1,062. Hii Hifadhi ya Saadan ni hifadhi ya kipekee kabisa Afrika Mashariki kwa kuingilliana na Bahari ya Hindi. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uoto huu wa asili, lakini lazima tukiri kuna changamoto ambazo zinatukabili ku-*enjoy* zawadi hii ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Wilayani Pangani kuna vijiji ambavyo vinataabika mno kwa kutokuweza kuwa-*control*/wanyama waliopo ndani ya Hifadhi ya Saadan. Kwa mfano, Kijiji cha Buyuni kiko ndani ya Hifadhi ya Saadan, pia Kijiji cha Mikocheni, Sange, Mkalamo, Bulizaga hivi vyote vinaathirika mno kwa tembo wengi sana ndani ya hifadhi ile. Vijihi hivi vimeduwa viñasua sua katika kilimo kwa sababu ya kuwepo kwa tembo wengi sana, lakini hata miundombinu ya barabara ambazo barabara zetu ni za *gravel*/zinapata shida mno kwa sababu ya uwepo wa tembo wengi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Mhifadhi Mkuu anakiri wazi kwamba tembo hawa ni wengi wananihindu nguvu. Nahofia kumwambia kaka yangu wa Songea tuongozane wote, lakini natamani kabisa Mawaziri hawa watoke pamoja tuone namna gani tunakwenda Pangani tushirikiane na watendaji wa Pangani kuweza ku-*control* hali ile. Tembo wanaingia kwenye mashamba kuanzia saa 12.00 jioni na

wanatoka saa 1.00 asubuhi na ni hatari kwa watoto wetu wakati ambapo wanakwenda mashulenii. Tunaomba sana sana tuunganike kwa pamoja tukatatue changamoto zilizopo Wilayani Pangani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pia kule Handeni, vijiji viwili na wananchi wawili walishawahii kuuawa kwa ajili ya tembo. Tuone namna nzuri ya kupambana kwa pamoja kwenda kuziondoa changamoto hizi, ni muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali kupitia Wizara hii ya Maliasili na Utalii iliwahi kutoa zuio kwa kusafirisha viumbe hai kwenda nchi za nje. Miongoni mwa viumbe hai vilivyoziuliwa ni pamoja na vipepeo wanaozalishwa na watu binafsi katika Wilaya ya Muheza, Mkoani Tanga. Kwa kuwa basi, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, alitoa wito kwa Watanzania tufuge wanyama mbalimbali na viumbe hai kwa ajili ya kujiongeza kiuchumi. Je, Wizara hawaoni kuendelea kuliweka zuio linaendelea kuadumaza wananchi waliokuwa wakifuga vipepeo hao kiuchumi? Ionekane haja sasa kwenda kuliondoa zuio hili ili wananchi waweze ku-enjoy kufanya biashara ile ya kusafirisha viumbe hai kuvipeleka nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza basi mapato ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii, nasi tujaribu kujikita kuzifanya hizi *routes* zetu za ndege zinapopita nazo zi-move zifanye *maneuvering around* a Mlima Kilinjaro. Naziona juhudi za Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kuutangaza Mlima Kilimanjaro kwamba upo Nchini Tanzania, lakini wenzetu hiyo ndiyo *technic* wanayoituma. Niliwahi kumpa mtu zawadi ya kahawa ya Kilimanjaro, nikamwambia kawaha hii inatoka Tanzania ananikalia inatoka ananiambia inatoka Kenya. Nikamwambia tu-google hapa, tulivyo googlendio akakubali kwamba kama Kilimanjaro ipo Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aliniambia, nilipoingia Nairobi, nilipitishwa maeneo yale nikauona Mlima wa

Kilimanjaro kwa mbali kwa hiyo sisi tunashindwaje ku-coordinate na ATCL kuhakikisha kwamba ndege zetu nazo zinafanya *maneuvering around area* ya Mlima Kilimanjaro ili tuweze kuwavuta watalii zaidi nchini kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuone haja basi ya kutengeneza *festivals* ambazo kila mwaka zitakuwa zinafanyika au kwa *season* maalum na zitangazwe *all over the world* kuhakikisha watalii zaidi wanakuja nchini kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asya Mwadini Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati ajiandae.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii muhimu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba Utalii ni Sekta muhimu sana katika uchumi wa Tanzania lakini sekta hii inachangia Pato la Taifa asilimia 17. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Bodi ya Utalii Tanzania, Tanzania inatembelewa na wageni wapato milioni moja kwa mwaka. Pia, Bodi hiyo ya Utalii imesema kwamba hao wageni milioni moja asilimia 60 ni wageni kutoka nje ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linanisikitisha sana ukizingatia kwamba tunawategemea sana wageni kutoka nje ya nchi kuliko sisi ambao tupo ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, faida inayopatikana kwa utalii wa ndani, kuna nchi kwa mfano Brazil wao wana wageni wa ndani ya nchi

wanaotembelea katika vivutio vyao ni asilimia 68. Wanategemea asilimia 32 tu, wageni kutoka Mataifa mbalimbali kwa ajili ya kwenda Brazil. Hii inaonesha kwamba unapokuwa umejipanga vizuri katika utalii wa ndani huwezi kutegemea sana ule utalii wa nje. Hilo la kwanza. La pili, pato lile unakuwa na uhakika nalo kwa sababu liko ndani ya nchi. Kwa hiyo, haliwezi kutoka nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, naishauri sana Serikali kwanza kabisa masoko yetu yajikite zaidi kufahamisha Watanzania; kwanza kuhusiana na masuala mazima ya utalii. Pili, hata hawa wanafunzi wetu shulenii tungewatengenezea mtaala au vitabu wakaanza kukua na utamaduni wa kufanya utalii ili iweze kusababisha, maana wanavyokuwa wakubwa wanajua utalii ni suala muhimu na linaweza kuwaletaa tija wao wenyewe binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiwategemee sana wageni kutoka nje ya nchi kuja kututembelea. Kwa mfano, tumeona mwaka jana 2019/2020 kulivyokuwa na janga kubwa la *corona*. Kwa hiyo, utalii uliteteraka. Tuna watoto wetu na ndugu zetu walikosa kazi wengi sana wakaendelea kukaa nyumbani. Kama tungekuwa tumeimarisha vizuri Sekta ya Utalii hapa kwetu hivyo wale watu wangeendelea kufanya kazi na masuala mengine yangeendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba niende kwenye kipengele kidogo tu, labda niseme, nimeipitia Sera ya Utalii ya Tanzania inanisikitisha sana. Tunavyosema tunahitaji kupiga hatua kwenye utalii lakini sera yetu bado ni ya mwaka 1999. Kwa hiyo, sera hii haikidhi mahitaji ya utalii wa sasa ambao tuko nao. Kwa hiyo, tunahitaji kwanza tuboreshe sera yetu pamoja na sheria za utalii ili tuweze kuinua utalii wetu na pia waweze kuingiza Pato letu la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye utalii wa ndani tusiwategemee sana japo tunapiga kelele Wabunge humu, ofisi mbalimbali, lakini, kwa nini hata hawa Wabunge ukiwaliza humu ndani wangapi wameweza kutembelea vivutio vyetu itakuwa ni mtihani kwa kweli. Wengine

wanaweza kukuambia wamefanikiwa tu kwenda kwenye Kamati ndiyo wameweza kuona tembo na chui. Sasa hili haliletii tija, maana tunapokaa tunapiga kelele hailetii tija, tuoneshe mfano sisi wenyewe viongozi kwanza. Twende kwenye vivutio, tuwape *support* Wizara ili na hawa watoto wetu tukiwachukua, watoto wakienda kwenye vivutio, unajua watoto wana *story*, wakirudi shulenii wanahadithia watoto wenzao. Kwa hiyo, watoto nao wanaenda kuhadithia wazazi. Kwa hiyo, tunakuwa na jopo kubwa la mwingilio wa utalii wa ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie kwenye masuala mazima ya vivutio vya utalii. Mwanzo nilisema kwamba tunategemea sana wageni wapato milioni moja. *Average* inaonesha kutokana na vivutio ambavyo tunavyo, hawa wageni bado ni kidogo sana. Ni kidogo kwa sababu vivutio vyetu ni vingi, maana yake vivutio vimewakumbatia wageni kwa hiyo, maana yake vinabaki vinahitaji watu. Kwa hiyo, niishauri Serikali kwenye suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, tuweze kuwapa wawekezaji vivutio vingine ambavyo hatuviwezi. Suala la pili, nakumbuka nilichangia kwenye uvuvi, nilizungumza sana *issue* ya *marine park* na nikaomba Wizara ya Uvuvi hili suala la *marine conservation* wawapelekee Idara ya Utalii, kwa sababu ukipitia takwimu inaonekana wageni kuanzia 45,000 kwenda 70,000, wageni hawa wanavyokuja Tanzania wanafanya *diving*. Wanaenda kuangalia matumbawe na masuala mengine kwenye bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia kwenye mitandao wageni amba wanatoka *Scandinavia* yaani kule kwetu Zanzibar wanavyokuja lazima wakifika waombe kwenda kuangalia *coral reef* na vitu vingine.

Kwa kuwa watu wa utalii ni wataalam zaidi kwenye masuala ya uhifadhi, niishauri Serikali hii Idara ya *Marine Park* iende moja kwa moja kwenye Wizara ya Utalii na tutaweza kupata pato kubwa zaidi kuititia hii *tour* moja tu, sikuwambii hiso zingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende pia zaidi kwenye masuala mazima ya kumshirikisha mwanamke katika utalii wa Tanzania. Tunaona kwamba tunazungumza utalii, nimepitia hotuba na vitu vingine vingi lakini hatuoni mwanamke anatajwa kama ana sehemu kwenye utalii na anafaidika vipi. Namzungumzia zaidi mwanamke ambaye yuko chini *grassroot* ambaye amepakana na *border*, hifadhi, yuko kwenye maziwa, yuko chini ya fukwe na yuko katika sehemu pengine nyngi za utalii. Kwa hiyo, mwanamke huyu utaona kwamba yeye yupo amepakana na hifadhi au amepakana na msitu lakini wanaofaidika ni watu labda wanaotokea mkoa mwingine kwa sababu analeta wageni. Yeye yuko pale tu na ule msitu, atafaidika labda kupata hewa safi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niishauri Serikali kwamba; kwanza, tuweze kutengeneza mkakati maalum kuweza kuwasaidia wanawake hawa kupitia miradi mbalimbali midogo midogo ambayo itaweza kuwainua akinamama. Kwa mfano, tuna utalii tunaita *culture tourism*. Huu utalii, mgeni anaweza akaja mimi mwenyewe binafsi napenda pia kujifunza. Niliwahi kwenda Kagera lakini nilifika nilitumia masaa matatu kuangalia Wanabukoba wanapika chakula chao cha ndizi kwa mtazamo upi. Kwa hiyo, huu ni utalii. Tuwape nafasi akinamama waweze kile kidogo ambacho wako nacho kule majumbani wanafua, wanapika, wanatwanga, lakini mgeni ana-*appreciate* sana na anajifunza vitu vingi zaidi pale kwa kuona. Kwa hivyo, akinamama watapata pato, lakini vile vile na Serikali nayo itaongeza uchumi. Tusuache utalii wa utamaduni, ni utalii ambao unaleta pato kubwa ndani ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukienda India, Wahindi hawakubali ukifanya utalii usipite katika *street* zao, usipite kwenye vichochoro vyao ili ujifunze bajia na kachori zinatengenezwa vipi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee zaidi nilizungumza suala zima la masoko na tunahitaji bado masoko yetu yako chini kwenye suala zima la utalii na tunahitaji zaidi Serikali kupitia Idara ya Utalii waweze kutengeneza

mechanism ambayo iko strong itakayo-deal na marketing on tourism only ili tuweze kupata pato lakini na kuleta wageni. Narudia tena, tusitegemee zaidi wageni kutoka nje ya nchi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nishauri labda kwa sababu tunatumia *TV*, magazeti, vipeperushi lakini kuna mitandao. Sasa hivi, dunia iko kwenye mkono, kuna hawa akina Ayo na wengineo, kwa nini tusingetengeneza vitu kama hivi mtu akiingia tu anapofungua simu yake akiingia kwenye mtandao anakutana na kitu kwamba *Visit Tanzania*, kuna *one, two, three, four* ili weze ku-motivate na nilishazungumza kwamba tutaenda kuwahamasisha watoto wa shule, vyuo vikuu, maana hapa tunakuja Bungeni tunawaleta watoto wa shule, tunawaleta watu kutoka vyuo vikuu, wanahamasika. Kwa hiyo na hiyo itatumika zaidi ili kuweza kukuza utalii wetu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa nisisahau, ni suala zima la uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa pamoja. Kwenye mazingira hasa masuala ya takataka na mambo mengine tumeukaribisha utalii Tanzania, kwa hiyo, Serikali nayo inapaswa kuanza kufahamu kwamba tayari tunavyoleta wageni nje ya nchi wanakuja na vifungashio vyao tofauti, wanakuja na *material* yao tofauti ambayo sisi kama utamaduni wetu yalikuwa hayapo.

Kwa hiyo, hatuna budi kwanza pia ku-focus na kwenye masuala mazima ya uhifadhi wa mazingira ili takataka ambazo zipo zinazalishwa kwenye upande wa utalii zisiwe zinachomwa, zisiwe zinapelekwa baharini na zisiwe zinafanyiwa mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tujifunze pia masuala mazima ya *recycling*, tutumie akinamama, tutumie vijana wetu ambao hawana kazi, wajifunze kwenye utengenezaji wa mbolea na masuala mazima mengi kwa ajili ya kukuza uchumi wetu, lakini na kutengeneza *step* ya kutoka hapa tulipo na twende kwenye hatua ambayo tunataka utalii ukue. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati na Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga ajandae.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kunipa muda huu mfupi ili nichangie katika hii Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza, wametoa pongezi zao nyngi sana kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na mimi bila kupoteza muda nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa kweli mimi nawakaribisha Jimboni kwangu ili tuweze kutembelea vivutio vipyta vya utalii. Kama Waziri hatakuwa na nafasi basi naweza kwenda na Naibu Waziri na kwa sababu kule barabara ni mbovu, wakati mwengine tunaweza tukalala huko huko kutohana na ubovu wa barabara. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara zitachukua ushauri japo nusu tu wa Waheshimiwa Wabunge, zitakuja na kitu kizuri sana. Wabunge wameshauri kwa ufasaha na kwa ufundi mkubwa sana. Wasiwasi wangu tusije kuwa tunatwanga maji kwenye kinu, wanayachukua hapa lakini hawaendi kuyafanya kazi. Hebu tujifunze kufanya kazi ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye vivutio vipyta, tuna tatizo la kugundua na kuvivumbua vivutio vipyta vya utalii. Hapa Dodoma Mjini, katikati ya Tanzania wameweka pale Jiwe na wameweka alama pale, hakuna shughuli zozote za utalii zinaendelea pale. Pale tungeweza kujenga hoteli, tungeweza kupika vyakula vya makabila yote ya Tanzania. Mtu akitembea hapa anaenda anatalii katikati ya nchi ya Tanzania, lakini hatuvumbui! Ukipikia jina la Dodoma kuna mahali tembo alizama hapa karibu na St. John, ndiyo Mgogo akasema *tembo idodomela*, ndiyo ikaanza Dodoma, Mzungu

akashindwa kutamka. Hakuna shughuli zozote zinafanyika pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda katika Jimbo la Kibakwe, hapo Pwaga, kuna ndege amba dunia nzima hawapo wako kwa Mheshimiwa Simbachawene, tena Mheshimiwa Simbachawene ni rafiki mkubwa wa Waziri lakini hajawahi kumkaribisha akaangalie. Kwa hiyo, ningeshauri tuendelee kuvumbua vivutio vipyta vya utalii. Tunajenga uwanja mkubwa wa ndege hapa Msalato. Hivi mtalii atashuka Msalato, aende Iringa kilometa 274 halafu ndiyo aende kuzitafuta tena kilometa 160 na kitu wakati tuna barabara katika hapa ambayo ni njia fupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa barabara hii ukitoka hapa unaenda Mpunguzi, ukitoka Mpunguzi unaenda Mwitikila, ukitoka Mwitikila unaenda Nagulo, ukitoka Nagulo unaenda Uzi, ukitoka Uzi unaenda Manda, unavuka mto Kizigo tayari umeshaingia Ruaha *National Park* kwa kilometa 125 tu. Badala ya kutembea kilometa 300, ukikatiza hii njia ya katika unafika kwenye maeneo ya utalii kwa urahisi Zaidi, tuimarishe. Kwa hiyo, sio lazima watalii wazunguke mbali, kilometa nyingi wanaenda kutafuta wanyama wakati ukikatiza hapa katikati unafika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna vivutio vingi sana. Ukija kwenye jimbo langu mimi kuna mapango yako hapo Kata ya Ilolo. Ukitembea hapo unaenda unakuta mapango mazuri, watu huwa wanaenda pale wakati mwingine wanaomba na mvua inanyesha hapo hapo, hata kama jua ni kali. Kuna jiwe moja kubwa sana liko Mloda pale, nawakaribisha Wizara waende wakaangalie, kuna vivutio vingi, vingi vingi, vinaweza kutusaidia nchi hii kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja nataka nishauri hapa. Suala sio kwamba wanyamapori wameongezeka kuvamia mashamba yetu, hapana. Sisi tunachoshauri kingine ni ucharaka wa kuwafukuza. Mnyama anaingia, anashinda humo analala mpaka siku tatu. Hivi,

tunasema eti oh! Hakuna silaha, hakuna watu, hawawahi mbona Bunge linawahi hapa Tanzania? Bunge halijawahi kuchelewa, saa tatu kamili limeanza. Mbona Bunge halichelewi? Kwa hiyo, Taasisi kubwa kama hii lazima tuipongeze, hakuna siku Bunge limechelewa hata dakika moja. Bunge ni saa tatu kamili kila siku na saa tatu kamili Bunge liko hewani. Mbona sisi tunawahi? Taasisi zingine za Serikali zinashindwa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewafundisha vijana ulinzi shirikishi. Hivi kwa nini wale vijana tuliofundisha ulinzi shirikishi kwenye kila kijiji kama pale Handali wapo vijana wazuri sana. Manda kuna vijana wazuri sana. Ukienda Chiluhuru kuna vijana wazuri sana wamefundishwa na nyie. Kwa nini wale vijana wasipewe silaha ili wawafukuze wanyama wakifika? Wanawaaminije kuingia mpaka hadi kwenye hifadhi wawafukuze majangili lakini hawawaamini kwenye kulinda mali zao? Kila Kijiji kingeweza kununua silaha, sio kusema kwamba wanaua wanyama, wazitumie kufukuza wanyama kwa sababu wamewaelimisha wao na Askari walio nao ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wale ambao tumeshawafundisha, tuwafundishe vile vile kujilinda kwa sababu kujilinda ni haki ya mtu. Mbona jambazi akiingia ndani mtu anamuua jamani na wala hashtakiwi na mtu yejote? Sasa tembo anaingiaje kwenye shamba la mtu anakula, anamaliza, anakula anamaliza tunakuja hapa tunajadili habari ya kifuta machozi, kifuta jasho, wakati tungenesema vijiji vyote vinavyopakana na wanyamapori na ambavyo vimesajiliwa, kila kijiji kimiliki silaha kwa ajili ya kufukuza wanyama hatari wanapoingia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo ajiandae.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii hoja muhimu. Kwanza nianze na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Mr. Kijazi na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya na kutuletea bajeti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mradi wa *REGROW*. Mradi huu ni mradi wa kukuza utalii Kusini. Huu mradi kwa kweli, umeanza mwaka 2018 na tunategemea mwaka 2023 utakuwa umekamilika, lakini naona kama kasi ya mradi huu ni ndogo sana. Kwa sababu, huu mradi tunategemea sasa Nyanda za Juu Kusini tuna vivutio vingi, Wabunge wengi sana wa Nyanda za Juu Kusini wameongea vivutio vyao vilivyopo katika mikoa yao. Hata hivyo, kama huu mradu utakuwa haujakamilika bado tutakuwa hatujawasaidia wananchi wa Nyanda za Juu Kusini kupitia Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea kwamba huu mradi ungeleta ajira nyingi za vijana, akinamama na watu wote na ungeorgeza pato kubwa sana, lakini hatuelewi kama mwaka 2023, huu mradi utakuwa umeshakamilika au umeshaanza kufanya kazi yake. Kwa sababu Makao Makuu ya huu mradi yanategemea kuwepo Iringa lakini pia *GNndiyo* kwanza juzi tu tumeona imesainiwa na yenyele ilichukua muda mrefu sana kusainiwa. Pia bado hatujaona hata Makao Makuu yenyele yameshaanza kujengwa na tunategemea sasa kutakuwa na vyuo vingi pale Iringa kwa ajili ya Nyanda za Juu Kusini, Vyuo vya Misitu, Maliasili na kila kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali ilichukue suala hili kwa umuhimu wake ili kuhakikisha kwamba huu mradi unakamilika na unaleta manufaa. Ikiwezekana labda kuwepo na mashindano kati ya Nyanda za Juu Kusini na Kaskazini, pengine labda hata watendaji wangechamka kuona kwamba haya mashindano yanaleta manufaa na pengine tungkuwa tunawapatia zawadi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vivutio bado havijatangazika kiasi cha kutosha. Bado tunaweza tukawa na utalii wa ndani kama vivutio vyetu itakuwa watu wanavielewa na nafikiri Wabunge wengi sana wamezungumzia kwamba utalii wa ndani pia unaweza ukalipa, unaweza ukasaidia pia hata mafunzo kwa watoto wetu, wakue wakijua kwamba tuna utalii katika nchi yetu. Hiyo inaweza ikamjenga kwamba sisi tuna maliasili ambazo zinaweza zikatusaidia wananchi wote. Kwa hiyo, niombe kwa kweli matangazo yaongezeke, biashara ni matangazo. Matangazo yakiwa mengi, vivutio vyetu vitaeleweka na wananchi watakwenda hata kuviangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nielezee kuhusu Ruaha *National Park*. Kwa kweli, hii mbuga ni ya pili kwa ukubwa na niliona hata Mwenyekiti wa Kamati aliizungumzia kwamba hii mbuga imesahauilka wakati ina wanyama wazuri, ina wanyama wengi, barabara haifiki kabisa. Maana hii ingesaaidia hata utalii wa ndani kama barabara ingekuwa inafikika. Hata sisi wenyewe Wabunge, nishukuru kwamba Kamati ilikwenda kutembelea na imeona changamoto nydingi sana zilizopo katika Ruaha *National Park*. Kwa hiyo, niombe kwa kweli ile barabara Waziri wa Ujenzi na Mawaziri wote wapiganie, watoe kipaumbele kwa hii barabara kwa sababu ni barabara ambayo itasaidia kabisa kukuza utalii katika nchi yetu na kuleta pato kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie kuhusiana na utalii ulioko Iringa Manispaa. Kuna sehemu ambapo wakoloni walikuwa wananyongea watu, panaitwa kitanzini. Pale kuna kitanzi ambacho kuna boma lake limebomoka kabisa, yaani watalii wanatakiwa waje watembelee. Nitamwomba hata Mheshimiwa Naibu Waziri Masanja twende sio mbali sana, akaone jinsi ilivyo. Pamesahaulika kabisa wakati ni utalii mzuri. Kuna jiwe lile Gangilonga, lilikuwa linaongea zamani, hata watalii wakienda...kutembelea pale wanapata madhara wanavamiwa. Kwa hiyo, ni vizuri hivi vivutio vingewekewa mkakati kwanza viwe vinafikika na viwe vinatangazika, lakini tatizo kubwa kwenye halmashauri zetu

hakuna Maafisa Utalii. Kwa hiyo, unakuta kwamba, kuna Maafisa Kilimo, kuna afisa nani, lakini Afisa Utalii bado Wizara hajjawapa kipaumbele, hakuna *connection* kabisa, unaona wanajifanyia tu kazi wenyewe, hawana vifaa, hawafanyi kitu chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ingewezekana pengine labda Wizara itoe ruzuku kwenye halmashauri, ili hivi vivutio viweze kufikika na viweze kutangazika vizuri ili tuweze kuongeza pato kubwa sana katika halmashauri au kuwepo na kurugenzi inayosughulikia mambo ya utalii tu katika manispaa zetu kwa sababu ndiko kwenye utalii mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie pia kuhusu mazao ya misitu. Tunayo mazao ya misitu Mufindi, Kilolo na kwagine kwangi Njombe, lakini tunaona tozo zimekuwa nyingi sana, karibu tozo 13 kwenye mazao ya misitu. Wananchi wengi wengine wamepanda haya mazao ili yawasaidie kusomesha watoto, yawasaidie kama ajira pia, lakini tozo zikiwa nyingi bado tunaona hatujamsaidia Mtanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nikushukuru, lakini niombe kwamba, matangazo, Simba niwapongeze kwamba, wametangaza nchi kwa kutumia jezi zao...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Haya, kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nicodemas Haji Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo na Mheshimiwa Deus Clement Sangu ajiandae.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi wakati huu ya kuweza kuchangia Sekta hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwanza siku ya leo kuniamsha nikiwa salama na Mungu akipenda nategemea kutinga pale Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Uwanja wetu wa Jamhuri pale, ili twende tukaweze kuchuana na hawa TBC. Niwaombe Wabunge wahudhurie, ili waweze kushabikia timu yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, naomba kaka yangu Mheshimiwa Damas Ndumbaro pamoja na dada yangu Mheshimiwa Mary Masanja, nijikite leo kwenye ushauri kuliko kuwapondea sana. Sekta hii ni sekta ngumu sana, maana ni sekta ambayo wanafanya kazi na watu. Ni sekta ambayo Wasukuma wanalia, wafugaji. Niliona jana Mheshimiwa Waziri ametengeneza *Operation Ondoa Mifugo Kwenye Hifadhi*. Unajua kuna vitu vingine unaweza ukakiona kama tu kitu cha rahisirahisi ukakitengeneza mtu mkubwa, lakini baadaye kikaumiza sana wenzako, binadamu wenzio. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa niaba ya wananchi wa Mbogwe. Ninalo pori ambalo ni la Kigosi, namshukuru Waziri ameniahidi kwamba, endapo atapata *advantage* kwenye ufalme wake atanisaidia kwani lile pori limesahaulika, barabara hazipitiki, hata wale wataalam wa Mheshimiwa Waziri wale wanaolilinda hawana barabara nzuri za kuweza kupitika. Ni vyema sasa muweke kwenye bajeti hii ili barabara ziweze kuchongwa na ziweze kupitika vizuri ili kuweza kupambana na ujangili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili niombi tu kuishauri hii Wizara, sheria zibadilishwe, binadamu wathaminiwe kuliko kuthamini tembo pamoja na nyoka na wanyama wakali ambao hawana faida kwetu sisi binadamu. Nikisoma maandiko, sisi binadamu tuliumbwa kwa mfano wa Mwenyezi Mungu, lakini wapo watu ambao wanalinda

kwenye mapori yetu haya hawana huruma, ni watu ambao kweli wanatekeleza hizi sheria. Kwa kuwa, sheria sisi ndio tunazitunga, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Waziri, tuzirekebishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwa ni hatari sana mtu labda hata amepotea njia tu akapita kwenye mapori yetu ambayo hayana sifa ya kuwa hata mapori anapigwa risasi. Vilevile ng'ombe, nikiangalia ng'ombe wanachukiwa sana kwenye hii Wizara kana kwamba, yaani sio pato lenyewe. Nikiangalia wengi humu tumeolea ng'ombe, hakuna mtu aliyeoa akatoa mahari ya tembo, kwa hiyo, niombe ng'ombe wathaminiwe sana, tutengeneze utaratibu mzuri kwenye hii sekta. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua katika utalii wasiangalie tu wazungu ndio watalii, hata ng'ombe nao ni watalii, tukipunguza *fine*, badala ya laki kila kichwa cha ng'ombe tukaweka elfu hamsini hamsini kila ng'ombe atakayekamatwa porini tutakuwa tumepata watalii. Mimi ukiniambia neno watalii kwanza silljui maana Ngorongoro sijawahi kufika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Waziri itakuwa ni vyema na Wabunge wengine maana wanaongelea tu hili suala la utalii, hawajafika kwenye pori lolote na wanajaribu kutoa mifano ya Indonesia ya uwongo mtupu. Kwa hiyo, ni vema... (*Kicheko*)

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiruswa, Taarifa. Mheshimiwa Maganga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumfahamisha mzungumzaji kwamba, kuna bidhaa ya utalii wa mseto ambapo kule ulaya wazungu wanasema *go to Serengeti and Ngorongoro to see the lion*

and the Masai. Kumaanisha kwamba, unaweza kwenda Ngorongoro au Serengeti ukamwona Mmasai ambaye ni binadamu na mifugo na wanyama. Kwa hiyo, biashara ya utalii mseto inawezekana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Yaani unampa taarifa kwamba, Mbogwe pia, wanaweza wakakaa na wanyama porini, ndio unachojaribu kusema?

Nadhani hilo mmefanikiwa nyie Wamasai, sina uhakika na wao kwa sababu, wao wanyamaporini wanakula, ninyi kule kwenu Ngorongoro mmewaacha wanyama waendelee na maisha.

Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilindie muda wangu nina vitu vya msingi hapa na vya maana sana. Naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mbogwe, Pori la Mkweni, lilitamaliza sifa ya kuwa pori maana halina tembo, halina wanyama wale wanaoangaliwa na watalii. Pori lile sasa hivi wamejaa Wachina, wanachimba usiku, lakini binadamu wakionekana mle wanavunjwa miguu pamoja na ng'ombe wakiingia mle wanatozwa laki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wapo vijana wa Mheshimiwa Waziri, ng'ombe wakiwa wanapita hata barabarani, maana pori lile limepakana na barabara ya lami, ile barabara kuu iendayo Kongo, wakionekana ng'ombe wanapita barabarani wanakamatwa wanaingizwa kwenye pori. Lengo na madhumuni kwa kuwa *fine* ni kubwa, ni laki moja, wanapata mwanya wa kupatia rushwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta hii , nataka nimweleze ukweli Mheshimiwa Waziri, maana nampenda pamoja yuko na dada yangu, wakae wakijua kabisa watu wanateseka sana walio jirani na mapori. Kwa maana hiyo,

ni vyema sasa hata wanapotengeneza huu mpango wa *Operation Ondoa Mifugo Porini* kwanza wajue kabisa kwamba, wana watu wa aina gani na kidogo Waziri ajaribu kuonesha makucha wasiwe wanawaonea tu watu wenye ng'ombe, maana sisi sote tumetoka huko kwenye ng'ombe, tunajua machungu ya ng'ombe hatujui thamani ya tembo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, mimi binafsi namchukia sana mtu anayechukia ng'ombe na kuthamini tembo. Maana tembo hawa tunategemea mpaka watu watoke Canada na sehemu nyingine ili tupate pesa za kigeni, lakini sisi wenye tukiwekeana utaratibu, tukawa tunachungia kwenye mapori yetu, kwa kuwa mapori yetu haya tuliyopewa na Mwenyezi Mungu ni makubwa, tukaweka *fine* hata ya shilingi 50,000, lakini vilevile kwenye llani ya Chama chetu Cha Mapinduzi kwenye ukurasa wa 52 tuliahidi kwamba, tutatenga kwenye mapori yetu maeneo ya kuchungia ng'ombe. Ni vyema na lenyewe hizi Wizara naziona zinafanana, ni kama kurwa na doto, sekta hii pamoja na sekta ya ardhi, wakakaa ili kusudi wakalitengeneza hili suala ili watu waweze kuishi vizuri kwenye mapori yao hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umeshaisha Mheshimiwa, kengele imegonga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, zimeisha?

NAIBU SPIKA: Ee, ndio muda umeisha Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, basi naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Haya, asante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi ajiandae.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara muhimu ya Maliasili na Utalii. Kimsingi nikiangalia michango ya Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba, wote tunakiri kuna kazi kubwa sana ambayo imefanywa na Wizara hii katika ku-*transform* sekta ya utalii kwa maana ya kuongeza idadi ya watalii, lakini pia kuongeza pato la Taifa, lakini bado kuna kutokuridhishwa kwa Wabunge wengi kwa jinsi hali inavyoenenda katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia michango ya Waheshimiwa Wabunge unaweza kuona kwamba, wengi wanaona kwamba, sekta hii haijatendewa haki kwa maana kwamba, kuna fursa nyingi za utalii ambazo bado hazijaguswa. Tumejikita sana kwenye utalii wa wanyamapori, lakini kuna talii za fukwe kuanzia Tanga mpaka Mtwara ambazo hazitumiki kikamilifu, tuna talii za kwenye visiwa ambazo hazitumiki kikamilifu, lakini tuna talii za kiutamaduni ambazo hazitumiki kikamilifu. Kwa hiyo, sekta hii ya utalii ikigusa maeneo yote haya naamini kabisa tunaweza kupata tija ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunaona kwamba, pato ambalo linatokana na utalii kama tunaenda ku-*adapt* sera ya ugatuaji wa madaraka ya *D-by-D*, kama tunaenda kushirikisha wafanyabiashara wadogo katika sekta ya utalii, tunaweza kwenda kuona makubwa katika sekta hii. Tatizo la sekta yetu ya utalii imehodhiwa na wafanyabiashara wachache wakubwa na hawa ndio ambaao wana-*drive* hii sekta kwa kuweka masharti magumu ambayo wafanyabiashara wadogo katika sekta ya utalii kushindwa kuingia na kufanya biashara. Matokeo yake vijana wachache ambaao tunawaelimisha kwa gharama kubwa katika sekta ya utalii wanaishia kuwa watumishi na vibarua katika sekta ya utalii na sio kama wajasiriamali katika sekta hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba kuitia Bunge lako wananchi wetu, hasa vijana wetu ambao wamesomea utalii wawekewe mazingira wezeshi ya kuingia katika sekta ya utalii kama wajasiriamali na sio kama vibarua. Ninachokiona kuna cha kujifunza kwa wenzetu, hasa nchi za Asia, kule wenzetu utalii mwingu uko katika ngazi ya familia katika ngazi ya vijiji. Huwezi kukuta mahotelii makubwa makubwa katika maeneo mengi ya vivutio, utakuta kuna *bed and breakfast*, utakuta kuna *vi-lodge*, kuna vihoteli ambavyo vinaitwa *boutique* kule Myanmar, Laos, Thailand hata Cambodia. Unaona kabisa jinsi gani utalii ulivyoenda kuajiri watu wengi kwa mpigo ukilinganisha na kwetu ambapo tunategemea wawekezaji wachache kuajiri vijana wengi kama vibarua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanahitaji fedha. Kitendo cha kuondoa fedha za Mfuko wa Utalii kupeleka katika Mfuko Mkuu wa Hazina, kwa kweli kwa namna mona ama nydingine imeuwa sekta ya utalii. Naomba Serikali ilitafakari tena upya kwa sababu, tuna maoni mengi ambayo tunataka Wizara hii isimamie mabadiliko katika sekta ya utalii, lakini swali, fedha wanapata wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha inabidi waombe kama wengine wanavyoomba kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Hali hii haitatupelekea sababisha kuona mabadiliko yale ambayo tunayatarajia katika sekta hii ya utalii. Ombi langu, ni Serikali kuona jinsi gani inarejesha Mfuko huu wa Utalii na ili Wizara isimamie mapato haya kwa ajili ya kuwekeza kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika *ku-transform* utalii wetu, lakini pia katika ujenzi wa miundombinu katika mbuga zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mawasiliano katika mbuga zetu ni suala la muhimu. Mtalii anayeingia Mikumi anaweza akaingia toka asubuhi mpaka jioni asitume *status* kwenye WhatsApp kwa sababu hakuna simu, lakini pia hata akitaka kutoka pale Mikumi kwenda Ruaha atapita pale Ng'apa, atapita Msimba, atapita Ruaha hana mawasiliano hata ya simu. Halafu tunataka mtalii huyu aende akatangaze

utalii kwao? Hakuna utalii mzuri kama watu kushuhudia nini ambacho kinaendelea katika mbuga za wanyama, lakini kama hawawezi wakajirusha wenyewe kwenye *status* kuonesha kwamba, nini wanachokiona katika mbuga zetu, si rahisi kushawishi wengine kuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nchi yetu kama ilivyo katika nchi nyingine, kasheshe la *corona* liliathiri sektu yetu ya utalii, lakini ilifungua fursa ya watalii kutoka nchibya Urusi ambaao walikuja kutokea Zanzibar. Sasa naomba Serikali iione hii kama fursa kwa nchi za Baltic na Russia kama sehemu ya kuhamasisha utalii wa kuja moja kwa moja kutokea Zanzibar kuja Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Deus Clement Sangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi na Mheshimiwa Ahmed Ali Salum ajiandae.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu niliyotumwa na wananchi wa Jimbo la Kwela katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu kwa kazi nzuri wanayochapa katika Wizara hii, wataalam wa Wizara hii pamoja na Kamati ya Bunge inayosimamia Wizara yao kazi ni nzuri, niwape pongezi zangu za dhati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi zangu, naomba niwakumbushe Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri hapo. Mnamo tarehe 12 Februari niliuliza swali kuhusu mgogoro wa *Uwanda Game Reserve* kule katika Jimbo langu la Kwela. Huu mgogoro umetutesa sana wananchi, hasa wa Kata ya Kapenta, Nankanga, Kilangawani na Kipeta baada ya hili pori kuchukuliwa na askari wa TAWA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzo lilikuwa linamiliikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, mwaka 2013

walipochukua ndio matatizo yalipoanza, maisha ya wananchi yamekuwa ya mateso miaka saba. Naibu Waziri ni shahidi, kila wiki nampigia simu zaidi ya mara mbili nampelekeaa migogoro, nashukuru ananisaidia, wananchi wangu juzi walinyang'anywa mipunga na askari, wamerudishiwa. Pia wavuvi wale wa Forodha ya Nankanga waliokuwa wamelazimishwa walipe shilingi milioni nane, Waziri ameingilia kati hawakulipa zile shilingi milioni nane. Nawapongeza kwa jitihada hizo ni nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hii ni *ad hoc solution*, tunatakiwa tuwe na *permanent solution*. Baada ya askari wa TAWA kuchukua pori lile mipaka ilivurugwa, haieleweki, kwa hiyo, wananchi wamebaki *dilemma* kwa miaka saba. Wamekuja Mawaziri waliowatangulia wanaahidi na wakawaambia wananchi tumeunda timu ya Mawaziri saba tutawapa majawabu, mlimi nimekuwa nikifuatilia hayo majawabu sijayasikia, wananchi wako hawajui kinachoendelea. Kwa bahati mbaya hii *Uwanda Game Reserve* hata wanyama wenyewe sio wengi, wako tembo wanen na nyati wawili tu na kwa miaka minne iliyopita tumepata watalii wawili tu, *for four years* watalii wawili. Kwa hiyo, imekuwa ni *cost generation centre rather than revenue generation centre*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri, kutokana na mabadiliko ya tabianchi Ziwa Rukwa linakua, limekua mpaka limeingia kwenye hifadhi, wavuvi wakiingia kuvua kwenye hili wanawakamata...

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa Taarifa mzungumzaji kwamba kilichopo kwenye hiyo *game reserve* anayoitaja, tuna *game reserve* pia nytingine iko *Masasi DC* inaitwa Misyenjesi. Wananchi wanatamani waachiwe lile eneo wafanye shughuli zao za kilimo kwa

sababu haina manufaa yoyote kwao na hakuna wanyama pale ndani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sangu.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hiyo Taarifa. Naomba niendelee kuchangia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deus ili uweze kuongea lazima nikuite tena, sawa?

Haya, Mheshimiwa Deus Sangu unapokea Taarifa hiyo?

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naipokea hiyo Taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nitoe ushauri kwa Wizara hii, waliniyahidi kwamba, tutaenda kutembelea hili pori. Nashukuru, nasubiri hiyo ahadi yao na aliniahidi Waziri kwamba, tukimaliza bajeti hii tunaenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wanakamata vifaa vyao. Boti ukilichukua ukalitoa kwenye ziwa ukaweka nchi kavu miaka mitatu, baada ya hapo wakifanya mnada inakuwa ni kuni, inakuwa hasara kwa mvuvi pia inakuwa hasara kwa Serikali, hakuna kitu kiinachozalishwa pale. Kwa hiyo, niwaombe sana ili tuondoe migogoro hii na kufanya ile *Uwanda Game Reserve* tutoe vibali kwa wavuvi wakavue kwa vibali, kwa sababu kitendo cha kutotoa vibali mmewahalalishia askari waanze kuchukua rushwa. Mvvi anatoa shilingi milioni moja, hela zinaenda kwa mtu binafsi, Serikali hawapati chochote, si bora watoe vibali ili waingize fedha katika Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana Wizara hii. Migogoro hii hata Rukwa Lukwati kule kuna mgogoro wa aina hii, wavuvi wananyanyasika sana. Wavuvi wanakuwa *charged* mpaka shilingi milioni tatu, hizo fedha wanachukua askari binafsi, Serikali haipati hata senti moja,

mateso ni makubwa, wananchi wameumizwa sana. Niwaombe sana watakapokuwa wana-*wind up* watoe kauli, migogoro ile wataimaliza lini ili la wananchi wa Kata ya Nankanga, Kapenta, Kipeta, Kilangawane, wafurahie kwamba, kuwepo kwa ile *Uwanda Game Reserve* kuna faida kwa sababu, wanatusaidia katika *bio diversity conversation*. Wamekuwa wakitusaidia pamoja na kwamba hamna watalii, lakini pia utunzaji wa mazingira, lakini wananyanyasika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ali Salum na Mheshimiwa Esther Edwin Maleko ajiandae.

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote nawapongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nawashukuru kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia kila mara tunapokuwa na changamoto, lakini pia nawapongeza wameanza vizuri, kasi yao ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia, Dkt. Kijazi kwa kazi nzuri, wananchi wa Serengeti wanatambua kazi yake pia. Nampongeza Mhifadhi Mkuu wa *Serengeti National Park*, Ndugu yetu Mwishawa anafanya kazi nzuri. Nadhani wote wamesikia hifadhi ile sasa imekuwa ya kwanza mara mbili mfululizo katika kuwa hifadhi bora Afrika, nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka siku moja Dkt. Bashiru alishauri Bunge hili ni vizuri likaweka *record* kuwa limeweza kusaidia ku-*transform* kilimo. Nishauri pia katika nchi yetu maeneo mawili pekee ambayo tunaweza tuka-*compete* kiuchumi ni kilimo na utalii tu, kwa sababu tunazo rasilimali nyingi sana katika eneo hili la utalii. Kwa hiyo niombi Serikali kwa safari hii tuwekeze sana katika utalii. Wabunge wenzangu wengi wamechangia kuwa bado *performance*

yetu si nzuri uki-*compare* na rasilimali tulizonazo, lakini nikiangalia si kwamba kwa sababu Wizara haifanyi kazi, hawatendi kazi, *no naangalia ni how much tuna-invest* katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Wizara sasa ijielekeze *core business* yake iwe ni biashara ya utalii, siyo kwenye uhifadhi tu na tutoe fedha nydingi tu *investsana* katika *marketing*. *Marketing* ina mambo mengi sana, ina watu wanaofanya kazi, *product zetu, service delivery*, miundombinu na vitu vingi sana. Kwa hiyo tujielekeze huko tunaweza tuka-*transform* sekta hii na kuifanya nchi yetu ifanye vizuri kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ningeomba Wizara hii pamoja na jitihada nzuri wanazozifanya, sasa waongeze kasi kwenye kutatua matatizo au migogoro iliyopo kati ya hifadhi pamoja na wananchi. Simba na tembo wameendelea kuua sana wananchi katika Jimbo langu la Serengeti. Najua jitihada zipo, lakini naomba ziongezwe na niombe sana Wizara hii ni vizuri sasa wale askari wa wanyamapor wa-*shift focusyao*, pengine wasikae kule ndani ya hifadhi, zamani wananchi walikuwa hawana *awareness*, sasa hivi hawaendi kuwinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa wale askari hata wangewajengea nyumba waishi huku vijijini, wapewe pia magari ili kwamba tembo anapoingia wawe huko, kuwapigia wale watu simu usiku ni ngumu. Sasa hivi ninapoongea ukienda Kata za Issenye, Natta, Nagusi ukienda Ikoma, Machochwe, kule Merenga, watu wanakaa usiku kucha wakilinda tembo wasiingie na wakati huo hawana silaha wala hawana magari. Kwa hiyo, nniombe sana Wizara, waende sasa wawahamishe wale askari, sasa hivi watu hawawindi, wakae huko ili waweze kutusaidia kufukuza tembo wakati wa usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo la mipaka, kuna vijiji saba mpaka sasa mipaka ile haijawa *solved*. Niombe sana mipaka ile waende kutatua hili tatizo, ni la muda

mrefu na wananchi walifungua kesi, wakashinda. Niombé vile Vijiji vya Mbirikiri, Bonchugu, Sedeco viweze kusaidiwa ili viweze kuondokana na tatizo hili, ilimekuwa ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala hili la kutaifisha mifugo mbona toka wameendelea kutaifisha bado watu wanaingiza tu. Kwa hiyo unaweza ukaona kuwa, hii sheria haiwezi ku-work, ni vizuri sasa suala hili la uhifadhi tuwashirikishe sana wananchi. Tuwashirikishe kwa kiwango kikubwa, nafikiri tunaweza tukatatua tatizo hili na likaisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, niiombe Wizara hii iangalie namna ya kuongeza namna ya wananchi kufaidika zaidi na utalii. Hapa nishauri eneo moja tu, hizi hoteli za kitalii ni vizuri sasa Wizara itafute namna ya kuboresha sera, zijengwe katika vijiji vya jirani ili wananchi waweze ku-trade kwa urahisi na hoteli hili, lakini pia uwepo wa hoteli hizi katika vijiji vinavyozunguka hifadhi itaongeza ile *spirit* ya kuhifadhi hifadhi zetu pamoja na ku-change ile *mind set* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Wizara tuende kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika kuona tunatengeneza miundombinu mizuri kule ndani ya hifadhi na katika vijiji ambavyo vinazunguka hifadhi. Leo wananchi wengi ukiwaambia hizi hifadhi zina maana zinaweza kusaidia nchi, hawaoni maana yake. Unamuuliza mwananchi kwa nini aendelee kuingiza ng'ombe ndani? Kwa nini aingie ndani ya pori kuwindia? Yeye anaona akiingia yeye binafsi anapata faida kubwa kuliko faida ambayo anasikia kwamba Taifa linapata, lakini tukimsaidia, akaona shule zinajengwa, barabara zinajengwa, vituo vya afya vinaboreshwaa, anaweza kuelewa na akawa mtu namba moja katika kuhifadhi maliasili zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Edwin Maleko na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris ajiandae.

Mheshimiwa Ally hayupo, Mheshimiwa Ester Edwin Maleko atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae.

MHE. ESTER E. MALEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii nyeti ya Maliasili na Utalii. Kwanza nianze kwa kutoa pongozi kwa Waziri Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mary Masanja kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia nitoe pongozi za dhati kwa timu nzima ya Wizara kwa sababu wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye kuchangia kwa sababu mud ani mfupi sana. Naomba nichangie kupitia utalii kwa sababu kwa kwetu sisi Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vingi nya asili ikianza Brazil ambayo ni nchi ya kwanza duniani kuwa na vivutio vingi nya asili. Pamoja na hayo sekta hii ya utalii inachagia pato la 17% katika pato la Taifa. Si hivyo tu, inachangia ajira zisizopungua milioni 1.6, zile za moja kwa moja na ambazo siyo za moja kwa moja. Kwa hiyo, Wizara hii ni nyeti kwa sababu pia inaingiza asilimia 25 ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye kuchangia kwenye vivutio vyetu nya asili. Tuna kivutio kikubwa sana katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro. Kivutio hiki ni mlima Kilimanjaro, mlima huu kwa takriban watalii 45,000 mpaka 50,000 wanapanda kwa mwaka. Hata hivyo, kiikolojia mlima huu unaweza kupokea takriban watalii 300,000 kwa mwaka mmoja. Hivyo, unaona idadi ya watalii wanaopanda mlima huu ni 45,000 mpaka 50,000, ina maana kuna nafasi hapo ambayo hatufanyi vizuri. Nadhani hatutangazi vizuri mlima wetu au matangazo yako chini sana, kwa hiyo tujitahidi sana kutumia *media*. Leo *media* ni kitu kikubwa sana, watu wanashinda kwenye *media*, tukiweza kutumia tu *Instagram* kuutangaza mlima wetu, ambapo hatutumii gharama yoyote

kubwa, tunaweza kuutangaza kwa kiasi kikubwa lakini pia hatuwezi kutumia gharama kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tukachukua watu maarufu mfano Ronaldo, Messy na wengine wengi tukawafanya wao wakaja Tanzania, tuisiwatoze hata senti tano, tukachukua wao wanapokuja Tanzania wakalala bure wakapata huduma zote bure, lakini yule mtu aka-post tu kwenye page yake yenye *followers* zaidi ya milioni 50 kwamba yuko Kilimanjaro, tayari tumetangaza mlima wetu na hatutumii gharama kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, nimeona Wizara inafanya vizuri sana, wamemleta Mamadou kama balozi wa utalii, lakini si hivyo tu jana amekuja *Zari the boss lady* kama balozi wa utalii. Namshukuru Mungu nilipata nafasi ya kuzungumza naye na kubadilishana mawazo. Kama Mbunge ninayetoka Kilimanjaro nilimwalika aweze kuupanda Mlima Kilimanajro na amekubali, hivyo nawahamasisha Wabunge tuungane pamoja kwenda na Zari kuupanda Mlima Kilimanjaro kwa sababu sisi ni vivutio na sisi ni wawakilishi wa wananchi. Wananchi wakiona sisi tunaenda kupanda mlima Kilimanjaro, nao watahamasika na wataenda kupanda mlima. Kwa hiyo nawaomba Wabunge tuungane pamoja kupanda mlima Kilimanjaro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, tunapaswa pia kuboresha *rescue system* katika mlima wetu wa Kilimanjaro. Watalii wanapokuja wakapata shida wakiwa kule mlimani wanapaswa kupata huduma sahihi. Ninaposema *rescue system* iboreshe, naamini Wizara inajua namaanisha nini. Kwa hiyo ninaomba Wizara iboreshe *rescue system* iwave wale watoa huduma elimu bora zaidi ili iweze kuwahudumia watalii wanaopata shida wakiwa kule mlimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu tuwe na *information center...*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga.

MHE. ESTER E. MALEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa Mheshimiwa Ester hujatuambia kama na wewe utakuwa unapanda, kwa sababu wako Wabunge hapa ambao watatamani kujua kama na wewe unapanda ili waambatane na wewe.

MHE. ESTER E. MALEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, nimewahamasisha kwa sababu na mimi nitakuwa mmojawapo kwa sababu nimemhamasisha Zari apande Mlima Kilimanjaro, nitakuwa pamoja nao. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt Oscar Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ajiandae.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu ya wataalam ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kwa kuwa muda ni mchache, niombe nijikite katika maeneo kama mawili, matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, niiombe Wizara kuna mbuga mpya ambayo imetangazwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo zamani ilikuwa ni pori la hifadhi. Niombe Wizara mbuga hii ni kubwa ina wanyama wengi, ina wanyama wakubwa na wazuri ambao inaweza kuwa ni kivutio kikubwa kwa watalii katika nchi.

Ombi langu kwa Wizara ni kwamba utangazaji wa mbuga hii bado haujakuwa mkubwa kiasi cha kuwafanya watalii wengi wafike kule. Ukiangalia bado tunatangaza mbuga ambazo ziko kaskazini wakati mbuga hii ni kubwa

inaweza ikaongezea mapato makubwa Serikali na kufanya kwamba mambo yaye mazuri katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naamini kabisa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo linajengwa kule nalo linaweza likawa ni moja ya kivutio kikubwa cha watalii. Kwa hivyo niombe sana Wizara iangalie hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ningependa kuchangia na sisi Morogoro kule kuna eneo linaitwa Kisaki majimoto. Kuna maji ambayo yanachemka na mayai yanachemshwa. Niombe nacho ni kivutio ambayo Wizara kwa namna moja au nyngine watume wataalam wakaangalie jinsi gani wanaweza wakakitumia kivutio hicho kuongeza mapato kwenye Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo ningependa kuchangia katika Wizara hii, kati ya mwaka 2016 na mwaka 2021, kuna watu 46 wameuawa na mamba, kuna watu 15 katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijiji wamepata vilema vyta kudumu kutokana na ongezeko kubwa la mamba katika Mto Ruvu na Mto Mvuha ambao unapita katika Vijiji vyta Tununguo, Mkulazi, Selembala pamoja na Kijiji cha Mvuha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, idadi kubwa ambayo imetokea katika vifo kutokana na mamba imetokea katika Kata ya Selembala. Mwaka 2016 kumetokea vifo vyta watu watatu; mwaka 2017 kumetokea vifo vyta watu tisa; mwaka 2018 watu watano; mwaka 2019 watu sita; mwaka 2020 watu 14 na hadi Mei mwaka huu, watu tisa wameshakufa katika Kata ya Selembala. Kuna taharuki kubwa kwa watu na hasa ukitilia maanani watu wengi vijiji wanatumia maji ya mto wanashindwa kwenda kuchota kwa sababu wakienda wanakumbana na vifo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali, naamini kwamba mamba wamekuwa wengi na naamini kwamba ni wakati muafaka kwa sasa kwenda kuvuna mamba hao ili tuepushe vifo vyta watu, lakini wakati huo huo

tukapata fedha katika kuuza ngozi za mamba hao. Sambamba na hili vile vile nikuombe kupitia Wizara kwamba, tunaomba vifuta jasho kwa watu hawa ambao wamepoteza maisha kwa mujibu wa taratibu na sheria za maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe vile vile kupitia Bunge lako Tukufu, kwa Wizara ya Maliasili na Utalii isaidie Halmashauri ya Morogoro Vijijini kwa vitendea kazi vya magari, lakini vile vile Askari wa Wanyamapori ili waweze kwenda kutusaidia ongezeko la wanyama ambao wamefanya uharibifu mkubwa kwenye Kata ya Kisaki, Kata ya Bwakila Chini, kata ya Serembala, Kata ya Mvuha. Nashukuru na naipongeza Wizara katika mwaka 2019 tumelipwa kifuta jasho kwa wakulima ambao waliharibiwa mazao na wengine ambao wamepoteza maisha wamepata kifuta jasho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado katika mwaka 2020 hatujapata kifuta jasho kwa wakulima ambao ekari 572 zimeathiriwa na ongezeko la wanyama hao waharibifu na wengine ambao wameshambulia watu. Ombi langu kwa Serikali...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, muda wako umeisha Mheshimiwa.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu na Mheshimiwa Amour Haji Amour ajiandae.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii kuchangia Wizara hii. Niungane na wenzangu Wabunge kuwapongeza Mheshimiwa Waziri,

Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameongea mazao mapya ambayo wameyaongeza kwa ajili ya kuongeza chachu na ufanisi katika Wizara ya Utalii, nayo ni utalii wa uvuvi na kujiburudisha, utalii wa kula Wanyama pori, utalii wa kula chakula porini na utalii wa kupiga makasia. Nawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wengi tumetembea katika nchi za wenzetu. Kwa mfano ukienda Misri, pamoja na kuangalia zile *pyramids* lakini jioni mkitoka kuangalia yale ma-*pyramids* mtakwenda Mto Nile, mtapiga ma-*cruise*, kuna ngoma za asili, mtakula chakula, inaongeza *value* kwenye *package* ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tanzania tutumie na sisi akili zetu jamani, tusibakie kwenda kuangalia wanyama sjui wapi, kuangalia sjui Tarangire, sjui Serengeti, tuongeze *value* kwenye kuangalia wale Wanyama, jioni hawa watalii wanaangalia nini, wanafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Hongkong pale ile Hongkong ilivyokaa ina vilima mithili ya Mji wa Mwanza, lakini vile vilima wamehakikisha wamevitunza na ni sehemu ya vichochoeo vya utalii, ile jioni mnapanda kwenye mlima mnaangalia Hongkong pale chini. Angalia Mji wetu wa Mwanza tunautumiaje kwenye sekta ya utalii, tumebakia na sekta ya utalii ambayo hatujaijumuisha na mazingira ya maeneo ya utalii wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna ziwa Victoria pale na maziwa mengine tunayaunganishaje kwenye sekta ya utalii kwa mfano Ziwa Victoria, Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi yupo pale, kuna kipindi pale Bukoba walikuwa wameandaa kuwa na *cruising party* kipindi cha mwisho wa mwaka, lakini ukienda kuazima meli ile ya Victoria wanakwambia hii siyo kazi yetu, siyo kazi ya utalii hii, ni kana kwamba Wizara ya Utalii inajitegemea, Sekta ya Uchukuzi inajitegemea lakini tunapaswa kuwa *holistic approach* tunapokuja kwenye sekta ya na masuala yote ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Burigi Chato, nawashukuru Serikali ile hifadhi ilikuwa ni majanga miaka ya nyuma, tusingepita mle, lakini kwa kuanzisha hii hifadhi imetuongezea usalama watu wa kanda ya ziwa. Nimwombe Waziri Burigi ndiyo imebeba maana ya ile hifadhi. Tuna Ziwa Burigi pale ambalo kwa bahati nzuri kama hawajawahi kufika, lakini najua hawawezi kufika kwa sababu lile eneo la Burigi halifikiki, hakuna barabara nzuri, lakini pili kama mchangiaji mmoja alivyosema hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, wakati anakuja ku-*wind up* atuambie wana mkakati gani kuhakikisha kwamba lile Ziwa Burigi linafikika. Watalii watakapokuja na nina uhakika, watalii wengi watatokea Bukoba kwenda kwenye Hifadhi ya Burigi Chato, tuhakikishe upande wa Muleba tunakuwa na *gate* kubwa la kuhakikisha kwamba watalii watakapotoka Bukoba kwenda Burigi Chato wanapata sehemu ya kuingilia, badala ya kuzunguka kwenda Biharamulo kwenda sijui Chato, waingilie eneo la Muleba. Mheshimiwa Waziri atatupa maneno yakeo atakapokuja kuhitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, wakati nachangia Wizara ya Mifugo, niliongelea hili suala la kuchukua mifugo. Bahati nzuri wewe mwenyewe ni Mwanasheria, Waziri ni Mwanasheria, wanajua maana ya sheria. Inapokuja katika Wizara hii, mifugo imelingizwa kwenye Hifadhi mwananchi wangu nilimwongelea katika Wizara ya Mifugo...amekamatwa, amefunguliwa kesi ya kuingiza mifugo kwenye hifadhi, ameshinda. Siku hiyo hiyo amekamatwa kwa kosa lingine eti ameharibu uoto wa asili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mahakama imesema arudishiwe mifugo yake kwa nini watu wa Wizara hii wanakaa na mifugo ya wananchi jamani! Wanafanya wananchi wachukie Serikali yao kana kwamba Serikali imewaibia mifugo yao, lakini ni watu wachache. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie wanatupatia wakati mgumu kwenye majimbo. (*Makof!*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga hoja mkono. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Jumanne Miraji Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Amour Haji Amour na Mheshimiwa Tabasam Hamisi Mwagao, ajiandae.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Nianze kwa kuwapongeza sana Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri, lakini pia kwa wasilisho lao ambalo wameliwasillsha mbele yetu. Wasilisho hili limeonesha mipango mizuri ambayo wanaipanga kwa ajili ya mwaka mmoja ujao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kuratibu shughuli hizi. Wote tunajua kwamba sekta ya utalii ni milongoni mwa sekta zinazotupatia fedha nyingi sana katika mapato ya nchi. Kwa hiyo ni maana yake ni kwamba, tunapotoa ushauri hapa tunataka tuendelee kuwa na uhakika wa mapato hayo ili kuisaidia nchi katika maendeleo. Wengi wamenekuu taarifa yake asilimia 17 ile ya Pato la Taifa, lakini tunapata asilimia 25 ya fedha ya kigeni, ambazo kwa kweli ni fedha nyingi zinazotuimarisha katika kuleta huduma za wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maeneo yangu nitasema pamoja na kuwa *TANAPA, TTB*, pamoja na wenzetu wa *TAWA* wanavyoratibu shughuli za utalii, lakini kuna wenzetu hawa wa sekta ya binafsi ambao ni *tour operators*, wanafanya kazi nzuri sana kusaidiana na Wizara. Ombi langu ni dogo tu kwamba, kuna baadhi ya mambo ambayo yanapaswa tuwawezeshe na kuwaimarisha ili waweze kufanya kazi nzuri kwa niaba ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli watu hao wanafanya kazi nzuri na Wabunge wengi wamesema hapa. Hivyo, changamoto zilizopo ni vizuri tukazitafutia ufumbuzi ili waweze kufanya kazi nzuri na kusaidiana na Serikali, kwa sababu wao wanakutana moja kwa moja na watalii, wao ndiyo mawakala wanaowaleta watalii katika nchi yetu. Baada ya sisi kutangaza kama nchi, wao ndiyo wanaratibu kule katika shughuli zao mbalimbali kwenye vivutio vyetu. Kwa hiyo, niombe Serikali wapate muda, wakae na na hao wenzenetu, waweze kuwapa taarifa mbalimbali zinazohusiana na taarifa za watalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watalii hawa lazima tufikirie kwamba wao wanataka nini ili tuweze kuwatafutia kile wanachotaka, tusiwe tunaandaa sisi kwa utashi wetu. Ni sawasawa wewe una duka, stahili ya nguo fulani unaiza unazozipenda wewe badala ya kutafuta nguo wanazopenda wateja. Kwa hiyo, hili ndiyo tatizo ambalo tunaliona liko mahali pale. Kwa hiyo niombe sana Wizara wakae na hawa *tour operators* waweze kuwaambia *taste* ya watalii wanaokuja nchini wanataka nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kikwazo kimojawapo ni pale mfano Serengeti; wamekuwa wana *imitation* katika yale makambi, wamezuia kuwa na mahema 10, sheria inasema kuwe na mahema kumi, maana yake mnamlazimisha huyo *tour operator* aweze kuwa na kambi nyingi ambazo zinamwongezaa mzigo. Kwa hiyo niombe sana angalau waongeze badala ya kuwa na hema kumi, ziwe hema 25 zisaidie kuwa na watali wengi katika eneo moja kwa ajili ya kusaidia kupunguza gharama ambazo wanaziingia hawa watalii ambao wanakuja kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee tu kwamba wawe na mikataba, badala ya miaka mitatu basi waende hata minne na kuendelea ili wawasadie kuwa na muda wa kutosha. Kama wachangiaji mbalimbali walivyosema leo limetokea tatizo la *Covid-19* waweze ku-*compensate* gharama zao ambazo wamewekeza katika eneo hili, vinginevyo tutawafanya washindwe kuendelea kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo ni muhimu sana, Wizara wanajua katika sekta hii kuna tozo na kodi 20 ambazo ni nyingi sana, zinawaletea vikwazo wale wanaoendesha sekta ya utalii. Mfano mdogo, ukiangalia, kuna tozo nyingi ambazo zimekuwa ni kikwazo, ni vizuri wakaziangalia upya mfano kuna *TALA*, kuna Halmashauri, kuna *COSOTA*, kuna *NEMC, OSHA, Fire, Land Rent, Property Tax* na *Swimming Pool License* yaani zote analipa huyu ambaye anatakiwa kuja pale. Maana yake nini, unamfanya huyu mtu awe na mlolongo na utitiri mkubwa wa zile kodi ambazo zinawaletea matatizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri waangalie upya namna ambavyo wataweza kusaidia kupunguza ghamama na mlolongo huu wa utitiri wa kodi, kwa sababu tunajua kwamba kodi inasaidia kuboresha maisha ya wananchi kweli, lakini ni vizuri watu walipe kodi kwa furaha ili kodi hii iwe endelevu kwa ajili ya kuipata kwa muda mrefu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, niongelee suala la sisi kujitangaza. Kuna mikutano mbalimbali, niiombe sana Wizara iweze kuhudhuria kwa ajili ya kutangaza vivutio vyetu katika dunia. Mfano, kuna wenzetu wa *World Travel Market* ambaao ni *WTM*, tuendelee kwenda kule kwa ajili ya kupeleka taarifa zetu za vivutio katika nchi yetu ili kusaidia utalii wetu kuweza kutangazika duniani kote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja na naomba niwatakie kila kheri Wizara hii. Ahsante. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Amour Haji Amour, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamisi Mwagao na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, ajiandae.

MHE. AMOUR HAJI AMOUR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa ruhusa yako nami nawashukuru watu wote wa Wizara ya Utalii kwa ujumla. Mimi sitakuwa na

maelezo mengi ya kuchangia hasa kwenye mambo ya Maliasili nitagusa kwenye masuala ya Utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utalii zaidi nizungumzie mambo matatu au manne. Kwanza tufahamu wazi kwamba utalii ni biashara, utalii ni huduma, utalii ni miundombinu. Sasa wakati mwingine, wakati wa hoja hapa nilikuwa najaribu kusikiliza hoja zote hizi za Wabunge wote ambao wanaozungumza, nikaona kwamba kuna haja ya Wizara yenyewe maana yake kuwa na mdahalo maalum utakaowahuisha Wabunge pamoja na wataalam wa utalii kujadili suala la mfumo wa utalii wetu Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kutokana na ile michango mingi ambayo imetolewa ambapo kila mmoja kajaribu kuzungumzia upande wake hasa unaouzungumzia suala la utalii, kuna wale watu waliozungumza kwa kutoa mifano mbalimbali katika nchi tofauti ambazo wameshabihisha Misri, *South Africa* pamoja na nchi zote zilizokuwa na utalii wa hali ya juu. Tufahamu wazi kwamba nchi hizo zote hizo ambazo zimezungumzwa kwa mifano, tukiangalia ile *nature* ya zile nchi maana yake kunakuwa na *identification* ya kitu wanachokitangazia hasa katika nchi zao. Kwa mfano kama nchi ya Misri, ukiangalia hasa kivutio chao kikubwa maana yake pale watakuwa wanazungumzia suala la *pyramid*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumzia suala la *South Africa*, utalii wao mkubwa maana yake unategemea kumbi za mikutano. Sasa sisi Tanzania maana yake tujaribu kuangalia kwamba *identity* ya Tanzania yetu hasa ni kitu gani? Maana yake ni kitu ambcho cha kuweza kukitizama kwamba, sisi Tanzania tunataka kuingia katika suala la utalii au tuko katika suala la utalii ambao ni biashara, ambao ni ajira kwa Watanzania, je sisi hasa *identity* yetu kuhusiana na utalii hasa ni kitu gani? Utakuta kila mmoja anazungumzia suala la vivutio mbalimbali, kwamba kuna kuna kivutio cha Mlima Kilimanjaro, kuna kivutio cha wanyama, kuna kivutio cha utamaduni, lakini kuna vivutio vingine tunaviita kwamba ni *alternative* katika suala la utalii. Sasa hapa tunatakiwa

tuwe na utalii ule ambao ni *identity* kwa nchi yetu. Katika nchi yetu ukijaribu kutazama hasa sisi kwa Tanzania kipaumbele chetu hasa kwenye utalii ni kitu gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nijaribu kuishauri Wizara ni kwamba, wakati mwingine utalii kama ulivyo katika suala la mzunguko wake, utalii ndiyo kichwa ambacho nitasema kwamba kwa Wizara kinachoweza kuleta ile biashara yenye na kwa nini nazungumza hivyo? Nasema hivyo kwa sababu utalii wenye na ndiyo uliosababisha vichochezi vyta hizi maliasili maana yake kuweza kutambulika. Sasa bila ya utalii maana yake hivi vichochezi vyote, vivutio vyote hivi ya maliasili maana yake visingewenza kufahamika. Sasa ukiangalia kutokana na mfumo wetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii maana yake maliasili imekuja juu sana ambapo ningetegemea sana utalii uje juu, ikisha maliasili ndio iwe ndani ya utalii, lakini sasa sisi tuko katika hali ambayo ni kinyume. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine tujaribu kuangalia suala la utalii; ukiangalia kwenye bajeti zetu hizo tumejaribu kugusa sana masuala ya *international tourism*, lakini suala la *domestic* hatukuligusa hata kidogo. Suala la *domestic* ambalo nalo lina umuhimu wake, lakini katika *domestic* naoko tunahitaji tufanye kazi kubwa sana. Ili tuwe na *domestic*, wakati mwingine, pamoja na vivutio vyote tulivyokuwa navyo, lakini ningeshauri tutengeneze hizi *amusement park* katika yale maeneo ambayo tunakusudia wale wenyeji wawe wanafika na kupumzika. Kwa mfano kama hapa kuna Mbunge mmoja kazungumzia suala la Dodoma, kuna jiwe pale, kule kungetengenezwa *amusement park*, maana yake pengine ingekuwa moja ya kivutio cha ile jiwe na kisha ile *amusement* maana yake watu pengine wanawenza wakapumzika na kuendelea na shughuli nyingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala la utalii ni suala ambalo ni kubwa sana linahitaji huduma ambazo zilizokuwa bora, tunahitaji miundombinu iliyo kuwa bora. Ili tuweze kufanikiwa katika suala hili la utalii, hayo yote yanatakiwa

yazingatiwe kwa ubora wake, tuwe na huduma zilizokuwa bora, tuwe na miundombinu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, yote hayo juu ya utalii maana yake ni kuwa na amani. Bahati nzuri sisi Tanzania amani yetu inajitosheleza, kwa hivyo amani yetu ndiyo inaweza kutusababisha kwamba kila mmoja akawa ni kivutio kwa mtalii kuja nchini Tanzania kutokana na amani yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tabasamu Hamisi Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi na Mheshimiwa Mary Masanja, ajiandae.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara hii kufanya kazi kwa uzuri sana ya kupongezwa, lakini nina masikitiko makubwa sana kutokana katika Wizara hii. Wizara hii inayo wataalam ambao watalaam hawa ili wawe watalaam waliandika maandiko sasa tunashangaa katika hiki Chuo chao cha Mwika kuna tatizo la wafugaji na hawa wasimamizi wa wanyamapori watu wa *TAWA*. Hawa ng'ombe kisheria wanaitwa ni wanyama na tembo, simba na wenyewe ni wanyama kwa lugha nzuri ya Kiswahili wanaitwa *hayawani*. Kwa hiyo ng'ombe anaitwa *hayawani* pia na ndio maana wanachungwa hawana akili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kwamba tunasikitika sana, maliasili maana yake katika Kamusi ni kitu ambacho sisi tumekikuta kama urithi, ambacho kinakuwa ni sehemu yetu. Kwa hiyo ng'ombe ni maliasili katika nchi hii. Tunashangaa ng'ombe wakienda kwao, wale wametoka tu porini kuja kukaa na binadamu wakafugwa. Sasa wakirudi

kwao wanakuwa ni adui, wanapigwa faini wakati tembo wakija kwa binadamu hatujaona Sheria ya Maliasili inasema, wanapigwa faini kiasi gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunawaomba watu wa Wizara ya Sheria na Katiba watutengenezee sheria ya tembo akitoka katika eneo lake akaja kwa binadamu faini yake itakuwa ni bilioni moja, milioni mia tano ili wananchi tujue. Haiwezekani sheria ikawa ya upande mmoja, hakiwezekani kitu kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kukwambia ni kwamba, hakuna kitu kibaya zaidi kwa wananchi wanachoona kwamba wanatungiwa sheria wao, wakati wale wanyama wengine hawatungiwi sheria, kwa sababu hawa ng'ombe sisi tuliwakuta, tumewakuta kama maliasili na wakakubali kuishi na binadamu waifugwe, ni kama vile sasa hivi ukija ukaenda Thailand, ukienda India, hawa tembo wanavalishwa mpaka mashada, wanatembea barabarani na ndio maana utalii wao umekuwa kwa sababu ya jambo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda India, nyani, tembo wanavishwa mashada, sasa sisi inakuwaje ng'ombe wanaenda kwao, linakuwa ni tatizo, kwa sababu hawa ng'ombe walitoka porini wakaja kuishi na binadamu, ni sawasawa na nyumbu akichukuliwa anakuja kuishi na binadamun wakapata mafunzon wanakuwa ni jamii katika sehemu yetu.

Sasa ifikie, sheria wanazozitunga za kuwazuia wananchi kuingia katika maeneo hayo na wao watunge sheria hao wanyama wasije katika maeneo yetu, tuwe *balanced*, vinginevyo kwamba ng'ombe akipita hata barabarani amekosea mchungaji amesinzia, linakuwa ni tatizo... (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tabasamu.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Ndio.

NAIBU SPIKA: Sheria ni kwa ajili ya binadamu, sio kwa mnyama. (*Makofi*)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini hawa...

NAIBU SPIKA: Subiri kwanza Mheshimiwa. Kama ulivyosema, vizuri mwenyewe kwamba hana huo uelewa.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Ndio.

NAIBU SPIKA: Hawezi kutungiwa sheria kwa ajili yake yeye mnyama, yaani kwamba mnyama akivuka hapa atafanywa hivi, sheria ni kwa ajili ya binadamu, kwa ajili ya mahusiano ya binadamu. (*Makofi*)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Sasa hawa ng'ombe wametungiwaje sheria sasa wakivuka mipaka tayari sisi inakuwa ni tatizo kwetu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mimi najaribu kukuweka vizuri kwa sababu ukisema wameenda kwao, basi maliasili wapo sahihi kuwazuia wale ng'ombe wabaki kule. Najaribu kukuweka vizuri ili mchango wako uupeleke kule unakotaka uende. Ukisema ng'ombe wamerudi kwao kwa namna hiyo, maana yake Maliasili wapo sahihi kuwazuia wale ng'ombe kutoka tena, maana si wamerudi kwao, kwa mchango wako yaani, ndio unamaanisha hivyo.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa...

NAIBU SPIKA: Sasa sijui kama ndio lengo lako, maana yake binadamu hawezi kwenda kumchukua tembo akaja naye nyumbani. Kwa hiyo hata hawa ng'ombe wakishaenda kule wabaki huko, si ndio kwao wamesharudi. Ndio mchango wako unachomaanisha ndio maana nakuongoza vizuri uende kule ulikotaka kusema. Ukisema wamerudi kwao

maana yake Maliasili wapo sahihi kuwazuia, maana unafuata wa nini wakati wapo nyumbani. (*Makof*)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa uelewa huo, lakini ninachotaka kukwambia ni kwamba wale ng'ombe ni hayawani, hii sheria wanatakiwa watungiwe binadamu sio ng'ombe. Kwa hiyo anayetakiwa kukamatwa pale ni binadamu ndio akapigwa faini sio ng'ombe. Sasa hawa watu wa *TAWA*, watu wa Maliasili ninachotaka kuwaomba sana wakae tuje na mjadala wa kitaifa tukae watu wa Sheria na Katiba, watu wa Wanyamapor, watu wa Wizara ya Ardhi na sisi Wafugaji, kwa sababu hapa Wabunge sisi hapa Wabunge wote hakuna Mbunge anayetoka kwenye jimbo lake hakuna mifugo na hakuna Mbunge anayetoka katika jimbo lake ambapo hakuna eneo la *game reserve* au *forest reserve*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati sheria hizi zinatungwa za kuweka haya maeneo ya *forest reserve* na *game reserve*, wakati huo nchi yetu ilikuwa na watu milioni kumi na mbili na hawa watu milioni kumi na mbili mwaka 1960 ni taarifa zilizopikwa, kwa sababu wakati huo kulikuwa hakuna simu, hakuna barabara, hakuna chochote, walipataje orodha ya watu kwamba Tanzania kuna watu milioni kumi na mbili na yalikuwa ni mapori. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hatua hiyo, sasa hivi nchi yetu, nchi haikui, ipo palepale ila wananchi wanaongezeka katika nchi yao na wanyama wanaongezeka, tuje na mjadala wa kitaifa kwa ajili ya hili jambo. Leo mifugo yetu, ukiichukua idadi ya mifugo iliyokuwepo mwaka 1960 na mifugo iliyopo leo vitu haviendani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupa mfano Geita Mjini kuna eneo la *game reserve* la kilometra mbili, inawezekana wapi na Geita ni Manispaa? Kuna Kwimba mita mia 600 kutoka Ngudu Mjini unaambiwa kwamba ni *game reserve*, mita 600, haviwezekani vitu kama hivyo na hiyo ukiangalia

ramani ni ya mwaka 1953. Sasa leo tunajitawala, hatuwezi hata sisi wenyewe kutengeneza ramani zetu, tunatumia ramani za Mwingereza, ramani za Mjerumanii! Waheshimiwa Wabunge hili ni jambo ambalo tuiombe Serikali, tupitie haya maeneo yote ziletwi hizi sheria, afadhalii hii Burigi tumeisikia ni ya mwaka jana, sijui hii *Selous* ilikuwa ni mwaka gani, na hii Serengeti ilikuwa ni mwaka gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa hatua hii, hii mipaka imeingiliana na tunaomba mjadala wa kitaifa twende tukaokoe wafugaji wetu. Hawa ng'ombe wataisha kwa kupigwa risasi huko na hawa ndugu zetu. Bahati mbaya sana wanaowapiga risasi ni watoto wa wafugaji, watoto wa wakulima, tunawashangaa sisi hawa watoto wa maskini wenzetu wanaenda kututia umaskini wazazi wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwangu lingine nataka kuishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, watengeneze Zoo za kila Makao Makuu ya Mikoa, wasitegemee watalii kutoka nije, leo kuna ugonjwa wa *Covid*, sasa hivi hatupati watalii, tungekuwa tuna watalii wa ndani hapa hapa, Jumapili hii leo mimi nilikuwa naweza kwenda Kongwa na familia yangu tukaangalie wanyama.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kengele imeshagonga Mheshimiwa Tabasam

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nawapongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Naibu wake,

Mheshimiwa Mary Masanja, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Allan Kijazi, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na muhimu wanayofanya ya kusimamia maliasili yetu kwa manufaa ya kizazi cha leo na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja kwa kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni ushauri kwa Serikali kuhusu haja ya kuinusuru Tasnia ya Uwindaji wa Kitalii katika Taifa letu. Tasnia hii ni moja ya vyanzo vyta mapato kwa Taifa letu ambayo kwa muda wa miaka 10 sasa imekuwa katika hali tete na inaendelea kushuka zaidi hasa katika kipindi hiki cha janga la ugonjwa wa *Corona*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na takwimu za Chama cha Wawindaji wa Kitalii (*Tanzania Hunting Operations Association - TAHOA*), idadi ya watalii wa uwindaji wanaokuja nchini kwetu imekuwa ikishuka kwa kasi sana. Idadi imepungua kutoka wawindaji 1,503 mwaka 2010 hadi 519 mwaka 2019. Mapato nayo yameshuka kutoka Dola za Kimarekani milioni 23.5 mwaka 2010 hadi kufikia Dola milioni 11.5 mwaka 2018, sambamba na kushuka kwa umiliki wa vitalu vyta uwindaji kwa asilimia 51 kutoka vitalu 157 mwaka 2010 hadi 87 tu ambavyo ndivyo vyenye wawekezaji kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamiliki waliviacha vitalu vyao kwa hiari tangu mwaka 2018 kwa sababu ya kushuka sana kwa faida na ongezeko kubwa la gharama ya ada na kodi wanazotozwa na Serikali, jambo ambalo linalifanya Soko la Tanzania la biashara ya Utalii wa Uwindaji kuwa la bei ya juu zaidi kuliko washindani wetu Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimbabwe kwa mfano, hupokea wastani wa wawindaji wa kitalii 800 japo wao wana vitalu 16 tu vyta Serikali ikilinganishwa na Tanzania yenye zaidi ya vitalu 150. Zambia ambayo ina vitalu 26 tu, kulingana na takwimu za mwaka 2019, ilipokea wawindaji 446

ikilinganishwa na Tanzania ambayo ilipokea wawindaji 541 tu kwenye vitalu vyake 76, na zilizobaki hazikupata wawindaji kabisa. Afrika ya Kusini wao hupokea wastani wa wawindaji 9,000 kwa mwaka ikifuatiwa na Namibia ambayo hupokea watalii wa uwindaji 8,000 kwa mwaka licha ya kuwa maeneo yao ya uwindaji ni machache ukilinganisha na idadi na maeneo tuliyonayo sisi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya tozo zinazolalamikiwa sana na *TAHOA* kwamba imechangia kuongezeka kwa gharama ya utalii wa uwindaji ni Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) ya asilimia 18 kwenye mauzo yao yote ambayo ilianza kutozwa mwaka 2016; na kufikia mwezi Machi mwaka 2020, pigo kubwa zaidi liliikumba tasnia ya uwindaji baada ya asilimia 80 hadi 100 ya watalii kuahirisha safari zao kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa *corona*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kufuatia kushuka kwa biashara ya utalii wa uwindaji, nashauri, Serikali iridhie mambo mawili muhimu ambayo yasipozingatiwa, tasnia hii itazidi kuathirika sambamba na kushuka kwa mapato yanayotokana na utalii wa uwindaji pamoja na ulinzi na uhifadhi wa maliasili yetu katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba *VAT* irejeshwe kwenye mfumo wa ugawaji kama ilivyokuwa kabla ya mwaka 2016. Kulingana na taarifa za *TAHOA*, tangu *VAT* ianze kutozwa kwa kiwango cha asilimia 100 ya pato lao, Tanzania imeshindwa kushindana na nchi nyingine za Afrika zenyetunzwa kama Zimbabwe, Zambia, Msumbiji, Namibia, Afrika ya Kusini, Botswana, Uganda, Ethiopia, Cameroon, Jamhuri ya Afrika ya Kat, Gabon na Benin. Nchi hizi wao hutoza *VAT* ya kati ya asilimia 10 hadi 18, lakini ni kwa baadhi ya bidhaa tu kama vyakula, malazi na ada ya uwindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mwaka 2016, *TAHOA* ilikuwa inalipa *VAT* kwenye vyakula na malazi tu na hizi zilikuwa zinahesabiwa kama asilimia 10 ya ada za safari na asilimia 90 iliobaki ilikuwa haihesabiwi ama ilipewa

msamaha, kwa sababu *TAHOA* walikuwa wanatambulika kama wauzaji wa nje (*exporters*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli *TAHOA* ni *exporters* kwa sababu hakuna mtalii wa uwindaji atakayekuja Tanzania kuwinda kama hatasafirishiwa nyara zake kwenda nchi aliyotoka aweze kwenda kufurahia. Hata Kimataifa, uwindaji wa kitalii unatambulika kama *export industry*, na hata Tanzania tuliitambua hivyo mpaka mwaka 2016 VAT ilipoanza kutozwa kwa asilimia 100 ya mauzo na mapato ya makampuni ya uwindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wetu wa Tasnia ya Utalii wa Uwindaji wanailalamikia Serikali kuwa pamoja na kulipia VAT kwenye mapato yao yote, kampuni hizi pia zinawajibika kubeba gharama kubwa za kudhibiti ujangili, kuendeleza vitalu, kuchangia miradi ya maendeleo ya jamii, kulipa ada za mwaka za vitalu (*Block Fees*), mambo yote ambayo yanawapunguzia kwa kiwango kikubwa faida wanayopata na wakati mwingine hujikuta zikijidesha kwa hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kutokana na kudorora kwa utalii wa uwindaji, nashauri Serikali isamehe kampuni za utalii wa uwindaji kwa muda au kupunguziwa Ada ya Vitalu vya Uwindaji. Kwa sasa, kwa mwaka kitalu cha uwindaji hulipiwa Dola za Kimarekani 60,000 kwa vitalu vya daraja la kwanza, *USD* 30,000 kwa vitalu vya daraja la pili, na *USD* 18,000 kwa vitalu vya daraja la tatu. Katika kipindi hiki cha janga la *Corona*, wenye vitalu wengi wanashindwa kulipia ada ya vitalu kutokana na kukosekana kwa wateja wa uwindaji. Kwa hiyo, kutokana na hali hii, makampuni ya uwindaji wanashindwa pia kufanya doria na ulinzi wa wanyamaporii kudhibiti ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2020, hadi tarehe ya mwisho kulipia ada ya vitalu, ni vitalu 64 tu ndivyo vilivyolipiwa na vitalu 48 hawakuweza kulipia kwa wakati hata baada ya kuongezewa muda wa ziada wa siku 30. Hii inaonyesha hali ilivyo tete kwa sasa katika tasnia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri ili kuinusuru tasnia hii yenye faida kiuchumi na kiuhifadhi, Serikali ifanye mapitio ya sera kuhusiana na tasnia hii na kufanya mabadiliko muhimu ili kuzidi kuboresha mazingira yake ya uwekezaji. Kuna haja ya kufanya marekebisho kwenye viwango vyta kodi na ada ya vitalu, pamoja na tozo mbalimbali ikiwemo VAT ya asilimia 18 kwenye huduma na mauzo yote ili kuchochea ukuaji na uwekezaji katika tasnia ya uwindaji na hivyo kuongeza mapato kuitia kuongezeka kwa watalii watakaovutiwa na pungozo la bei kuja kuwinda nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya mapato yanayotokana na uwindaji hayatokani na ada ya vitalu kwani huchangia asilimia 15-20% tu na asilimia 80 - 85 hutokana na ada za nyara pamoja na ada za leseni. Hivyo naishauri Serikali ipunguze kodii ya vitalu ili kampuni ziweze kumudu kupunguza bei kwa wateja wao na hivyo kuvutia idadi kubwa zaidi ya watalii wa uwindaji. Kwa njia hiyo, wataweza kuinua mapato yanayotokana na tasnia hii ambayo kwa sasa yameshuka kwa zaidi ya asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni ushauri kwa Serikali kuhusu kufuta pendekezo la kutaka kuanzisha Pori la Akiba katika Wilaya ya Longido Ukanda wa Ziwa Natron.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu na wewe mwenyewe kuhusu mchakato wa Wizara ya Maliasili ulioanzishwa mapema mwaka 2020 wa kutaka kuanzisha Pori la Akiba katika maeneo ya viji ya wafugaji wa wilaya ya Longido na ambayo wao wenyewe wameyatenga na kuyahifadhi mahususi kwa ajili ya malisho ya akiba kwa mifugo yao misimu ya kiangazi na nyakati za majanga ya ukame ambayo hutokea mara kwa mara katika wilaya yetu ya Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na hali ya kijigrafia na maisha ya wakazi wa Wilaya ya Longido ambao kwa asilimia 95 ni wafugaji, kutakuwa na athari kubwa sana

kijamii na kiuchumi endapo Pori la Akiba liliopendekezwa litaanzishwa katika maeneo ya malisho ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, naomba niishauri Serikali yetu sikuvi ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mama yetu jasiri, mpendwa wetu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, isitishe mchakato huu kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ya wafugaji wanaoishi katika eneo husika wanatunza mazingira na tayari eneo hilo ni Pori Tengefu (*Game Control Area - GCA*) na linatumika kwa uwindaji wa kitalii tangu miaka ya 1950. Sambamba na shughuli ya ufgaji kwa Jamii ya Kimasai ambayo ndiyo wakazi Wakuu wa Wilaya ya Longido, kuna azma ya Serikali yetu kuongeza maeneo ya wafugaji na siyo kuyapunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo liliopendekezwa la Ukanda wa Ziwa Natron, milima ya Gelao, Ketumbeine, Matale na nyanda za malisho ya vijiji zaidi ya 17 za Tarafa ya Ketumbeine na Engarenaibor ambazo zitamezwa na Pori hilo la Akiba, linategemewa sana na wafugaji ambao ni asilimia 95 ya wakazi wa Longido na mifugo ndiyo njia kuu ya uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kufanya eneo husika Pori la Akiba litaleta mgogoro kati ya wananchi na hifadhi na itaongeza migogoro ndani ya Wilaya ya Longido na maeneo ya jirani Wilayani Ngorongoro ambako tayari hali ya uhifadhi na jamii imekuwa tete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wake, walizirudishia zaidi ya vijiji 900 ardhi ya hifadhi ili wananchi wapate maeneo ya kuishi na kufanya shughuli za kiuchumi; na kwa Vijiji vya Wilaya ya Longido, hazikuwa kwenye orodha yoyote ya vijiji vyenye mgogoro na hifadhi. Hivyo, siyo vizuri sasa kuongeza tena eneo la hifadhi kwa wananchi ambao

tayari wanaishi vizuri na wanyamapor na bila kuwa na migogoro na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la Akiba linalopendekezwa litaathiri viji 19 vya Tarafa ya Ketumbeine; Viji 11 vya Tarafa ya Engarenibor na Kijiji kimoja cha Kiserian katika Tarafa ya Longido. Hili ni eneo lenye zaidi ya watu 90,000. Vilevile Pori hilo litaathiri baadhi ya viji vya Wilaya ya Ngorongoro na ikizingatiwa kuwa eneo la Ngorongoro tayari kwa sehemu kubwa ni hifadhi na hivyo ikifanyika hivi wananchi hawatakuwa na mahali pa kuishi na kufuga; hivyo kuongeza migogoro katika wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Longido tuna kiwanda kikubwa na cha kisasa chenye uwezo wa kuchakata nyama ya mifugo zaidi ya ng'ombe 1,000 kwa siku, mbuzi na kondoo 4,000 kwa siku; na hivyo eneo kubwa zaldi ya hili tulilonalo kwa sasa linahitajika kwa ajili ya kufuga na kunenepesha mifugo yetu kwa ajili ya viwanda vyetu vya ndani. Hivyo pendekezo la kumegua sehemu ya ardhi ya Longido haliendani na azma ya Serikali ya kuongeza maeneo ya malisho ili kuinua sekta ya mifugo na kukuza uchumi unaotokana na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya kwanza ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa Bunge letu ya tarehe 22 Aprili, 2021 Dodoma, alikazia dira ya Taifa letu la kuendelea kuongeza maeneo ya ufugaji. Wilaya ya Longido ni moja ya wilaya kame sana nchini na ambayo hukabiliwa na majanga ya ukame mara kwa mara, hivyo milima inayotaka kutwaliwa pamoja na eneo la nyanda za Ziwa Natron ndiyo huwa kimbilio la kupatia malisho na maji wakati wa majanga ya ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii katika ngazi zote (Kijiji, Kata kuititia *WDC*, Halmashauri ya Wilaya kuititia Baraza la Madiwani, wala *DCC* na *RCC*) hawakuwahi kushirikishwa katika mchakato wa pendekezo la kuanzishwa kwa Pori hili ili kupata mawazo yao. Hivyo jambo hili siyo shirikishi. Pori linaloonekana kama liko wazi kwa wageni ni maeneo ya asili

ya wafugaji waliyopangilia matumizi ya malisho na maji kwa misimu tofauti ya mwaka ili kutunza ekolojia na upatikanaji wa malisho bora ya mifugo kwa majira ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya milimani ndiyo hunusuru mifugo kwa malisho na maji wakati wa kiangazi na nyanda za chini hufaa nyakati za mvua na masika tu kutokana na ukosefu wa vyanzo vya maji misimu ya kiangazi katika Wilaya ya Longido. Hivyo kuyatwaa maeneo hayo ni sawa na kuwaangamiza wafugaji wa Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naomba Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii isikilize kilio cha wananchi wa Jimbo langu la Longido na ichukue hatua sahihi bila kusita kusitisha na kulifutilia mbali pendelezo la kutaka kutwaa eneo hili la wafugaji na kulifanya kuwa Pori la Akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na ahsante kwa kupokea mchango wangu.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro; Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary F. Masanja na wataalamu wa Wizara na wadau wa maendeleo kwa mchango mkubwa sana kwenye Sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye suala la *Half Mile* na umuhimu wa kufungua njia mpya za kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia maeneo ya kata za mpakani za Uru na *Old Moshi*; na uwepo wa mti mrefu kuliko yote Afrika katika Kijiji cha Tema Kata ya Mbokomu, Jimbo la Moshi Vijijini. Huu ni mti wenye miaka mingi zaidi duniani. Una miaka 600. Pia nitachangia kuhusiana na ongezeko la watu na wanyama wa kufuga linavyotishia hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Half Mile* ni eneo lenye upana wa kati ya 0.5 -0.8 ya *mile*. Eneo hili lilikuwa linatenganisha Mlima Kilimanjaro na makazi ya watu. Eneo

hili kwa upande wa Majimbo ya Moshi Vijijini na Vunjo linajumuisha vijiji 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia inaeleza kwamba watu walianzisha makazi katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro takribani zaidi ya miaka 2000 iliyopita. Pamoja na wachaga kuwepo kwenye makazi yao miaka niliyotaja hapo juu, Mkoa wa Kilimanjaro una historia ngumu inayohusisha uhifadhi wa Mlima Kilimanjaro na umiliki wa rasilimali ya ardhi ambavyo walivirithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1921, wakoloni walipitisha Sheria ya Kuhifadhi Viumbe wa Porini (*Wildlife Conservation*) ambapo misitu ya Kilimanjaro iliusika. Sheria hii iliwayima haki wenyeji wa Kilimanjaro wasiingie msituni. Aliyeingia alionekana mharibifu na mhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1922, Sera za Ukoloni zilimpa nguvu Gavana kuwa mmiliki wa ardhi yote. Mwaka wa 1923 wakoloni walianzisha programu ya kuwanyang'anya wananchi kwenye ardhi yao yenye rutuba na kuanzisha mashamba ya Masetla ya Wazungu. Mashamba haya yalitaifishwa kwa Azimia la Arusha la Mwaka 1967, na bado hayako mkononi mwa wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, Wakoloni walitumia sheria kandamizi kujimilikisha ardhi ya wana Kilimanjaro na rasilimali za msitu wa Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sheria ya *Wildlife Conservation* ya 1921 na ile ya kuwanyang'anya mashamba ya 1923, wakoloni waliingiwa na huruma na kuanzisha Sheria ya *Half Mile Strip* mwaka wa 1941 kwa lengo la kuwapatia majirani wa Msitu Kilimanjaro huduma za mazao ya misitu kama vile dawa za asili (ngesi), mboga za majani (mnafu) miti ya kujenga nyumba, kuni na majani ya ngombe. Kiuhalsia, eneo hili liko kwenye *Forest Reserve* na siyo kwenye *National Park*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na malengo ya kuanzishwa kwa eneo la *Half Mile*, tokea enzi za ukoloni, kazi za kibinaadamu zilisababisha uharibifu wa mazingira katika *Half Mile* na yale maeneo ya hifadhi kwa kukata miti, kupasua mbao, kuchoma misitu, kuchunga mifugo na kuendesha shughuli za kilimo ndani ya hifadhi. Hii ilitokana na kukosekana kwa usimamizi mahiri kutoka katika mamlaka husika Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uharibifu huu, Serikali ilisimamisha vijiji vyote 40 kutokutumia *Half Mile Strip* tokea 2004, kwa sheria iliyoanza kutumika 2005. Hii ilitokana kusainiwa kwa sheria ya kuziingiza *Half Mile Strip* za maeneo ya Moshi Vijijini na Rombo iliyotiwa sahihi na Marehemu Rais Mkapa 18/7/2005 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 16/9/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya zuio hili, Serikali yetu iliondoa ile huruma ya Wakoloni kwa Wana Kilimanjaro ya kutumia ile *Buffer Zone* ya *Half Mile*. Siku hizi hakuna cha *Half Mile* tena na ukikamatwa na maaskari wa *KINAPA* utakuwa na bahati mbaya sana. Wapiga kura wangu wameniambia kuwa wengi wamepigwa na wameambulia vilema, wamebakwa, na wengi wamedhalilishwa kwa namna mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kunyima watu matumizi ya *Half Mile*, hii imesababisha umasikini mkubwa, ikiwa ni pamoja na wanyama waharibifu (*needed*; kama, nyani, Tembo) kuingia kwenye mashamba ya wanakijiji na kuharibu mazao. Kabla ya mwaka 2005, shughuli za wananchi kwenye *Half Mile* zilizuia wanyama kuingia vijiji vya mpakani na ilikuwa hakuna uharibifu wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu wa Rais Dkt. Ali Mohammed Shein alipotembelea Mkoa wa Kilimanjaro mwaka 2008 akiambatana na Waziri wa Maliasili Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe wananchi walimweleza matatizo yaliyojitekeza baada ya Serikali kuunganisha eneo la hifadhi la *KINAPA* na misitu ya hifadhi za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ziara hiyo, Wizara ilikaa na kuiagiza *TANAPA* (kwa barua Kumb Na. *CAB*. 315/484/01/A ya tarehe 22/1/2008 ya Waziri, Mheshimiwa Prof. Maghembe kwenda kwa Mwenyekiti wa Bodi ya *TANAPA*, na barua kumb na CJA.246/374/01/42 ya tarehe 27/2/2009 ya Katibu Mkuu Dkt. Ladislaus Komba kwenda kwa Mkurugenzi wa *TANAPA*) wachore ramani upya na kutenga eneo la nusu mile liwe nje ya Hifadhi ya *KINAPA* kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelekezo hayo hapo juu na kukumbushwa mara kwa mara na wadau wa maendeleo wa mlima Kilimanjaro, hadi leo ramani hiyo haijatoka na sheria hii kandamizi kwa wananchi wa vijiji 40 vya mpaka na mlima Kilimanjaro bado inawanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria kandamizi kama hii siyo nzuri na zinasababisha migogoro isiyo ya lazima baina ya wananchi na Serikali yao. Kama mwakilishi wa wananchi, hata mimi naikataa kabisa sheria kandamizi kwa wapiga kura wangu. Namwomba Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan aliangalie jambo hili kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wetu ambaye ni msikivu sana afuatilie pale wenzake walipoachia ili haki itendeke. Wana Moshi Vijijini, Vunjo na Rombo tunaomba maeneo yote ya vijiji vya mpakani vipewe fursa ya kuulinda na kuutunza mlima wao kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ikibadilishwa, *Half Mile Strip* inaweza kutumika kwa mafanikio makubwa chini ya usimamizi wa Serikali Kuu, Serikali ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji na kusaidia wananchi wa vijiji husika:-

- (a) Kuutunza mlima;
- (b) Kuwapatia wananchi huduma;

(c) Kuinua uchumi wa wananchi, Wilaya, Mkoa na Taifa; na

(d) Kukuza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ikibadilishwa, tunatarajia kupanda miti ya muda mfupi kama *Cyprus, Pine*, Mikaratusi na aina nyinginezo zinazokua haraka kwa ajili ya nguzo za umeme, nguzo za ujenzi wa nyumba zikiwemo ghorofa. Miradi kama hii iko Iringa. Rais akiruhusu hili, nchi nzima itanufaika kwani Kilimanjaro ina miundombinu bora ya kusafirisha hizi bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni ule wa kuiomba Wizara ifanye utafiti na kufungua njia mpya za kupanda Mlima Kilimanjaro kuititia kata za mpakani huko Uru na *Old Moshi*. Njia hizi zinaweza kuwa fupi, na baadhi ya watalii wanaweza kuzifurahia sana. Kwa kufanya hivyo, tutaongeza uwekezaji kwenye maeneo haya, ajira na mzunguko wa pesa utaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu ni kuhusu mti mrefu Afrika. Wagunduzi kutoka Chuo Kikuu cha Beyreuth Ujerumani wakiongozwa na Dkt. Andrew Hemp wamegundua kwamba mti mrefu (81.5m) kuliko yote Afrika uko katika Kijiji cha Tema, Kata ya Mbokomu, Jimbo la Moshi Vijijini. Mti huo unaitwa *Entandrophragma Excelsum* (Mkusu). Inasemekana kuwa mti huo ndiyo ulio na miaka mingi zaidi duniani (*600 years*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, watafiti wa Kijerumani wameshauri kuwa mti huo unaweza kuishi zaidi kama utatunzwa na kuhifadhiwa vizuri. Ninaiomba Serikali iboreshe uhifadhi wa mti huu na kuboresha miundombinu ya barabara kuufikia, kwani hiki ni kivutio kipyaa cha utalii ndani na nje ya Tanzania. Barabara ya kwenda eneo hili ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa nne ni kuhusu hatari inayoikabili Hifadhi ya Ngorongoro. Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro lilianza mwaka 1959 likiwa na wakazi

8,000. Ripoti inaonyesha kwamba sasa hivi kuna wakazi zaidi ya 100,000 na ongezeko kubwa la mifugo kama ngombe, mbuzi na kondoo katika eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za uhifadhi kule Ngorongoro zimekuwa ngumu kutokana na migogoro baina ya binadamu wanaoishi eneo la hifadhi na wanyamapori. Wanyamapori huvamia maboma ya wfugaji na kula wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo. Vilevile kuna baadhi ya wananchi wanaolima katika eneo la hifadhi. Hii imesababisha eneo hili kushambuliwa na magugu vamizi na kuishia kupunguza eneo la malisho kwa wanyamapori na wale wa kufugwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha mifugo kimeongezeka sana na hii imesababisha kuongezeka kwa magonjwa ya kuambukiza toka kwenye wanyama wanaofugwa kwenda kwa wanyamapori na kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa wanaofugwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatua stahiki hazitachukuliwa mapema, hali itakuwa tete sana miaka michache ijayo. Naishauri Serikali ichukue hatua stahiki kwa kuirekebisha Sheria ya Kuanzisha Hifadhi ya Ngorongoro. Maboresho ya sheria yalenge kulinda wanyamapori, kwani Ngorongoro ni mahsus kwa wanyamapori. Wakazi na wanyama wa kufugwa waondolewe eneo la hifadhi na wapelekwe kwenye maeneo yao ambayo yako ya kutosha nje ya eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri ya bajeti na kazi nzuri inayotekelze wa na Wizara. Ukiondoa kipindi hiki ambapo dunia nzima imeathiriwa na *Covid 19*, sekta hii ni katika sekta zinazofanya kazi nzuri sana Tanzania. Hongera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera kuna mapori matano yaliyopandishwa hadhi na kuwa Hifadhi za Taifa za Burigi - Chato, Ibanda -Kyerwa na Rumanyika - Karagwe. Hifadhi hizi ni mpya, bado zinahitaji uwekezaji mkubwa ili kuweza kufikia lengo lililokusudiwa ya kuimarissha sekta hii na kuongeza pato la Taifa. Hivyo ili kuchochaea ukuaji huu katika Hifadhi Mkoani Kagera napendekeza:-

- (1) Tuletewe wanyama wengi zaidi ili waongezeka, wazaliane hifadhi zivutie watalii;
- (2) Hifadhi hizi zijengewe miundombinu ya barabara na mageti yaongezwe, ili zipitike wakati wote;
- (3) Tujenge Hoteli nzuri, makambi na *Lodge* za kudumu.
- (4) Hifadhi zilipoanzishwa vijiji jirani hawakupatiwa elimu ya kutosha. Napendekeza viongozi na wanavijiji wapewe elimu ya Uhifadhi, Ulinzi shirikishi, ni faida gani wao watazipata kutokana na hifadhi hizi wa mkoani Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la wanyamapori kama tembo, ngedere kuingia kwenye maeneo ya wananchi, wanaharibu mazao na kuua wanadamu. Wakulima wanapata hasara na vifo vinatokea mara kwa mara. Serikali ifanye yafuatayo: watafute njia ya kuzuia tembo kuingia katika maeneo ya wakulima ya kudumu; tutumie *technologies* za kilo kuwaondoa tembo hawa; wanyama waharibifu kama ngedele nyani wamezaliana sana, ni wengi vijiji, wanaharibu sana mazao ya wakulima. Napendekeza wavunwe, wapunguzwe ili kupunguza hizi athari. Tufufue kitengo cha *Vermin Control Unit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vyatia na vyakifuta machozi ni vyatia siku nyingi, ni vidogo sana, havina uhalisia, virekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya utalii ni sekta ya kipaumbele ya Serikali mbayo inachangia kwa kiasi kikubwa

pato la Taifa. Sekta hii imeathiriwa sana na Covid 19. Serikali ichukue hatua za haraka kunusuru sekta hii. Tunaiomba Serikali ianzishe *Stimulus Package* ili kunusuru haraka sekta hii. Serikali itoe fedha kuwasaidia wafanyabiashara wenye hoteli, wasafirishaji na Wizara ili kunususuru sekta hii haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, kama nchi tuwe na Mfuko wa Dharura kuweza kutatua matatizo kama haya yakijitokeza. Mfuko uwe wa Kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iwe na mipango kabambe ya kuchochea utalii wa ndani. Kutoka viwandani, mashulen, wakulima, wavuvi, watumishi na kadhalika, wote wahamasishwe na kuwekewa utaratibu ili washiriki. Itasaidia kuongeza namba ya watalii nchini na pato la Taifa.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Simiyu una mito miwili muhimu sana. Mito hiyo ni Mto Simiyu na Mto Duma. Kwa miaka ya hivi karibuni mito hiyo imekuwa inakauka muda mfupi tu baada ya mvua za masika kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa, miti mingi imekatwa ili kutengeneza mkaa na kuni kwa ajili ya kupikia na hii ni kwa sababu hakuna chanzo kingine cha nishati. Imefika hatua akina mama wanatumia kinyesi kupikia, kitu ambacho kinasababisha macho yao kuwa mekundu. Hii ni sababu ya lawama na kusingiziwa ni wachawi na hatimaye kuuawa kwa kukatwa na mapanga.

Je, Serikali ina mpango gani mahususi na wa dharula ili kuleta nishati mbadala na wenye gharama nafuu ili kuwanusuru akina mama wenzetu wa Mkoa wa Simiyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii wengi wanatokea Arusha kuelekea Serengeti, lakini sisi Mkoa wa Simiyu hatuna barabara wala mlango wa kuingilia Hifadhi ya Serengeti. Je, ni lini sasa barabara hiyo itajengwa ili wananchi wa Mkoa

wa Simiyu nao wapate fursa ya kuitumia hifadhi ya Serengeti na kufurahia urithi wa Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Simiyu miradi ya barabara hatuioni na wakati kuna Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Pori la Akiba la Maswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao yatokananyo na nyuki yana mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu, pia kuna nchi hapa Afrika, kwa mfano Ethiopia, mazao ya nyuki yana mchango mkubwa sana katika *GDP*. Tanzania ina mazingira mazuri sana kwa ufugaji wa nyuki kwa mfano Mikoa ya Katavi, Rukwa, Tabora na Kigoma pamoja na Singida, lakini hata hivyo sioni mpango mkakati wa kuliendeleza jambo hilo. Vilevile hakuna watalaam wa nyuki kwa sababu hata chuo kilichopo Tabora ni kidogo utadhani ni chuo cha mtu binafsi. Tunaomba chuo hicho kiongezewe miundombinu ili kiongeze udahili. Serikali iendelee kuchukua hutua madhubuti ya kuwezesha chuo hiki na kutengeneza ajira kwa vijana na kuliwezesha zao hili kuongoza Kimataifa.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia nzima inatafuta ahueni kwenye sekta ya utalii katika kipindi hiki cha *Corona*, lakini Tanzania tunaongeza tozo mfano kuanzia Julai, 2021 *Park Fees* zitaongezeka kwa *10 USD* kwa Serengeti na Nyerere kipindi cha *high season* wakati Kenya, Uganda na Rwanda wamepunguza. *TANAPA* pia pamoja na uwekezaji ndani ya hifadhi kulipiwa *Concession fee* ya *50 USD* bado wanaanzisha *Land Base Rent* ya *2000 USD* kwa *Seasonal Camps*, *Permanent Tented Camps* *20,000 USD* na *Lodges* *50,000 USD*. Suala hili linaongeza gharama za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* wana hifadhi 22 ila hifadhi zinazoweza kujidesha ni hifadhi zisizozidi tano na ndiyo maana kila mara wanaongeza tozo na kuongeza mzigo kwa hifadhi kama Serengeti, Nyerere na *KINAPA*. Nashauri tozo hizi zisitishwe hadi Julai, 2022 ili kutoa ahueni kwenye sekta ya utalii kipindi cha *corona*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo kama ukikodisha gari ya utalii kwa kampuni nydingine pamoja na kulipa *TRA* pia inabidi ulipe *50 USD* Wizara ya Maliasili na Utalii. Hii ni kuongeza gharama za kufanya biashara Tanzania. Nashauri tozo hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TDL*, fedha hizi nashauri ziwekwe kwenye akaunti maalum na zifanye kazi iliyokusudiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kupima *Corona* ni kubwa nchini Tanzania ambayo ni *100 USD* wakati Kenya ni *30 USD* Serikalini na *50 USD* kwa Hospital binafsi. Gharama hizi ziangaliwe upya. *Rapid test* kote ni sawa kwa maana ya *25 USD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha ikae na bank na *BOT* ili kuangalia uwezekano wa kutoa ahueni kwa wadau wa utalii ambao walikopeshwa magari ya utalii na kushindwa kulipa kwa sababu ya *Corona* ili deni lao lisogezwe mbele bila *penalty* kama sehemu ya kutoa ahueni kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu kwa Wizara, naomba utalii wa ndani uimarishwe kwa kufanya *promotion* au *ku-promote* utalii wa ndani na hasa kuimarisha *cultural heritages site* zetu. Watalii wa ndani waje waone Makumbusho zetu na maeneo *mentioned* ya urithi wa Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwininge, Serikali sasa ijipange kuhakikisha wanaanzisha *Plantation Museums* ambazo zitasaidia watoto wetu kujifunza.

Tunakoelekea, wanafunzi wa mijini hawatakuwa na sehemu ya kujifunza kwa vitendo na kwa kuona uhalisia wa mazao mbalimbali

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. OTHUMAN HIJA JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hii ni mionganoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha katika Bunge lako Tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza kwa dhati Serikali yetu kwa namna inavyochukua jitihada kubwa ya kuboresha miundombinu katika sehemu za kitalii. Uboreshaji huu utavutia kuja kwa watalii jambo ambalo litaongezea Taifa letu kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii umegawanyika katika sehemu mbili; utalii wa ndani na utalii wa nje. Naipongeza Serikali kwa kuboresha utalii wa nje lakini bado utalii wa ndani haujaka vizuri. Bado bei za kuingilia katika vituo vyetu vya kitalii ni kubwa kwa watalii na wananchi wetu. Wengi wanashindwa kutumia fursa hii ya kuona rasilimali yetu. Ushauri wangu katika suala hili kwa Serikali ni kuweka bei rafiki kwa watalii wetu wa ndani ili nao waweze kufaidi rasilimali za nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyochukuwa jitihada ya upandaji

wa miti. Bado juhudhi hii haijafika katika kiwango cha kuridhisha. Idadi ya ongezeko la mashamba bado ni dogo. Ongezeko kutoka mashamba 23 mpaka 25 ni dogo mno. Ushauri wangu kwa Serikali ni kuongezwa kwa jitihada za makusudi ya kupanda miti ili kuboresha utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kutoa mchango wangu katika bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021 - 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nakushukuru wewe kwa kuongoza kikao hiki kwa uweledi na Ufanisi. Nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Tanzania kwa uongozi wake imara na wenyе matokeo chanya kwa Taifa letu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani na pongezi hizo, nina michango, ushauri na maswali yenyе lengo la kujenga, siyo kubomoa. Naishauri Wizara kushirikiana na Serikali za Mikoa, Wilaya na Mitaa. Lengo kuu ni kushajiisha utalii wa ndani, kwani wananchi wengi hawana uelewa juu ya dhana nzima ya utalii. Hivyo basi, Serikali hizo zitasaidia kushajiisha, kuhamasisha na kuelimisha dhana nzima ya utalii. Pia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ndio Wenyeviti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa sehemu zao. Amani na utulivu ndio kitu muhimu sana kwa ustawi wa utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ni sekta mtambuka, hivyo basi, naishauri Wizara kuendelea kushirikiana na baadhi ya taasisi ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya TAMISEMI, Kilimo na Ardhi, kwani itasaidia kufikisha huduma stahiki kwa watalii wa ndani na wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara kuboresha miundombinu tofauti ikiwemo mawasiliano ya simu, barabara kwa baadhi ya hifadhi sambamba na sehemu za vivutio vya utalii. Kwani ukosefu wa Mawasiliano kutazorotesha uongezekaji wa watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kutokana na janga lililoikabili dunia, *Covid 19*, nashauri Serikali kuboresha utalii wa ndani kwa ushirikiano baina ya SMZ na SMT kwani kuna vivutio vipo Zanzibar ambavyo Tanzania Bara hakuna, pia vipo vivutio Tanzania Bara ambavyo Zanzibar havipo. Tubuni vivutio ziada vya Utalii, mfano ngoma za jadi ili kuhifadhi utamaduni, silka, mila na desturi, kuendeleza miradi kwa kiwango kizuri na kwa muda stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri nilloainisha hapo juu, napenda kutoa pongezi za dhati tena kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. Nimefarajika kuona kunaanzishwa aina tofauti za utalii, ukiwemo utalii wa michezo, utalii wa fukwe na utalii wa meli. Swali langu ni: Je, meli kwa ajili ya utalii huo ipo wapi sasa hivi; na je, ina hadhi ya watalii wa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hamwonni haja ya kuanzisha utalii wa tiba asili? Je, Wizara imejiandaa vipi kukuza utalii wa ndani kwa vitendo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kazi njema kwa maslahi ya uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri yafuatayo: kwanza, kutambua na kutangaza vivutio vya utalii tulivyonavyo kwenye maeneo mbalimbali. Mfano, Wilayani Ukerewe kuna mapango ya

Handebezyo, jiwe linalocheza la Nyaburebeka (Ukara), *beach* ya Rubya na kadhalika, lakini bado havitangazwi kama inavyostahili na hatimaye vililingizie Taifa letu pesa na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuwekeza kwenye miundombinu inayozunguka vivutio vya utalii. Mfano, vivutio nilivyovitaja hapo juu kwa sababu ya kukosa uwekezaji na maeneo haya hayafikiki. Kwa, hiyo nashauri Wizara ishirikiane na Halmashauri kujenga barabara na njia za kufikia vivutio hivi hasa Wilayani Ukerewe ambako vivutio hivi havifikiki.

NAIBU SPIKA: Sasa tunaingia upande wa Mawaziri, tutaanza na Mheshimiwa Wiliam Vangimembe Lukuvi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Masanja na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, mtoa hoja ajiandae.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada nami nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Ndumbaro na Naibu wake na watendaji wote wa sekta ya maliasili kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia na kulinda rasilimali muhimu sana ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema mambo machache mionganoni mwa mengi ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. La kwanza nafikiri nifafanue tena kazi ambayo Serikali imeshafanya, nataka kuwapa tu taarifa Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua mengi ambayo yanasemwaha hapa kwamba idadi ya watu na shughuli zao zinaongezeka na wananchi sasa wamekuwa wengi sana, lakini hifadhi zimebaki vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwakumbusha kwamba Serikali ilishafanya uamuzi na imefanya uamuzi baadhi ya maamuzi ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kutambua hilo Serikali imefuta Mapori Tengefu 12 yenyeye ukubwa wa ekari laki 707,659.4. Haya mapori yalikuwa na *GN* zao yamehifadhiwa kwa mujibu wa sheria na Serikali imechukuwa jukumu la kuyafuta ili yapangwe yaweze kutumika kwa shughuli za binadamu za kilimo na mifugo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji umeshafanyika, Wizara ya Maliasili imeelekezwa na Waziri amesha-*degazette*, yaani ameshayaondowa kwenye orodha ya Mapori Tengefu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, baada ya hapo Serikali imeshafuta, iliagiza misitu yenyeye ekari 46,715, hifadhi saba za misitu ambazo zimekosa sifa kwa sababu ndani yake kuna watu, kuna shughuli za binadamu na nini, hizi nazo zimefutwa, ekari 46,715 za misiti zimefutwa ili wananchi waendeleza shughuli zao za kilimo na mifugo katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maeneo ni yale yaliyokutwa angalau tunasema wavamizi, lakini wananchi wameingia katika maeneo hayo, wameanza kujishugulisha na shughuli mbalimbali za kibinadamu humu ndani. Kwa hiyo Serikali ilishafanya uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, uamuzi mwengine uliofanywa pamoja na kwamba haya yameshakuwa *degazetted*, lakini bado Serikali ikasema hapana tuangalie tena maeneo mengine ya hifadhi za misitu 14 ili tukayapunguze na yenyeewe yatumike kwa shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naweza nikasema haya ni kwamba, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge labda shughuli za kutekeleza haya hamjazona, lakini kama nilivyoahidi mara ya mwanzo kwamba sasa mwaka huu tumeweka bajeti wizara husika ili sasa tushirikiane na wananchi wa maeneo hayo na viongozi wa maeneo hayo,

tuwaonyeshe kabisa, tunaposema hizi ekari laki saba ni zippi na watu gani watanufaika nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema misitu hii ekari 46,000 zimepunguzwa au zimefutwa ni ipi na iko katika maeneo gani. Tunaposema misitu mingine au hifadhi za misitu 14 zitapunguzwa ni maeneo gani, lakini haya naweza nikasema baadhi ya maeneo ya hifadhi ambayo tunatarajia kwenda kuyapunguza mengine yanapatikana katika maeneo ya Uliyankulu, Geita, Rwamgasa, Lwande, Usindankwe, Ushirombo, Mbogwe, Bukombe, Runzewe, Biharamulo, Kahama, Miyeze, Tongwe East, Masanza, Uyui Kigwa Rubuga na Loasi River. Haya ni baadhi ya maeneo ambayo yana hifadhi za misitu ambazo Serikali imefanya uhamuzi lazima hifadhi hizi zipunguzwe ili wananchi waendelee na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi mwengine ni ule ambaao tumekuwa tunausema mara zote kwamba Serikali ililetewa orodha ya kitaifa kwamba vijiji vипatavyo 975 inaelekea ndio vina mgogoro. Ni bahati mbaya sana hii orodha iliandikwa na Wabunge waliopita, lakini na Wakuu wa Mikoa na Wilaya, tutaileta kwenu muione hiyo orodha ya vijiji 975, kila mkoa na kila wilaya pengine ninayoyasema sio vijiji hivi. Kitaifa tulishafanya uhakiki na tukajua ni vijiji 975. Uamuzi wa Serikali ni kwamba vijiji 920 vinabaki na usajili wao lakini kuna kazi ndogo baadhi ya vijiji itafanywa ya kurekebisha mipaka, lakini haitafuta usajili wa vijiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji 55 vilivybaki ndivyo tuliambiwa tuendelee kufanya utafiti, tumeshamaliza kama nilivyowaambia, tunapeleka taarifa kwenye Baraza la Mawaziri na watatupa uamuzi. Kwa hiyo, ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba *concern* yenu na sisi ndio *concern* yetu kama Serikali, nimeongea na mwezangu Waziri wa Maliasili, inaelekea pengine tumefanya uhakiki mara nyangi sana, wahifadhi zetu tunapofanya uhakiki maana yake ni kwamba kila hifadhi imesajiliwa kwa GN namba na mipaka inajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine uhakiki tuliokuwa tunaufanya ulikuwa haushirikishi wananchi, kwa hiyo wapo wananchi ambao hawajui hiyo *GN* iliyoandikwa kwenye karatasi inatafsirika vipi kwenye ardhi.

Kwa hiyo tumekubaliana, pamoja na kwamba tumeshafanya mara nyingi sana tutakuja kufanya uhakiki mpya. Tunayo maandishi hakuna mtu ambaye anania mbaya kwamba ataongezaongeza mipaka nje ya ile mipaka ambayo imetafsiriwa na imeandikwa na imeruhusiwa na *GN*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunazo *GN* tutakuja na mimi ndio *custodian* ambaye ni kama msuluhishi wa mambo haya, nitaunda timu za wataalam wangu ambao wako chini ya Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani, nitatumia *GN* za Maliasili, tutashirikiana na watu wa Maliasili, maana wenzangu ndio wana bajeti, tutafanya mara moja, tutakuja kuhakiki kwa mujibu wa *GN* na tutakapofanya, tutakapofika Uyui, Mbunge wa Uyui tutamwita. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndio *GN* na hii ndio mipaka uthibitishe, leo kuna vifaa ambavyo ukipima hivi kinaweza kikakupa mwelekeo hata kilometra 25 hatutachukuwa muda, tutaunda timu nyingi. Kwa hiyo nataka tu niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge, mengi wamezungumza, inaelekea kwamba wananchi hawajui *exactly* na wala hawajawahi kushirikishwa kujua mpaka wa hifadhi hii umeanzia wapi na umeishia wapi. Hilo tunataka tulifanya safari hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si lazima tufanye kwa hifadhi zote, ningeomba kwa sababu tupo hapa, kila mmoja anayefikiri ana hifadhi ambayo ina mgogoro mkubwa wananchi wanataka kujua mipaka yao imeingia vipi, wakati wa kufanya uhakiki wale vijana wetu wana macho wataona na yaliyopo. Naomba kila mmoja wetu aandike hiyo hifadhi anayofikiri ihakikiwe ampe Waziri. Tukiwa hapa Bungeni maana hatuwezi kufanya zote hata ambazo hazina matatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge yeote anayefikiri wananchi wanamghasighasi sana kujua mipaka imeishia wapi tupeni hiyo hifadhi iko wapi na inaitwa nini, msitu gani hifadhi ya wanyama ipi hata kama ni *national park* mpeni Waziri sisi tukishapa hiyo orodha tutaunda timu, zitaanza kazi mara moja ya kufanya huo uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka nisimame hapa kutoa ufanuzi wa haya ambayo yamezungumzwa sana. Ni kweli wamesema tunafanya kazi pamoja Wizara ya Ardhi, ni kweli Serikali ni moja na haya ninayoyasema tumeshazungumza na Waziri wa sekta na yupo tayari, mnawona alivyokuwa mpole Waziri huyu, msikivu, hana shida na Naibu wake ndio yule, hana shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutayafanya haya mambo waliyoyaomba Waheshimiwa Wabunge. Tukifika tutawashirikisha Viongozi wa Mikoa wa Wilaya na wale vijiji wanaohusika lakini kama Mbunge aliyeleta ile orodha tutamshikisha na atawenza kutusaidia pengine tusihakiki maeneo yote, tukaenda kwenye kona ambayo anafikiri ina mgogoro zaidi katika pori au katika hifadhi inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nichangie hayo ili niwaondolee wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, tumewasikia, maneno yamesikika sana na kila leo yamekuwa yanarudiwarudiwa sana kana kwamba waliofanya uhakiki walifanya usiku au kuna watu wanaendelea kupanua hifadhi mpaka leo. Tutakuja kuhakiki kwa mujibu wa *GN* ambazo zimetangaza hifadhi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Masanja, tutamalizia na mtoa hoja (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na leo tumekutana katika

Bunge lako hili Tukufu. Kipee nikushukuru sana wewe binafsi, kwa kuendelea kulitumikia Bunge hili Tukufu, lakini pia kwa leo kuwa katika uamuzi au ujumuishi maalum wa Sekta yetu hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Wabunge wote waliochangia kwenye sekta yetu hii ya maliasili na utalii na niwapongeze sana kwa kuweza kutupa mawazo chanya ya kuweza kujengwa sekta hii ya maliasili na utalii. Mawazo yao, michango yao na ushauri tumeupokea. Niwaahidi kwamba tunaenda kuufanya kazi kwa nguvu zote, nikishirikiana na Mheshimiwa Waziri na niwaahidi kwamba sisi tuko imara na tumejiandaa kuhakikisha kwamba tunachapa kazi ili tusiwaangushe wao pamoja na wananchi waliotupa dhamana ya kuwaongoza katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuelezea kwenye eneo la maliasili misitu. Jukumu la Sekta ya Maliasili na Utalii kwanza kabisa tunahifadhi maliasili zilizopo nchini, lakini pia tuna malikale, lakini baada ya kuhifadhi tunaendeleza utalii. Kwenye eneo hili la maliasili misitu nitapenda sana kuzungumzia upande wa matumizi ya mkaa na kuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa asilimia 95 ya Watanzania tunatumia nishati ya mkaa na kuni na naomba nilielezee hili kwa ufasaha kabisa kwa kuzingatia Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002, Sura 323 inasema kwamba mkaa ni moja ya mazao ya misitu yanayoruhusiwa kuvunwa kisheria. Naomba hili nilifafanue kwa ufasaha kwamba hakuna Waziri wala mtu ye yeyote ambaye amewahi kuzuia uvunaji wa mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea hivi kulingana na sheria hii, lakini nitapenda kufafanua kwa nini sisi Maliasili na Utalii tunasimamia eneo hili. Tunaomba sana na sheria hii tunaisimamia pale tu ambapo uvunaji wa mkaa unafanywa kiholela. Tunasimamia kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunahifadhi maliasili misitu ili iwe endelevu kwa vizazi na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, kwa kuzingatia kwamba zao hili

linachangia asilimia 3.5 ya *GDP* lakini pia kwa asilimia 43 ya *GDP* inachangia pato ghafi la sekta ya misitu ikiwemo mbao na mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili tunawahamasisha wavunaji wa mkaa na watengenezaji wa mkaa kwamba pale tu ambapo wanahitaji kwenda kuvuna mkaa, basi watapata vibali maalum ili kuonyesha maeneo stahiki ambayo yanapaswa kuvunwa, lakini pia kuendelea kusimamia maliasili misitu kwa ajili ya maendeleo ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba wiki moja iliyopita ambayo tulikuwa kwenye Wiki ya Mazingira Duniani ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia alitoa tamko juu ya tuijandae sasa kuanza kuhama kutoka kwenye matumizi ya nishati ya mkaa na kuni twende kwenye nishati mbadala ya gesi. Aliagiza taasisi mbalimbali vikiwemo vyuo, mashule, mahospitali na magereza kwamba tuendelee sasa kuhamasisha wananchi waanze kuhama kutoka kwenye matumizi ya mkaa na kuni, tuelekee sasa kwenye kutumia gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kupunguza ukataji wa miti holela, lakini pia pale panapo umuhimu sana wa uvunaji wa mkaa, basi utoke kwa vibali, si kama ambavyo sasa hivi wananchi wamekuwa wakijichukulia kwa namna ambayo si stahiki sana na inasababisha sasa uvunaji unakuwa ni holela, miti inakatwa ovyo na mwisho wa siku itasababisha jangwa litokee hapa nchini na tutaonekana sasa sisi kwenye usimamizi wa maliasili misitu kwamba tumelegea kidogo. Kwa hiyo niwaombe sana na katika hili tuendelee kuwaelimisha wananchi, ye yote yule ambaye anahitaji kwenda kuvuna mkaa, basi apate kibali aelekezwa na eneo ambalo anapaswa kwenda kuvuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitapenda kuongelea kwenye eneo la utalii, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwenye eneo hili, wametupanua mawazo mengi na wametupa michango mingi sana ya kwenda kuboresha

kwenye sekta ya utalii. Tumeyapokea mawazo yao, lakini nitapenda tu kuwakumbusha kwamba, sisi kama Watanzania, nitaomba sana uzalendo uanze na kwetu sisi. Nikisema hivyo, naamini kabisa utalii ukianza na sisi wenyewe, tutachangia pato kubwa sana hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalendo uanze na sisi Wabunge tuliomo humu ndani na kwa ridhaa yako, nitaomba baada ya kumaliza Bunge lako hili Tukufu, tumeandaa safari, Wabunge tuwe mfano, Wabunge wazalendo naamini wote humu tuko ni Wabunge wazalendo tutembelee maeneo yetu ya vivutio na sisi tuwe mabalozi namba moja wa kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Naamini kabisa sisi wenyewe tukiwa wazalendo, utalii utakua kwa kasi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeandaa mikakati mingi ya ku-*promote* utalii na vivutio viliiyomo hapa nchini na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba baada ya Bunge hili nadhani wataanza kuona tu amshaamsha zitakazokuwa zinaendelea. Pia tulikuwa tumeshaandaa mipango mikakati ya kukutana na watu mbalimbali wakiwemo Waandishi wa Habari. Hata hivyo, tuna mkakati wa kusambaza vipeperushi mbalimbali hasa kwa wale ambaao wanapokea wageni wetu wanapoingia hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikatolea mfano, kwa mfano, tunaweza tukaandaa hata vipeperushi kwa hawa vijana wetu au wananchi ambaao wanapokea wageni wetu kutoka nje ya nchi, wakawa na vipeperushi maalum lakini pia wao wenyewe kwa uzalendo kama Watanzania, pale ambapo unambeba abiria ye yote yule aliyetoka nje ya nchi mueleze kwamba tuna Mlima Kilimanjaro, tuna hifadhi, tuna malikale, tuna kila aina ya vivutio hapa nchini. Kwa hiyo ile elimu wakati unampeleka kule anakoenda kupumzika, anakuwa tayari ameshaanza kujua kwamba Tanzania ina vivutio vya namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutasambaza vipeperushi ambavyo vitasaidia pale ambapo abiria wa

kutoka nje ya nchi anaingia ndani ya nchi, basi ataonyeshwa *Ngorongoro crater* kopo wapi, kama ni Serengeti iko wapi, lakini pia ataonyeshwa vivutio mbalimbali vinavyotokana na malikale. Hii yote ni kuhakikisha kwamba mgeni ye yeyote anayeingia hapa nchini, basi aelezwe Tanzania ina mazao gani ya utalii ambayo yatahamasisha yeye aende kwenye kutalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda pia kuongelea kwenye *swahili tourism*, hili nalo litakuwa ni eneo mojawapo la kuhamisha utalii, ambapo tutandaa vitu mbalimbali ikiwemo maonyesho ya mavazi, lakini pia tutaanda matamasha mbalimbali ya vyakula yya asili, ngoma na utalii wa utamaduni. Haya yote ni maeneo ambayo tumejipanga, sisi kama Wizara kuhakikisha kwamba sekta hii ya maliasili na utalii inakuwa kwa kasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo tuna uhitaji wa kuonyesha ubalozi katika maeneo yetu, naweza nikaja kwenye wilaya mojawapo nikataka kucheza hata zile ngoma zetu ili kuhakikisha kwamba utalii wa utamaduni unakua, tushirikiane kwa pamoa kuhakikisha kwamba tunauendeleza utalii wa Tanzania na vivutio vyake vilivyomo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda pia kuongelea eneo la miundombinu; ni wahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hili tumezingatia bajeti hii mtakayoipitisha ninyi kuhakikisha kwamba maeneo yote yenye vivutio yanapitika kwa ufasha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeandaa bajeti ambayo itakidhi kulingana na maeneo yote ambayo yana changamoto ya miundombinu. Kwa hiyo hifadhi zote na maeneo yote ya malikale tumezingatia. Tutawaomba tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tunapopitisha bajeti hii basi muipitishe tu vizuri mkiamini kwamba tunakwenda kutekeleza na kuhakikisha kwamba miundombinu itapitika na watalii waweze kuingia hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuliongelea ni kuhusu mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wamependa kuyaongelea kuhusu ufunguzi wa mageti. Eneo hili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, mtoa hoja. (*Makofi/Vigelegele*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa sisi wote uhai na afya na kutuwezesha kuendelea kuwatumikia Watanzania kuititia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kuendesha mjadala huu vizuri kabisa. Pia nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Kamati nzima ya Maliasili na Utalii kwa hotuba yao na ushauri wao. Katika hotuba yao wametoa mapendekezo 14 ambayo Wizara imeyapokea kwa mikono miwili na tunaahidi kwamba mapendekezo hayo tutakwenda kuyatekeleza kwa kushirikiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wabunge 78 ambao wamechangia hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini pia Wabunge 16 ambao wamechangia kwa maandishi. Hoja zao, michango yao na maelekezo yao tumeyapokea na kuahidi kwamba ushauri wote walioutoa tutautumia ili kuboresha utendaji wa Wizara hii na hatimaye kuleta tija kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niongelee mambo machache sana ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni migogoro iliyopo kati ya wahifadhi na wananchi. Imetamkwa hapa kwamba wananchi kadhaa wamefariki, lakini niseme pia na wahifadhi 12 wamefariki. Roho hizi za Watanzania ni nyingi sana, sina mamlaka hayo lakini ningekuwa nayo ningekuomba Bunge lako Tukufu lisimame angalau kwa sekunde 15 kuwakumbuka Watanzania hawa ambao wamefariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Rais mama Samia haipendi kuona mwananchi wake yejote anakufa kwa sababu yoyote ile. Sisi kama Wizara ya Maliasili na Utalii hatufurahishwi na jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, mmesema hapa kwamba wananchi wengi wamefariki kutokana na migogoro kati ya wahifadhi na wananchi, lakini nami nimesema hapa askari 12 wameuawa pia katika migogoro hiyo. Tufike sehemu tuseme sasa inatosha. Tutafute ufumbuzi wa suala hili na ufumbuzi ni wa kwetu wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, sisi kama Wabunge tuelimishe wananchi wetu kwamba maeneo ya uhifadhi tusiingie kufanya shughuli nyingine, lakini hata tutapokamatwa na hao askari tusilet *resistance* ambayo inasababisha mapigano na baadaye kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara tumeanza kuchukua hatua; hivi ninavyoongea askari wetu 61 tumewafukuza kazi. Hivi ninavyoongea askari 40 wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi. Moja kati ya kazi za kwanza ambazo mimi na Naibu Waziri tulifanya ni kwenda Ifakara kufukuza kazi askari watatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wetu ni rahisi sana; tukipata malalamiko yenyе ushahidi usiokuwa na shaka, sisi tunaitisha *parade* na tunamfukiza huyo askari kwa aibu na fedheha. Kwa sababu hatupendi askari ambaye amepata mafunzo anakiuka miiko ya kazi yake. Tunachohitaji ni ushirikiano toka kwa wananchi, ushirikiano toka kwa Waheshimiwa Wabunge na sisi kama Wizara tunahakikisha tukipata ushirikiano huo suala hili limekwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwashauri wananchi wetu, chanzo cha migogoro hii mpaka kuuana wakati mwingine ni rushwa; askari wetu wanaomba rushwa ili waingie kulima, askari wetu wanaomba rushwa ili waruhusu wafugaji waingie. Sasa ile pesa ya rushwa ikiisha anataka aongezewe rushwa, ndipo mgogoro unapoanza. Wananchi tukatae kutoa rushwa kutoka mwanzo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namba yangu mimi na namba ya Mheshimiwa Naibu Waziri na namba ya Katibu Mkuu ziko wazi kwa mtu ye yeyote kupokea malalamiko yoyote yenyе Ushahidi ili tuweze kuchukua hatua. Ninaamini suala hili sasa linakwenda kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhakikisha kwamba nidhamu ya askari wetu hawa inakaa vizuri, kwa sababu hivi sasa bado zile Kanuni za Jeshi Usu hazijasainiwa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba nitasaini kanuni hizo Jumatatu ili kuanzia tarehe Mosi, Julai, askari atakayekiuka miiko yake ya kazi haendi kwenye mahakama za kawaida, anakwenda kwenye mahakama za Kijeshi na anafukuzwa kazi mara moja. Kwa hiyo hii tunaamini italeta sana ufumbuzi kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeongelewa suala la vitalu hapa na ushauri mwingi umetolewa. Naomba niseme tumepokea ushauri huo wote. Hata hivyo, niongeze kitu kidogo tu, kwamba Wizara hii imekuwa na desturi ya kubadilisha Mawaziri kila baada ya miezi 18 na chanzo kikubwa cha Mawaziri kubadilishwa ni mfumo wa zamani wa

ugawaji wa vitalu ambao ulikuwa umegubikwa na wingu kubwa la sintofahamu, rushwa na upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo mpya uliowekwa wa kielektroniki umekuja kutibu matatizo hayo. Jambo lolote jipya haliwezi kuwa *perfect a hundred percent*, litakuwa na dosari hapa na pale. Tusichukue dosari hizo kubomoa mfumo huu mpya ambao una uwazi, una ushirikishwaji, unaleta wadau wapya kwenye sekta hii na unaondoa rushwa. Turekebishe matatizo hayo taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu ambao umeshaanza kutumika katika minada minne tumeweza kuuza vitalu 12, lakini vitalu hivyo 12 ambavyo vimeuzwa vimetuletea fedha ambayo inatusaidia sasa kwenda kujenga madarasa. Inatusaidia sasa kwenda kujenga hospitali, inatusaidia sasa kwenda kujenga barabara na la muhimu zaidi tunasaldia kwenye ujirani mwema kati ya uhifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Festo hapa amesema kule Kitulo anataka ujirani mwema; fedha inatoka hapa. Nimhakikishie Mheshimiwa Festo kwamba hilo jambo litakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pia *performance* ya vitalu imeshuka. Ilianza kushuka kabla mfumo huu haujaingia. Kilichosababisha kushuka kwanza ilikuwa ni katika nchi za wenzetu ambako watalii wengi ndio wanatoka, hasa Marekani, walianza kuweka zuio ili hizi *trophies* zisiende. Walivyozua kutokana na harakati za wapigania haki za Wanyama, tukajikuta kwamba soko la *trophies* kule Marekani likashuka, likishuka na uwindaji wao unashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Marekani walifungua, lakini baada ya Marekani kufungua hivi juzi *European Union* nao wametoa azimio la kuzuia *trophies* zisiingie huko. Sasa siyo jambo letu sisi peke yetu, tumeungana na nchi nydingine zote za *SADC* tunafanya mchakato ili kuondoa zuio hilo. Haya pamoja na ugonjwa wa *Covid-19*

ndiyo yamechagia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa utalii wa uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Serikali yetu imeanza kuchukua hatua stahiki kabisa na hatua madhubuti kupambana na ugonjwa huu wa *Covid-19*. Tunaamini tutakavyoweza kuweka sawa suala la *Covid-19* na kuondoa hili zio la kutoka *European Union* na kuboresha mfumo huu wa uwindaji wa vitalu wa kielektroniki tutaweza kupandisha tena *performance* ya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda huu mfupi mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara tumeshakutana na wawindaji na vyama vyao mara tatu. Tuliitisha mkutano Morogoro, siku nzima tumeshinda nao, asubuhi mpaka jioni. Tumeongea nao tumepata maoni na maoni yao ni muhimu sana katika kuboresha utendaji wa Wizara. Tunaomba tuwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hili nalo tunakwenda kuliweka sawa kabisa, na tutaboresha kuondoa sintofahamu yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja mahususi kabisa kutoka kwa Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge, wakili msomi. Hoja yake iko kwenye mawanda mawili; moja, alisema kwamba sheria hiyo haipo; pili, akasema sheria hiyo ni ya uonevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikubaliane naye labda kwenye hiyo hoja ya pili, lakini ya kwanza sheria ipo. Sheria ya Wanyamapori, Kifungu cha 116 kinasema; Sheria ya *TANAPA* Kifungu cha 28 na Sheria ya *TFS* Kifungu cha 95, ila tunahitaji kuwa na mjadala wa eneo hilo ili tuweze kuliboresha zaidi, ili kuondoa kelele na malalamiko kutoka kwa Watanzania hao wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kazi hiyo ni kazi ya Bunge hili Tukufu, ndiyo kazi yake kushughulikia sheria kama hizi, kuzirekebisha, kuzitunga na ndiyo maana sisi tuko humu ndani kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo Mheshimiwa Olelekaita, wakili

msomi, ambaye mimi huwa nawaasiliana naye sana, karibu sana tuje tuongee hili. Naamini pia tutaliweka sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la wanyama wakali na waharibifu sambamba na kifuta jasho. Juzi hapa tulifanya semina kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanatoka kwenye maeneo hayo kwa lengo la kuwapa uelewa nini chanzo cha tatizo hili.

Niseme, nashukuru sana mjadala wa leo unaonesha kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wametambua chanzo ni nini. Baada ya kutambua chanzo ni nini sasa, tujielekeze tutawezaje kuondoa changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya kuondoa changamoto hii ni moja tu; turudi kwenye mpango bora wa matumizi ya ardhi. Vijiji, halmashauri na Wizara; haya maeneo tuyaainishe. Wakati mwingine wananchi wanaingia kwa sababu hawajui; ameshajenga, ameshalima ndiyo anajua kwamba hii ni shoroba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni wakati kuanzia kwenye vijiji, kuanzia kwenye halmashauri na nasema halmashauri kwa sababu sisi wote humu ni Madiwani. Kwa hiyo kwenye halmashauri zetu tukatoe kipaumbele kwenye kitengo cha maliasili katika halmashauri. Kwa sababu kila halmashauri ina kitengo cha maliasili, lakini hatukipi umuhimu unaostahiki. Imesemwa hapa wana mabunduki ya zamani, hawana risasi, hawana usafiri, lakini wako chini ya halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama Wabunge, ambao pia kama Waheshimiwa Madiwani, tulichukue jambo hili kwa umakini mkubwa sana. tutakavyorudi kwenye Mabaraza yetu ya Madiwani tujiulize ni kwa kiasi gani tunaweza kuimarisha kitengo cha maliasili ili kupunguza kadhia hizi ambazo zinajitokeza. Tukishazipunguza sasa ndipo tutaweka mchakato zaidi wa kuweza kuangalia kwamba zile chache zinazoweza kuwezekana tuweze kufanya vipi katika jambo zima la kifuta jasho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi kwa ufanuzi mzuri ambao ameutoa. Yeye ni Mbunge mzoefu na ni *Senior Minister*. Jambo hili la migogoro ya mipaka alilifanyia kazi vizuri sana, yeye ndio aliongoza Kamati ile ya Mawaziri nane; amefanya kazi nzuri iliyotukuka, kilichobaki ni utekelezaji wake tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kurudia aliyojasema, lakini niongeze jambo moja. Katika zile hekta ambazo zimefutwa, kuna hekta mahususi 29,000 kwa ajili ya wafugaji. Tutakwenda kuzigawa hekta hizo ili wafugaji wawze kupunguza kadhia yao. Najua haitaondoa kabisa tatizo lao, lakini tutaweza kupunguza. Ili tatizo liondoke kabisa tunapanga uelimishaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ndaki, ameshalombwa Wizara ya Maliasili na Utalii tufanye mkutano wa Kitaifa wa pamoja wa Maliasili pamoja na Mifugo. Mkutano huo unakuja kuanzia sasa mpaka Oktoba tutakuwa tumeshaufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongelewa hapa kuwa watu wameshinda kesi lakini mifugo yao haijulikani ilipo, hawajakabidhiwa. Nchi hii inaongozwa na utawala wa sheria na sheria inatafsiriwa mahakamani. Mtu akienda mahakamani ameshinda kesi lazima apate kile alichokishinda mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaahidi Waheshimiwa Wabunge na niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, tutafuatilia kesi zote hizi ili haki za wale walioshinda kesi mahakamani zisipote. Tumelichukua jambo hilo kwa umakini wa hali ya juu na niwaahidi tutakwenda kutekeleza. Kama ambavyo tumekuwa tukipokea maombi ya Wabunge na kutekeleza kwa haraka na hili tutalitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kesho nimealikwa kutembelea kwenye majimbo la Wabunge wawili na nakwenda baada ya bajeti hii. Hiyo yote ni kuonesha kwamba pamoja na kwamba Wizara hii ni muhimu sana

katika uchumi, lakini pia ina umuhimu katika mustakabali na maslahi ya wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeongelewa suala la WMAs na wewe unalifahamu vizuri sana kwa sababu ulikuwa *consultant* wakati hili jambo linaanzishwa. Kwenye hilo kwa sababu ulikuwa ndio mwanzilishi wa hili, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wakupigie makofi kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna WMAs 38 lakini ambazo zinafanya kazi ni 22 tu, hizi 16 zimekuifa. Labda niseme WMAs ni nini; *WMA* ni kifupi cha *Wildlife Management Area*, kwamba Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi iliona ni bora na ni vyema kukabidhi madaraka ya kusimamia wanyamapori kwenye maeneo ya vijiji kwa wananchi kupitia Serikali za vijiji. Vijiji kwa mkusanyiko kadhaa vinatengeneza kitu kinaitwa *authorized association*. Wakitimiza masharti yyale wanapata usajili, wakipata usajili wanafanya uhifadhi na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo ambazo zinafanya vizuri sana kama ile ya Ikona. Imeonesha wanataka kufikia mapato ya shilingi bilioni 2.6 kwa mwaka. Sasa angalia, hiyo ni *WMA* moja inapata fedha hiyo, lakini wengine wameingia kwenye migogoro ya uongozi, wameshindwa kuhifadhi na ukishindwa kuhifadhi wanyama wanatoweka na wawekezaji wanakimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hizi 16 ambazo wameshindwa kufanya majukumu yao, wanyama wametoweka na hali imekuwa ni ngumu, ndizo ambazo tumesema Wizara tunaziangalia kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeponga pia ku-build capacity na kuendelea kuwa karibu na hizi WMAs kwenye utendaji. Kuwashauri zaidi kwa sababu kuna wengine wameingia kwenye mikataba ya kiunyonyaji ambayo haiwasaidii. Tunarudisha kwenye mfumo sasa tuweke mikataba mizuri ili hizi zote 22 ziweze kufanya vizuri na hatimaye zile 16 tuzirudishe kwenye mstari stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja mahususi pia zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Moja, tumepokea maombi mengi sana ya kuhusu vibali nya kuvuna kwa wananchi ambao walilima katika maeneo ya hifadhi kimakosa, walikuwa wamezuiwa. Kama nilivyosema wakati wa kulima kuna kuwa na makubaliano na wakati wa kuvuna wanataka kuwe na makubaliano mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kupitia Bunge lako hili Tukufu naomba Wizara itoe maelekezo, hayo makubaliano ya rushwa hatuyataki. Naagiza leo wananchi wote ambao walilima katika maeneo ya uhifadhi, waruhusiwe kuvuna kwa kibali maalum. Maelekezo haya ni kwa nchi nzima, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge hakuna haja ya kuja kuomba tena jambo hili tumelitolea maelekezo mahsusni kwa nchi nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kibali mahsusni kwa mamlaka ile husika kwa sababu unapoingia kwenda kuvuna unaingia eneo la hifadhi kwa hiyo unapewa kibali. Baada ya kibali hicho tunawaomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie, wasirudi tena kulima kwenye maeneo hayo, ili mwakani tusilijadili hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Asenga aliongelea kwamba pale Mang'ula kuna kona moja kali sana ambayo inasabababisha ajali, Watanzania wanafariki na ikiinyooshwa ile kona inakula eneo la hifadhi la mita 50. Kubadilisha mpaka wa hifadhi ni Mamlaka ya Mheshimiwa Rais, lakini naomba nijivilishe kilemba cha ukoka, niagize pale mkandarasi anyooshe zile mita hamsini, nitaenda kumwombwa msamaha Mheshimiwa Rais kwamba nimeingilia mamlaka yake na abariki maamuzi hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mkandarasi yule anyooshe pale ili tupunguze ajali kwa Watanzania ambao wanafariki. Bahati nzuri kona ile naifahamu kwa kuwa nimesoma Ifakara, lakini nimeoa kule, naenda kusalimia wakwe kila siku na naona madhara ya kona ile. Kwa hiyo hili

nalo naomba, watendaji wa Wizara wamenisikia utekelezaji wake huo uanze leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imegawa namba 14 *hotlines* kwa ajili ya kupokea malalamiko ya wananchi kutokana na wanyama wakali, hiyo yote ni kusaidia kupunguza kero hii. Namba hizo ni za bure, ukipiga wala huchajiji, tunaomba kuititia Bunge lako Tukufu, tuwaambie watanzania wote, ambao wana matatizo ya kukabiliana na wanyama wakali, watumie namba hizo kutoa taarifa ili askari wetu nao waweze kufika kwenye eneo husika kwa haraka kabisa, tutaendelea kuzisema namba hizo kwa wananchi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongeleta hapo hoja mahsusini ya miundombinu ya Burigi - Chato, mimi nimetembelea, nimefika nimejionea tunahitaji kuboresha miundombinu ya Burigi - Chato na bajeti hii ndiyo imebeba fedha za kuboresha miundombinu ya Burigi - Chato kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Oscar ukiipitisha bajeti hii tume-*solve* tatizo la Burigi - Chato, tushikamane twende kumaliza tatizo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufanuzi ambao nimeutoa kwa hoja zote ambazo zimewakilishwa na Wabunge hapa, pia hoja ambazo Wabunge wamezitoa kimaandishi na sisi tutazijibu pia kimaandishi na kuzileta kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana wewe, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao na maelekezo yao, niwaombe sana sasa tupitishe bajeti hii ili twende kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. (*Makofi*)

Sasa sijaelewa hayo makofi ni ya nini, lakini nataka kuamini wale waliokuwa wanataka ufanuzi wameahirisha. (*Makofi*)

Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 69 – WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*.....Sh. 4,471,563,700

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Waziri na Wabunge mbalimbali wameomba ufanuzi, tutaanza na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru na nipongeze kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri. Nataka kupata ufanuzi kidogo tu na Mheshimiwa Waziri atusaidie, Wabunge wengi wakati wa michango wamezungumzia juu ya habari ya upungufu wa watalii kuja nchini. Hii ni sambamba na wengine waliozungumza juu ya namna gani utaratibu wa kusafirisha viumbe hai inaweza kuwa ni sehemu mojawapo kubwa itakayoendelea kuchangia leo, kesho na keshokutwa kufanya watalii wengi zaidi wasije.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini msimamo wa Serikali kuhakikisha jambo hili sasa haliendelei isipokuwa kwa sababu na makusudi maalum yatakayofanya jambo hili litokee. Nakushukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, uafanuzi.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Stanslaus Mabula kwa hoja zake hizo mbili nzuri. Hili la kwanza tumelieleza na tutaendelea kulieleza, Wizara imekuja na mkakati mahsuswi wa kuongeza idadi ya watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tunaongeza mazao ya utalii ili tuwe na aina nydingi za utalii. Tumesema kwenye bajeti *speech* na tumeongea kwenye michango ya Wabunge kwamba; tutaongeza utalii wa fukwe, utalii wa mikutano, utalii wa utamaduni, lakini nilisema kwenye hotuba yangu kwamba tunaenda kwenye utalii wa michezo na pia utalii wa matamasha mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitolea mfano, tamasha moja kubwa na zuri, tamasha la *Tulia Marathon*, ambalo limekuwa likitumika kukuza utalii katika maeneo ya Mbeya na Nyanda za Juu Kusini. Mheshimiwa Festo na Waheshimiwa wengine kutumia tamasha la *Tulia Marathon* tunaweza tukatangaza utalii wa Kitulo na maeneo kule ya Kimondo na maeneo mengine ya Nyanda za Juu Kusini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaweza kutumia matamasha mengine kama matamasha ya *Kili Marathon*, *Rocky City Marathon*, Maji Maji Serebuka, *Kili Fairna* mengine yote. Mheshimiwa Naibu Waziri hapa amesema tumekuja na *Swahili Tourism Package* tuna *combine* lugha ya Kiswahili, utamaduni wa Kiswahili, mavazi ya Kiswahili yanaenda pamoja na utalii. Hii tunaamini kwamba tutazidi kuongeza idadi ya watalii wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaimarisha pia miundombinu, maana bila miundombinu kuwa mizuri

hautaweza kuwa na idadi nzuri ya utalii. Tunaongeza *marketing approach* kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmetushauri, tumechukua ushauri huo na tutahakikisha kwamba kwa juhudzi za pamoja utalii utaongezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, usafirishaji wa viumbe hai nje ulisimamishwa na Serikali tarehe 25 Mei, 2016, kwa sababu ilionekana madhara yake ni makubwa kuliko faida kiuchumi. Unaposafirisha hivi viumbe hai wanaovinunua wanakwenda kule nje vinakwenda kuzaliana, vikishazaliana wanatengeneza *zoo*, wakitengeneza *zoo* watalii wanaona kule na utafiti unafanyika kule. Kwa hiyo, tutakosa watalii na tutakosa watafiti kutoka nje kuja hapa na anayeathirika ni nani? *Tour guide* wa Kilimanjaro ataathirika, *Air Tanzania* itaathirika, wewe mwenye *guest house* utaathirika simuoni Mheshimiwa Nkuti hapa ana *guest house* ile, *guest house* yake itakosa wateja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpika chakula ataathirika na nchi itaathirika. Mwisho wa siku idadi ya watalii itapungua ndiyo maana Serikali ilisimamisha hili na tunakwenda sasa *ku-formalize* huo usimamishaji, tuwe tumemaliza jambo hili kwa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Naibu Waziri ambavyo wamejibu vizuri sana hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye hili ambalo Mheshimiwa Waziri amelieleza suala la mifugo ya wananchi ambayo bado inashikiliwa mpaka sasa hivi na jawabu ambalo amelitoa Mheshimiwa Waziri. Jawabu ambalo

amelitoa Mheshimiwa Waziri ni zuri, lakini sijaona *commitment* hasa sahihi ambayo inatupa imani kwamba baada ya kikao hiki hii mifugo ya wananchi tutaenda nayo nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo hii baada ya kukamatwa na wananchi kushinda kesi mahakamani walipoenda kufuatilia mifugo hawakuwakuta.

MWENYEKITI: Hawakuikuta. (*Makofi*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, hawakuikuta mifugo kwa sababu mbalimbali; moja, mifugo mingi ilikuwa kwa kukosa huduma ya maji, malisho, chanjo na dawa. Hawakuikuta mifugo kwa sababu mingine ilikuwa imeuzwa, kwa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti hoja yangu ni kwamba tunaomba *commitment* ya Serikali sasa kwa sababu Waziri amesema kwamba hana tatizo kuwarudishia mifugo wananchi hawa.

MWENYEKITI: Umeshaelewaka, kengele imegonga Mheshimiwa.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Ahsante sana.

MWENYEKITI: Sasa Waheshimiwa Wabunge zimebaki dakika kumi, tunaingia kwenye *guillotine*.

Katibu.

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource Management</i>	Sh. 4,471,563,700
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 871,894,700
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh. 1,753,433,900
Kifungu 1004 - <i>Government Communication Unit</i>	Sh. 396,144,100
Kifungu 1005 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 554,198,600
Kifungu 1006 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 559,009,700
Kifungu 1007 - <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 446,071,700

Kifungu 1008 - *Management Information Systems Unit*.....Sh. 1,007,558,500
Kifungu 1009 - *Research and Training Unit*....Sh. 15,986,839,000
Kifungu 2001 - *Wildlife*.....Sh. 346,071,428,600
Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping*.....Sh. 22,999,539,400
Kifungu 4001 - *Tourism*.....Sh. 14,691,265,100
Kifungu 4002 - *Antiquities Unit*.....Sh. 9,050,597,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 69 – WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....Sh. 33,701,696,000
Kifungu 2001 - *Wildlife*.....Sh. 111,893,184,000
Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping*.....Sh. 3,478,000,000
Kifungu 4001 - *Tourism*.....Sh. 700,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI – Mheshimiwa
Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa.
(Makofii)

TAARIFA

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako liliaka kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NAMAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji kwa utaratibu wetu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana. Naona na pongezi wameshamaliza Wabunge kabisa kwa hayo makofi waliyotoa. Pia hayo makofi yanaashiria ubunifu uliokuja na hii Wizara, bahati mbaya tu kwamba imekuja mwishoni, naamini watu wengi wangeigaiga hivi, lakini sasa nilikuwa nawasikiliza hapo wanasema wanajaribu kuhamasisha utalii wa ndani ni pamoja na hayo. (*Makofi/Kicheko*)

Nichukue fursa hii kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, wamepata pongezi nyingi kwamba wao ni wasikivu, wanawasikiliza Waheshimiwa Wabunge na mkisema mnawahitaji wanakuja kwenye maeneo yenu. Kwa hiyo hata hii bajeti imepitishwa kama mlivyoomba, kwa hivyo Bunge limeidhinisha hayo matumizi. Tunaamini kwamba mtaweza kufikia yale malengo ambayo mmeyaweka na changamoto mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezianisha wakati wa michango, tunaamini mtazifanya kazi. (*Makofi*)

Pia, tuwapongeze watalaam wenu ambao wapo hapa wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika eneo hili la Maliasili na Utalii. Ni Wizara

kubwa, ina mambo mengi, lakini bado wamejitatihidi kufanya vizuri, kwa hiyo tunawapongeza sana sana na tunawatakiia kila heri kwenye ukusanyaji maana ni Makadirio ya Mapato na Matumizi. Ukusanyaji lakini pia matumizi yake, tunaamini tutakapokuja safari ijayo basi mambo yatakuwa mazuri zaidi na changamoto mbalimbali zilizojitokeza mtakuwa mmezifanyia kazi. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo machache; moja, nakumbusha siku zote kwamba sisi hapa watu huwa wanatusikiliza na wanajua tunachosema ndiyo sahihi. Sasa kwa sababu huwa tunatazamwa na watoto wadogo, saa nyingine tujaribu kuangalia zile lugha zetu, wakati mwengine mtu anafanya masihara, lakini mtoto akishamsikia mtu mzima anafikiri ni sawasawa.

Umejengeka utamaduni wa mtu kupokea taarifa kwa mikono mitatu, sijui mikono saba, mikono mingapi, sasa mtoto atawea kuulizwa shulenii na yeye akajibu mikono ipo mingapi akajibu mitatu na anaweza akasema nilimsikia Mbunge. Kwa hiyo tujitatihidi kujizuia sana kwenye matumizi ya haya maneno.

Kingine ambacho nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri hapa ameeleza kuhusu wale wanaotakiwa kwenda kuvuna kwenye maeneo waliyokuwa wamelima ambayo hayaruhusiwi, ameweeka mkazo kwenye neno kibali maalum.

Sasa natamani utakapokuwa unatoa hicho kibali, utakapokuwa unatoa hayo maelekezo pengine kifafanuliwe, maana sasa kama mtu mkulima yupo pale anatakiwa afuate kibali sijui wapi itakuwa umeongezeka tena mtihani mwengine. (*Makof!*)

Kwa hiyo, nafikiri kwa sababu wao wanafahamu, hakuna mkulima ataenda kuvuna mazao ambayo siyo ya kwake, wao waruhusiwe kwenda kuvuna halafu baada ya hapo ifuate hiyo elimu kwa nguvu kabisa ili watu wapate mazao yao kama ambavyo umeelekeza. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo machache hapa; la kwanza, linahusu siku ya leo, siku ya leo Wabunge wote wanatakiwa saa 10.00 juu ya alama mchezo utaanza kuchezwa uwanjani Jamhuri. Wenzetu wa *Bunge Sports Club*, Ndugai Boys watakuwa wakicheza na timu ya TBC. Katika mchezo huu wananchi pia wanakaribishwa kwa sababu utaonyeshwa moja kwa moja na wakati huo wananchi watapata fursa ya kuona Wabunge wao kwamba hawako vizuri tu kwenye uwakilishi, lakini wapo vizuri uwanjani pia. (*Makofii*)

Pia *Bunge Queens* watakuwa, sasa sijui kama ni tunacheza mara mbili au mara ngapi, lakini hapa naambiwa tutacheza na *staff* wa *Benjamin Hospital*. Kwa hiyo wale wanaotutibu tibu, tunaenda kuwafunga pale. Nasema tunaenda kuwafunga kwa sababu mimi mwenyewe mchezaji, kwa hiyo mje muone mambo mazuri. (*Makofii/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, m jitahidi kuwahi kwa sababu mchezo huu utaonyeshwa moja kwa moja na wamepanga muda maalum inavyoonekana *Bunge Queens* wataanza kuchenza saa tisa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tujitahidi kwa haraka twende huko, lakini Wabunge mwende kushangilia ila na mimi niwatangazie wale vijana kutoka Mbeya Mjini watakuwa tayari kabisa kushangilia timu za Bunge kule Jamhuri, watakuwepo na mtaiona kazi yao nzuri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati hii kwamba kesho tarehe tano kutakuwa na mafunzo ya uongozi katika Kituo cha Mkutano cha *St. Gasper* kuanzia saa 5.00 asubuhi. Mwenyekiti anawaomba sana msiache kuhudhuria mafunzo haya Wajumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mwenyekiti hili tangazo ni leo, ni kesho, maana saa tano ishapita.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, ni kesho tarehe 6.

NAIBU SPIKA: Sawa. Haya tarehe sita, kwa hiyo kesho msikose Waheshimiwa Wabunge kwenda *St. Gaspersaa* 5.00 asubuhi.

Lipo pia tangazo linalotoka kwa Mwenyekiti wa *TWPG*, Mheshimiwa Shally Raymond, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanawake wote kwamba kesho saa 4.00 katika ukumbi wa Msekwa kutakuwa na Semina ambayo ni muhimu sana wanawake wote mhudhurie, kwa sababu kutakuwa na mafunzo muhimu ambayo wote tunayahitaji. Mgeni rasmi kwenye semina hii itakayofanyika Msekwa ni Mheshimiwa Job Yustino Ndugal, kwa hiyo mje wanawake, mje mumsikilize Mheshimiwa Spika anasemaje lakini pia na wavezeshaji wetu wengine. Kwenye tangazo hili naona nimetajwa na mimi kwamba ni mwezeshaji, kwa hiyo karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Tarehe 7 Juni, siku ya Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 8.00 Mchana Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 7 Juni, 2021, Saa Tatu Asubuhi)